

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Tatu – Tarehe 31 Januari, 2013

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu.

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, leo ni siku nyingine ya Alhamisi tunayo maswali kwa Waziri Mkuu, lakini kwa sababu tunamwona Kiongozi wa Kambi ya Upinzani akiwa hapa kwa mujibu wa taratibu zetu ataanza yeye kuuliza swali. Mheshimiwa Mbewe.

MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi.

SPIKA: Samahani kidogo Mheshimiwa Mbewe naomba ukae kidogo. Kwa mujibu wa taratibu zetu ile Kanuni inayosema iwapo Waziri Mkuu ana jambo analotaka kulieleza siku hiyo ya Alhamisi anaweza kutumia muda usiozidi dakika kumi na tano (15) kutoa hayo maelezo yake halafu tunaendelea na utaratibu wa kawaida. Kwa hiyo samahani sana Mheshimiwa Mbewe. Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kwa muda ulionitengea kutanguliza maelezo kidogo kutokana na umuhimu wa jambo linalohusu yaliyotokea pale Mtwara. Mheshimiwa Mbewe naomba radhi kwa kuku-*disturb* kidogo.

Mheshimiwa Spika, hali ya Mtwara kwa ujumla imekuwa ni shwari kwa ujumla kwa kipindi chote isipokuwa mnamo tarehe 27 Desemba, 2012 ndiyo kulitokea maandamano makubwa pale na kwa kweli kikubwa kilichojitokeza ilikuwa ni kupinga mpango wa Serikali wa kusafirisha gesi iliyosafishwa kwenda Dar es Salaam kwa bomba kwa ajili ya matumizi mengine. Lakini tarehe 25 Januari, 2013 na tarehe 26 Januari, 2013 kulitokea vile vile matukio ambayo sasa yalikuwa yameandalama na uvunjifu mkubwa wa hali ya amani katika Wilaya ya Mtwara pamoja na Masasi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na vurugu hizo yapo madhara yaliyopatikana ambayo nilidhani ni vizuri Bunge lako Tukufu nalo likaarifiwa. Mjini Mtwara tarehe 25 Januari, 2013 nyumba ya Mheshimiwa Mohammed Chikopa, Diwani wa Kata ya Chikongola iliharibiwa kwa kupigwa mawe, nyumba ya Mheshimiwa Hawa Ghasia inayoendelea kujengwa iliharibiwa kwa

kupigwa mawe vioo na madirisha pamoja na kuharibu milango ya nyumba na kuiunguza kabisa.

Nyumba ya *Assistant Inspector* wa Polisi Jumanne Malangahe, katika eneo la Sabasaba ilipigwa na kuchomwa godoro moja kwa kulimwagia petrol pamoja na kuharibu mita ya umeme ya nyumba pale Magomeni jengo la Kata ya Ufukoni lilichomwa moto pamoja na kuunguza nyaraka mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, gari la polisi lilihambuliwa kwa mawe na kuvunjwa kioo cha mbele, Mahakama ya Mwanzo Mtwara Mjini lilichomwa moto na kuteketea pamoja na kuteketeza nyaraka mbalimbali. Magomeni duka la Mohamed Ali Mchanyambe Diwani wa Kata ya Ufukoni lilivunja na kuibiwa mali mbalimbali zenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni thelathini (30,000,000/=), Magomeni *Grocery* nyumba ya Askari mmoja ilishambuliwa na kuibiwa vitu mbalimbali vyenye jumla ya thamani ya shilingi milioni moja laki nane na tisini na tano elfu na mia tano pamoja na fedha taslimu shilingi laki mbili na nusu (250,000/=).

Mheshimiwa Spika, Askari Shaban alijeruhiwa na kupigwa jiwe sehemu ya kichwani upande wa kulia karibu na jicho na hali yake kwa bahati nzuri inaendelea vizuri.

Tarehe 26 Januari, 2013 kule Masasi madhara yaliyotokea ni pamoja na kuungua na kuteketea kabisa ofisi za Manunuzi na nyaraka zote zinazohusu Manunuzi kwenye Halmashauri, kuteketea kabisa kwa ofisi ya Elimu ya Msingi na Nyaraka zote, kuteketea kabisa kwa ofisi ya Ukagazi wa Shule pamoja na nyaraka zote, kuungua kwa ofisi ya Maliasili na nyaraka zote, kuvunjwa kwa baadhi ya vioo vya madirisha ya ofisi kuu za Halmashauri yenyе majengo matatu, ofisi Kuu, ofisi ya Mipango na jengo la Mawasiliano, kuchomwa moto na kuteketea kabisa kwa magari 11 (kumi na moja) yaliyokuwa yamepaki katika *Yard* ya Halmashauri yakiwemo sita (6) ya Serikali mionganoni mwa magari hayo sita, mawili yalikuwa ni magari ya wagonjwa na moja lilikuwa ni gari jipya kabisa. Yapo pia magari matano ya watu binafsi ambayo yalikuwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, pia pipipiki nne na baiskeli moja za watu binafsi, zilichomwa moto magari saba yakiwemo ya Serikali matano(5) yenyе namba mbalimbali yalivunja vioo, kuvunjwa na kuharibiwa kabisa kwa vifaa vilivyonunuliwa kwa ajili ya ukarabati wa ofisi ya fedha vikiwa ni madirisha ya *alminium* na vioo vyote pamoja na vigae vyote viliungua. Kuvunjwa kwa geti kuu la kuingilia ofisi kuu ya Halmashauri, kuondolewa kwa mabati ya uzio wa jengo jipya linalojengwa na Halmashauri, kuungua kwa kumpyuta *desktop* tano, *laptop* nne, *printer* tano, *scanner* na *photocopier machine*.

Mheshimiwa Spika, pia kuungua kwa *strong room* ya Idara ya Maliasili yenyе silaha na kuteketeza bunduki moja, kuungua kwa shehena ya mbaо zilizokuwa zimekamatwa na kuhifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia matukio haya ya siku hizi mbili niliona ni busara na mimi niende Mtwara badala ya kuja Dodoma ili nione halisi ikoje, sababu ni nini, kazi ambayo nilifanya kwa muda wa siku tatu. Kwa hiyo, katika muda wa siku zile tatu niliamua kufanya mazungumzo na viongozi wa ngazi mbalimbali. Kwanza ilikuwa ni viongozi wa Vyama vya Siasa vya Upinzani pamoja na Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Wanaharakati, nikapata nafasi ya kuzungumza na Viongozi wa Madhehebu ya Dini ya Kiislamu na Kikristo, nikapata nafasi ya kuzungumza na Wafanyabiashara na Wakuu wa Taasisi mbalimbali zikiwemo Taasisi za Fedha za Manispaa ya Mtwara, Madiwani na Wenyevitи wa Serikali za Mitaa, Wajumbe wa Kamati za Siasa za Chama Tawala za Wilaya na Mkoa. Hii yote ilikuwa ni katika kunisaidia kujua hali ikoje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa kweli baada ya kuwasikiliza wote kilichojojiteza ni kwamba sababu kubwa ya mambo yaliyojiteza pale ni mwendelezo wa hoja iliyokuwa imejitokeza tarehe 27 Desemba, 2012 ingawa uliibuka katika mazingira tofauti na yale ya tarehe 27 Desemba, 2012. Kwa hiyo bado sababu kubwa ilikuwa ni kwa nini gesi hii ipelekwe Dar es Salaam badala ya kubaki hapa Mtwara itumike kwa ajili ya matumizi mbalimbali kuendeleza Mkoa.

Kwa hiyo, nilichukua nafasi ya kujaribu kueleza kinachoendelea ni nini katika miradi hii inayoenedelea pale, na kimsingi nilichowaambia ni kwamba gesi inayozalishwa Mtwara ni gesi ambayo ni sehemu ya rasilimali ya umma, ni gesi ambayo inapaswa kuwasaidia na kuwanufaisha Watanzania wote, lakini kwa kufanya hivyo tusifanye kwa kupuuza wale Wanamtware ambaao nao wana sehemu ya mchango katika eneo hilo kwa kuwa gesi hiyo inatoka katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia jambo hilo, nikawaeleza kwamba kwa mfumo ulivyo wa gesi, viwanda vingi vitajengwa Mkoani Mtwara pamoja na Lindi ambako nako vilevile gesi inapatikana na nikawahakikishia kwamba gesi inayotoka katika visima vya Msimbati, visima vinavyokadiriwa kuwa kiasi cha karibu futi za ujazo trilioni tatu mpaka tano cha gesi na ambapo sasa kiasi ambacho kinaendelezwa ni billioni kama mia mbili na sitini tu.

Kwa hiyo bado ni gesi nyangi na hiyo gesi ndio tunataka iletwe pale Mjini Mtwara kiwanda cha kusafisha gesi kinajengwa Mtwara sehemu ya Madimba. Kwa hiyo, mabaki yale yote ambayo ni rasilimali au ni malighafi kwa ajili ya matumizi ya viwanda mbalimbali karibu yote yatabaki pale Mtwara. Haya ndio yanayoleta mvuto kwa makampuni mengine kwa ajili ya kuwekeza katika viwanda vya mbolea na viwanda vingine kama hiki sasa cha Dangote ambacho tunatarajia kianze kujengwa mwezi wa Machi, kwa ajili ya uzalishaji wa saruji.

Mheshimiwa Spika, nikawaambia vilevile kwamba mtambo huo vile vile utaweza kutoa gesi ya kutosha ambayo itawezesha vile vile kuzalisha umeme na nikawaambia kwamba sasa hivi tunazungumza na baadhi ya makampuni ambayo yameonesha nia kuwekeza pale katika kuzalisha umeme wa kiwango cha megawati 600 kwa kuanzia na lengo ni kuiunganisha na Mikoa ya Ruvuma kuititia Songea ili kufungua ukanda wa maendeleo katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo kurudiarudia kwa vikundi mbalimbali nikabaini kwamba kwa kweli kilichokosekana ni maelezo thabiti ya kutosheleza kuwapa picha kamili juu ya nini hasa kitaendelea kutokana na hii miradi, na katika kumalizia, niliamua Mawaziri kutoka sekta mbalimbali, Waziri wa Viwanda kuititia Katibu Mkuu wake, Waziri wa Ardhi, Waziri wa Uchukuzi Waziri wa Elimu, Waziri wa Mambo ya Ndani nikawaita na watalaam kutoka kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*), wote walitaa maelezo mazuri ya kina kuonesha mipango ilivyo na faraja ni pale tuliposikia kwamba kuititia kituo cha Uwekezaji Makampuni 51 yameomba kwenda Mtwara kuwekeza katika mambo mbalimbali ya Kilimo, Usindikaji wa Mazao mbalimbali, upande wa Matumizi ya Gesi na maeneo mengine mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikatambua kwamba pengine jambo hili lilichanganywa kwa kukosekana maelezo sahihi. Lakini ni lazima tukubali kwa upande mwингine vilevile kulikuwa na upotoshaji mkubwa, mwингine unaweza kuwa ulikuwa ni wa kiuchochesi, mwингine unaweza kuwa ni ule ambaao mtu anafanya bila kujua. Maana kulikuwa na taarifa ambazo zilichangia sana kukuza tatizo kwamba gesi hii sasa imehamishwa inapelekwa Bagamoyo wakilihusisha na uwepo wa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Bagamoyo jambo ambalo siyo kweli. Wote tunajua kwamba kitovu chake ni Kinyerezi kama itaendelea itakuwa ni Tegeta.

Mheshimiwa Spika, kukawepo vilevile na maneno nayo ambayo si ya kweli kwamba mradi wa Bandari umefutwa haupo tena na wenyewe umehamishwa umepelekwa Bagamoyo, sasa wote mnajua kwamba mradi wa Bagamoyo ni kitu kingine, mradi pale wa Mtwara ni jambo tofauti. Kwa hiyo Dkt. Mwakyembe alisaidia sana kuliweka jambo hilo vizuri na wengi wakaelewa.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya pale katika majumuisho niliwaomba sana Wanamtware watambue kwamba sababu ya Serikali kuomba sehemu ya gesi ile iende ikasaidie Dar es Salaam ni upungufu mkubwa wa umeme tulionao kama Taifa na wao kama Watanzania tatizo hili ni lao vilevile. Kadri bidhaa zitakazokuwa zinazalishwa kwa bei kubwa Dar es Salaam zitarudi kuuzwa Mtwara na zitauzwa kwa bei kubwa. Pale Dar es Salaam viwanda viro vingi vinahitaji umeme wa bei nafuu sasa hivi tunatumia pesa nyingi sana kwa ajili ya kununua mafuta ya *diesel* pamoja na mafuta mazito kwa kuendesha mitambo, inatugharimu karibu shilingi trillioni 1.6 kwa ajili ya gharama hizi tu za mafuta. Tukitumia gesi pale tunaweza kabisa tukapunguza gharama hizi kutoka kiwango cha sasa hadi kufikia karibu kiasi cha senti saba mpaka nane cha dola moja katika gharama za uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa ujumla nilipata faraja kwamba uelewa ulipatikana kutokana na mazungumzo yetu na nikawaomba basi kuanzia pale sasa wote tutoke na mtazamo mmoja kujaribu kwenda kusaidia nchi kuielezea hali hii kwa kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, nataka nirudie kusisitiza niliyoyasema na ninawaomba Watanzania wote walione hili jambo kwa nia njema. Vurugu, uvunjifu wa amani hauna kitakachotusaidia kama Taifa na tunaijua mifano mingi, haitatusaidia kabisa. Ninawaomba Watanzania wote na ninawasihi sana watu wa Mtwara, maelezo niliyoyatoa ni thabiti, ni ya kweli, mpango ule ndivyo ulivyo, miradi ile ni kweli itakuwepo pale kwa sababu hakuna atakayeweza kwenda kuwekeza kiwanda cha mbolea nje ya eneo ambalo gesi inatoka kwa sababu kiuchumi haitakuwa na tija. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, viwanda karibu vyote vinavyotumia malighafi inayotokana na gesi, hata vile vya kutengeneza vitu kama plastiki na vifaa vingine kwa sehemu kubwa vitabaki Mtwara kwa sababu ndiko kwenye malighafi.

Kwa hiyo, imani yangu ni kwamba baada ya maelezo yale na jitihada tulizozifanya basi Wanamtware na Watanzania kwa ujumla watakuwa wamelielewa na ninaomba niwasihhi sana, kwa sababu mimi nilitoka pale nikijua tumeelewana, na jambo hili kusema kweli linapaswa kuwa kwa sasa limekwisha. Niwaombe Viongozi wenzangu wote ndani ya Bunge na Viongozi wa Vyama vya Siasa wote tuzungumze lugha moja inapokuwa kwenye suala la amani na utulivu kwa sababu halitamsaidia mtu ye yeyote kama ataendeleza vurugu kwa namna yeyote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nataka niwashukuru sana Wananchi wa Mtwara kuitia makundi yale ambayo nilikutana nayo, walikuwa wawazi, walionesha hisia zao, lakini kusema kweli baada ya maelezo tuliona wengi tulifika mahali pazuri na wote tulitoka pale kwa kweli tumefarijika na tulifurahi sana kwamba jambo hili limefika mahali pazuri.

Ninawaomba kwa mara nyingine kutambua tu kwamba Tanzania ni moja, rasilimali hizi zitumike kwa kadri itakavyowezekana kutupunguzia matatizo makubwa kama Taifa, lakini kufanya hivi tutaendelea kuzingatia vite vile kwamba Mtwara ambao wana nafasi kubwa hii, viwanda vite ambavyo havina mahali pa kwenda isipokuwa Mtwara, kazi kubwa waliyonayo pale ni kuhakikisha Mtwara inatulia, iwe ya amani, ili wasije wakatoa tena fursa ya wawekezaji kuanza kukimbia kutokana na hofu kwamba pengine kutakuwa na uvunjifu wa amani. Haya

matukio ya juzi tu tayari baadhi ya makampuni yamesitisha baadhi ya jitihada zao za kutaka kuwekeza pale, wengine wametuambia ngoja tusubiri miezi mitatu, wengine wamesema tutangoja mpaka hali itulie, tumejitahidi kuwahakikishia kwamba mambo ni shwari na yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, makampuni yanayotafuta gesi kule ndani ya bahari hasa kwenye kina kirefu, na yenewe yameshtuka baada ya matukio haya, sasa hii inaanza na sisi kutupa hofu kwa sababu jirani zetu Msumbiji wanazo huduma wanaweza kuzitoa kutumia Bandari yao na sisi walishakubali kuja kutumia Bandari ya Mtwara kwa shughuli zao zote, ukarabati wa meli, matengenezo ya meli, usindikaji wa gesi ile ya kimiminika ambayo itakuwa imegandishwa kidogo kwa ajili ya kusafirishwa na kuuzwa nje, kwa hiyo tusiikose fursa hii, tukiikosa kwa kweli itaturudisha nyuma kwa kiasi kikubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwapa pole kwanza wale amba wamepoteza maisha katika tukio hili, niwape pole Wabunge na Viongozi wengine wote amba mali zao zimeharibika kwa kiasi kikubwa sana, tutajitahidi kama Serikali kurejesha hali ya huduma kwenye upande wa Halmashauri zilizopata matatizo mapema iwezekanavyo ili Watanzania waendelee kupata huduma hizo. Tutiliangalia vile vile suala la wenzetu hawa amba wameharibiwa mali zao katika mazingira haya, tuone ni namna gani tunaweza tukawasaidia kuwapunguzia mzigo amba umetokana na hilo tatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, imani yangu ni kwamba jitihada hizi za kweli za Serikali basi zitatuwezesha kuendelea na majukumu yetu kama Taifa katika hali ya amani na utulivu. Nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii, nakushukuru sana Mheshimiwa Mbobe kwa kunivumilia kidogo, sasa niko tayari kwa maswali. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Waziri Mkuu kwa brief hii kubwa. Kwa hiyo, sasa nimwite Mheshimiwa Freeman Mbobe aulize swali lake la kwanza. Nadhani na wewe utatumia muda mfupi ili kusudi na wengine wapate nafasi pia.

MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru sana kwa maelezo ambayo ninaamini ni ya msingi na ya muhimu sana kwa Taifa. Lakini nitaomba swali langu nilielekeze hapo hapo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni dhahiri kwamba yaliyotokea Lindi na Mtwara yamesababishwa kwa kiwango kikubwa na *Political Mis-management*, pamoja na mawasiliano hafifu kati ya Serikali na wananchi, na ni dhahiri kwamba kauli za Viongozi mbalimbali wa Serikali na Chama cha Mapinduzi, vilichochea kwa kiwango fulani kujaza hasira ya wananchi. Na ni usuhuda ulio wazi kwamba baada ya wewe kwenda na kuona umuhimu wa kufanya mawasiliano ya moja kwa moja na wananchi wale umeweza kupata ufumbuzi angalau wa muda wa tatizo hili. Pamoja na mimi kuwapa pole sana wote walioathirika na maafa haya ni kwa nini sasa Serikali, isiwachukulie hatua za uwajibikaji Watumishi wote wa Serikali na wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama amba waliona viashiria vyote vya wananchi kutokuridhika na yaliyokuwa yanaendelea Mtwara na bado haikuchukuliwa hatua yoyote ya maana ya kufanya mawasiliano kama ulivyofanya wewe? Pili hapohapo Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kwa sababu gani sasa Serikali, isiweke wazi Mikataba yote inayohusu *Oil and Gas* ambayo imeonesha hofu kubwa sana kwa wananchi wa Lindi na Mtwara na hata kwa Tanzania kwa ujumla, ili mambo haya yaye wazi na kila mtu aweze kuyaona, kuondoa hisia ambazo pengine zinajengeta kwa kutokuelewa? (*Makof*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, ndugu yangu Mbewe. Kuhusu swali la kwanza, kitu nilichojifunza pale ni kweli, inawezekana analolisema kwa kiasi fulani linaweza kuwa lina mshiko. Lakini tukubali vilevile kwamba, vyama vya siasa kwa ujumla wake vimechangia sana katika kupotosha jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na tatizo lililoitokeza ni kwamba, kila mmoja kwa namna yake alilichukua na kulitafsiri kutegemea na malengo ambayo anataka kuyafikia katika eneo lile. Kwa hiyo, uko vilevile ukweli, wala sio siri, ushindani wa chaguzi zinazokuja na kwa hiyo, jambo gani ukilichukua sasa linaweza likakupa *Political mileage* lakini bila kujua kwamba, unaweza hata wewe usifike huko katika mazingira ya vurugu kama hizi. Kwa hiyo, mimi ninadhani kikubwa sasa tumefika mahali pazuri, kubwa lisiwe kutafutana uchawi, hapana; tutafanya kazi ya kuchunguza jambo hili kwa kina kujaribu kuona wapi tulikosea, wapi nani alifanya nini, lakini kwa ujumla wake kubwa iwe ni kwamba, hapa tulipofika basi tusirudi tena pale wote kwa ujumla wetu. Litatusaidia sana huko tunakotaka kwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili. Aah, hili la kuwawajibisha na nini, liko ndani ya uwezo wa Waziri Mkuu, liko ndani ya uwezo wa Rais. Tutaangalia mazingira tutaona kama yanahitaji hatua za namna gani. Lakini mimi kama ninavyotazama pale tutalaumiana wengi tu kwa sababu, jambo lile lilikuwa ni la watu wote pale. Kubwa tu iwe ni ile kwamba, huko tunakokwenda kwa upande wa Serikali, tunapokuwa na mambo makubwa kama haya ushirikishwaji wa jamii kwa ukubwa sana, ndio liwe jambo la msingi.

Mheshimiwa Spika, vema, umezungumza juu ya Mikataba na unaona kwamba, pengine ni moja ya kichocheo kikubwa sana katika jambo hili, ni namna tu tutakavyoleze. Mimi sidhani kama Mikataba ile ina mambo ambayo ni ya ajabu ya siri kubwa sana ambayo, haiwezi kutolewa ufanuzi watu wakajua ni nini kimo ndani, kinetengenezwaje, kinatakiwa kujibu hoja gani, kwa hiyo, kwa kweli, ni jambo tu ambalo tukikaa kwa utaratibu wa kawaida hata kuititia mfumo wa Kibunge tu, ni vitu vinavyoweza kupatikana mkavitzama, ilimradi tu tufuate utaratibu.

MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru sana kwa majibu yako, lakini hapa mwisho kidogo umekuwa *elusive*. Hukutaka kutoa Kauli kwamba, Serikali, inakiri Mikataba hii itatolewa wazi, umesema tunaweza, tunaweza, tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu uwe *firm* kwamba, Mikataba hii itawekwa wazi ili kuondoa utata na hofu ambayo wananchi wanaijenga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini wakati huohuo Mheshimiwa Waziri Mkuu, utakubali na utakiri kwamba, Serikali yenu inakuwa siku pale *pressure* ya wananchi inapokuwa kubwa? Kwa sababu, bila *pressure* ya wananchi, mambo yote mazuri ambayo yameelezwa yanayokusudiwa kufanywa Lindi na Mtwara, yalikuwa hayazungumzwi, hayana mawasiliano. Haya mambo yamekuja kuzungumzwa baada ya *pressure* ya wananchi; utakiri kwamba, sasa Serikali yako inakuwa siku baada ya *pressure*, ikiwemo maandamano? (*Kicheko/Makofii*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbewe, anajenga hoja lakini haina mshiko hata kidogo. Mimi naamini suluhu na jibu la kweli, si maandamano hata kidogo. Suluhu ya kweli pale ambapo jambo halieleweki ni watu kukaa chini mkaomba kupewa zinazohitajika, zikatolewa, mkazitumia kwa shughuli za maendeleo. Maandamano ukishayaendekeza mara nydingi matokeo yake huwezi ukayadhibiti ndio shida ninayoiona mimi kwa hiyo, ni vizuri hata kama unaweza ukasema pengine hiyo ndio njia ya kuishiniza, kuifanya tu, Serikali imekuwa siku muda wote. Mambo mangapi hapa yanafanya kwa njia hiyo, muda wote tumekuwa

tukisikiliza. Kwa hiyo, ni kitu tu ambacho nadhani ni cha kujiepushanacho kwa sababu, si kitu kizuri sana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini naona umerudia tena lile la Mkataba. Naomba niseme Mheshimiwa Mbewe, Serikali, ilikwishakubali kwamba, Bunge hili linayo fursa ya kupata Mkataba wowote, kubwa ni kufuata utaratibu kuititia Ofisi ya Spika. Spika, ataiarifu Serikali, Mkataba unaohitajika tutauleta utatazamwa kwa utaratibu tuliokulaliana. Sasa ukisema uanikwe maana yake unataka twende tukatoe kwenye magazeti na kwenye nini, mikataba nayo ina misingi yake kwa hiyo, ni lazima tuendelee kuiheshimu vilevile. Lakini hiyo, haina maana kwamba, watu wasipate kujua ni nini kimo kama wanaona iko sababu ya kufanya hivyo.

SPIKA: Ahsante, naomba tuendelee. Kwa hiyo, kwa dakika zilizopo, mnawenza kuona kwamba, nitawaita watu wachache sana. Nianze na Mheshimiwa Namelok Edward Moringe Sokoine.

MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, wenyeji wa Wilaya ya Ngorongoro, wamekuwepo pale kabla ya ukoloni na kabla ya eneo lile kutangazwa kuwa Hifadhi. Kwa hivyo basi, wana sababu ya kutumia rasilimali zilizokuwepo katika eneo lile, lakini Serikali, ilipitisha Sheria bila kuwashirikisha wananchi wa eneo lile ya kupiga marufuku kufanya shughuli zozote za kiuchumi, ikiwemo kulima bustani katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tulipata taarifa kwenye vyombo vya habari kwamba, wananchi wale wanateseka na njaa na hivyo kuwapelekea akinamama, watoto, kuteseka na njaa na hata baadhi ya watoto kulazwa katika Hospitali, wakiwa wamepata utapiamlo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, je, Serikali, wakati inatunga Sheria hiyo, ilikuwa ina mpango gani wa kudumu kwa ajili, ya wenyeji wanaishi katika eneo lile? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, sina hakika kama nimemwelewa vizuri kwa sababu, Morogoro ... Ngorongoro, ooh, sorry. Alikuwa anazungumzia Ngorongoro, nilisikia kama Morogoro. Samahani sana.

Mheshimiwa Spika, suala la Ngorongoro ni jambo ambalo pengine, suluhu ya kweli, labda ni kukaa na kulitazama tena. Kwa sababu, si jambo limeanza leo, ni jambo la muda mrefu. Ni jambo ambalo limekuwa likitazamwa kwa misingi ya kisheria kwa muda mrefu. Lakini moja ambalo unaweza kabisa ukaliona ni kwamba, kadiri idadi ya watu inavyoongezeka, shinikizo la hali ya maisha katika eneo lile na yenyeze inazidi kuongezeka. Ndio maana unaona sasa hivi kunajitokeza mahitaji ambayo inabidi kama Serikali, tukae chini tuone tunafanyaje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nikubaliane na Mheshimiwa Namelok kwamba, pengine kitakachohitajika hapa ni kuchukua muda kidogo kujaribu kulifanyia kazi, tuone Sheria zile zinasema nini, sasa hivi wanaishije, tulikuwa tukifanya nini muda wote katika mazingira ambayo wamekuwa wakikabiliana nayo. Halafu, tuone kama bado Sheria hizo ni *relevant* au bado ni za msingi au kama kunahitajika kuzirekebisha kidogo katika kujitahidi kukidhi mahitaji mapya. Ni lazima tukubali ni eneo nyeti kidogo na ni lazima tuone namna ya kushughulika nalo.

MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru sana kwa majibu yako mazuri. Kwanza, niipongeze Serikali, kwa hatua iliyochukua ya kuamua kupeleka mahindi mara baada ya kutangazwa. Lakini pia, niipongeze Kamati ya Ardhi, Mazingira na Maliasili, pia walikwenda kuona hali halisi inayoendelea ndani ya Ngorongoro. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, unafikiri ni muda gani tutachukua mpaka ufumbuzi huo utakapopatikana, wakati Watanzania wenzetu wanateseka na njaa? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, swali gumu. Ukisema itachukua muda gani, siyo rahisi sana kulijibu. Lakini mimi ninadhani kubwa hapa, kama nilivyosema, tukae chini tuliangalie suala zima kwa mtazamo ambao utajaribu kuwianisha maslahi yote ya wananchi, ya nchi, halafu tuone ni namna gani tutaweza kuondokana na hili tatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tunachofanya ni kujaribu tu kusaidia kujibу tatizo la sasa. Inapotokea kwamba, kuna njaa mahali tunajitahidi kusaidia, lakini ni dhahiri kwamba, hatuwezi kuendelea hivyo kwa muda wote. Kwa hiyo, ni lazima tufike mahali tuone suluhu ya kweli ni kitu gani.

MHE. MWIGULU L. M. MADELU: Mheshimiwa Spika, asante. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hali ilivyo sasa ni karibu kila Halmashauri, ina upungufu wa watumishi. Na Idara nydingi za Serikali, kama si zote, zina upungufu wa Watumishi wa Serikali, mpaka Tume ya Mipango ina upungufu wa Watumishi wa Serikali. Na wakati huo huo karibu kila mtaa kuna mwanafunzi aliyetoka chuo chenye heshima hapa Tanzania na wengine nje ya nchi, anatafuta kazi.

Sehemu nydingine kuna mtu mmoja anashikilia nafasi zaidi ya moja, yaani nafasi yake na anakaimu nafasi ya mtu aliyejkuwa anakaimu. Swali linakuja. Hawa vijana wanaotoka chuo wakienda kuomba kazi, wanaambiwa waje na uzoefu wa miaka mitatu (3) na zaidi. Swali la kwanza, ni kwa nini Serikali, inaruhusu upungufu wa Watumishi Serikalini, ilhali kuna wanafunzi inaowasomesha kwa gharama kubwa wako mtaani wanatafuta kazi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kama tatizo ni uzoefu, wanaambiwa waje na uzoefu wa zaidi ya miaka mitatu (3) ama minne (4), ilhali hakuna chuo kinachofundisha uzoefu. Ni kwa nini usitoe tamko leo kufuta kigezo hicho, wanafunzi wanapotoka chuo wanapoomba nafasi za kazi za kuanzia?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kumjibu ndugu yangu Mheshimiwa Mcemba, kama ifuatavyo; kubwa ni kweli tunakubali kwamba, uko upungufu wa watumishi kwa ujumla. Na upungufu mkubwa zaidi hasa uko kwenye eneo la Walimu, ambao ndio bado linatusumbua, ingawa tunaendelea zile jithhada za kujaribu kutoa wanafunzi wengi zaidi kwenye sekta hii ya elimu, kama tulivyosema mwaka huu tunatarajia kuajiri Walimu 25,000.

Lakini bado utakachokiona kwa upande wa Walimu ni kwamba, ongezeko la wanafunzi mwaka hadi mwaka na ongezeko la shule, litaendelea kuwa ni tatizo litakaloendelea kwa muda kidogo kabla hatujamaliza kabisa. Lakini juhudhi za kuendelea kuongeza udahili wa wanafunzi vyuo vikuu nadhani unakwenda vizuri kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa watumishi wengine, Sekta ya Afya nayo, bado haijakaa vizuri. Wizara ya Afya, inajitahidi kuongeza udahili wa wanafunzi katika eneo hilo, lakini bado kama mnavyojua mradi ule ni mkubwa, Zahanati kila Kijiji, Kituo cha Afya kila Kata kwa hiyo, *demand* ni kubwa kidogo, lakini nayo inasimamiwa inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa Idara nydingine, ninachoweza kusema kwa uhakika ni kwamba, tuko katika hali nzuri zaidi kuliko katika Sekta hizo mbili. Inawezekana kwenye Halmashauri moja moja kwa sababu moja au nydingine pakawa na upungufu zaidi, lakini kwa ujumla wake Idara nydingi katika Halmashauri nydingi hazina matatizo makubwa, tumejitahidi sana. Na wala si kweli kwamba, tunapoajiri kigezo hicho ndio tunakizingatia muda wote, hata kidogo; tumechukua vijana wengi sana tumewajiri moja kwa moja na wengine kwa kweli, uzoefu wanaupata wakiwa katika Halmashauri zenywewe.

Mheshimiwa Spika, na tunatambua kwamba, mahitaji kwenye Halmashauri, huwezi ukasubiri eti mpaka apate uzoefu, uzoefu anaupata wapi kama yeye mwenyewe ni mtu wa mipango na mipango iko ndani ya Halmashauri.

Kwa hiyo, tumeajiri wengi; tatizo tunaloweza kulikubali tu ni kwamba, inawezekana Sekta ya Umma, haitoshi kuwaajiri wote kama pengine inavyohitajika. Lakini hata hivyo, tutajitahidi kuangalia kwa karibu zaidi tuone wapi, labda kwenye Halmashauri yako kuna tatizo pengine maalum, tutajaribu kulikabili na kulimaliza.

MHE. MWIGULU L. M. MADELU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri Mkuu, lakini pia bado natambua kwamba, kuna tatizo kubwa la ajira kwa vijana na hili la uzoefu. Ni kwa nini, Serikali, isiandae mpango maalum wa kuwa inachukua vijana kwa ajili ya *attachment*, hata wakalipwa gharama za usafiri tu, ili wawe wanapata uzoefu na kuweza kutambua ujuzi wa mwanafunzi? Kwa sababu vyeti peke yake havitoshi kujua mwanafunzi ana uwezo gani wa kazi. (*Makofii*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, sawa. Nadhani ni ushauri mzuri tu, acha tutaungalia tuone namna ya kulitekeleza.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, muda wenyewe umekwisha. Lakini napenda kukushukuru sana kwa namna ulivyotuelimisha hasa kwa suala la Mtwara na machache haya uliyotueleza. Ahsante sana. (*Makofii*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, lakini naomba tu niseme. Nilisahau kidogo pale Mtwara Mjini, nyumba ya Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Ndugu Sinani na yenyewe ilichomwa moto; nilikuwa nimepitiwa kuitaja ile nyumba.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. (*Makofii*)

Katibu tuendelee na Maswali ya Kawaida.

MASWALI YA KAWAIDA

Na. 30

Kuboresha Huduma za Hospitali Teule - Ilula

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA aliuliza:-

Hospitali Teule ya Ilula – Itunda, Wilaya ya Kilolo, haina huduma muhimu kama vile chumba cha kuhifadhi maiti, mashine ya X-Ray na gari la kubeba wagonjwa.

Je, Serikali, ina mpango gani wa kutoa huduma hizi kwa wananchi wa Kilolo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibuu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Peter Mahmoud Msolla, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Hospitali Teule ya Ilula – Itunda, kwa sasa haina mashine ya *X-Ray*, chumba cha kuhifadhia maiti na gari imara la kubebaa wagonjwa. Hata hivyo, Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, tayari imewasiliana na Serikali ya Netherlands ambayo, imeahidi kupeleka mashine ya *X-Ray* mwezi Februari, 2013 katika Hospitali hiyo. Aidha, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) katika mpango wake limepanga kujenga chumba cha kuhifadhia maiti pamoja na Chuo cha Uuguzi Hospitalini hapo. Kipaumbele kilichowekwa kwa mwaka 2012/2013 ni ujenzi wa Chuo cha Uuguzi. Ili kutatua tatizo la gari katika Hospitali Teule ya Ilula – Itunda, Halmashauri katika Mwaka wa Fedha 2011/2012 iliwasilisha maombi maalum ya shilingi milioni 150 Wizara ya Fedha, lakini hazikupatikana. Aidha, katika mwaka huo, Halmashauri iliomba maombi maalum ya shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Kati ya fedha zilizombwa shilingi milioni 100 zilitolewa na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya unaendelea kwa awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yetu kwamba, mashine ya *X-Ray* ambayo imeahidiwa na Serikali ya Netherlands, kwa ajili ya Hospitali Teule ya Ilula – Itunda, itasaidia kupunguza changamoto za matibabu katika Hospitali hiyo wakati Serikali inajipanga kukabiliana na changamoto zilizobaki.

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa maeleo yake. Lakini pamoja na maeleo yake, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumweleza Mheshimiwa Waziri kwamba, Hospitali Teule ya Ilula – Itunda, ndio Hospitali pekee katika Wilaya nzima ya Kilolo. Hospitali hii vilevile iko katika eneo la Milima ya Kitonga, ambapo kunatokea ajali nyingi sana za magari na kimbilio la wote wanaopata ajali ni kukimbilia Ilula. Juu ya Netherlands, waliahidi kwamba, wangesaidia kujenga chumba cha maiti, iwapo tu *KKKT* wangeweza kuanzisha Chuo cha Wauguzi, jambo ambalo limeshindikana mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, maswali yangu madogo mawili ni kama ifuatavyo:-

(a) Je, Serikali, ina mpango gani wa dharura wa kuhakikisha na kunusuru huduma za Hospitali hii ya Ilula – Itunda?

(b) Je, Serikali, itakuwa tayari kuweka mipango ya kuimarisha Hospitali hii Teule ambayo inahudumia Wilaya nzima kuweka katika Bajeti ya mwaka 2013/2014, ili kusudi iweze kufanya kazi zake kama inavyotegemewa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mimi naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla tuliondoka naye hapa tukaenda katika Jimbo lake haya mambo yote anayozungumza ana hakika kwamba ninayafahamu na ninayajua na hii shida anayoeleza pale naifahamu kwa sababu nilikwenda nikaiona mimi mwenyewe kwa macho yangu.

Sasa tunazungumza habari ya mpango wa dharura, mpango wa dharura ni kwamba sisi tuliofanya pale kwamba ile ni Hospitali Teule. Hospitali ile siyo Hospitali ya Wilaya ni hospitali ya Kanisa la KKKT kwa hiyo ni katika mpango huo wa kuona kwamba je tunafanyaje ili tuwasaidie wananchi pale waweze kusaidika.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hilo kwamba tumelitumia hilo la Hospitali Teule ili tuweze kuondokana nalo ile Halmashauri ya Kilolo ni Halmashauri mpya. Ni katika hizi Halmashauri ambazo zilizanzishwa nyuma kidogo siyo hizi mpya. Kwa hiyo, tunachofanya ni kuimarisha huduma iliyopo katika Hospitali hiyo teule pale na hilo eneo la Kitonga analosema ni kweli zinatokea ajali pale ni sawasawa tunazungumza habari ya Kibaha pale matatizo yanayotokea pale.

Kwa hiyo ninachosema hapa ni kwamba sisi tunafikiri kwamba njia mojawapo ya kusaidia hapa ni kuhakikisha kwamba tunaimarisha huduma inayotolewa katika Hospitali teule iliyoko pale.

Mheshimiwa Spika, katika hili la pili ambalo anazungumzia la Bajeti hilo hakuna swali lolote la kuulizana hapa, sisi katika mfuko ule tunapeleka 25% ndio inayopelekwa katika mfuko. Kwa hiyo, hii itakuwepo katika Bajeti na katika mipango na tutahakikisha kwamba tunashirikiana naye.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo nataka nikuahidi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba tutasogea karibu zaidi kuona kwa karibu zaidi ukiambiwa mahali ambapo hakuna chumba cha maiti unaweza ukajiuliza kwamba wanafanya fanyaje inapotokea hali ya namna hii kwa hiyo tutasaidiana na Mheshimiwa Peter Mahamudu Msolla ili tuweze kuona kwamba tunawasaidiaje hata katika hali hiyo ya dharura anayozungumzia.

SPIKA: Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, swali lingine la nyongeza.

MHE. SELEMANI SAIDI JAFO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa niulize swali la nyongeza changamoto inayoikabili Hospitali ya Ilula ni sawa sawa na changamoto inayoikabili Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe na katika kumbukumbu za *Hansard* mwaka jana nilikuuliza swali langu la msingi nilipata majibu ya kwamba ukarabati ungefanyika wa kutosha katika suala zima la ujenzi wa chumba cha maiti pamoja na kuikarabati Hospitali ya Wilaya.

Sasa nataka kupata ahadi ya Serikali leo, nini mpango wake katika kuhakikisha Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe inaimarishwa katika huduma za Afya?

SPIKA: Akiwa na majibu sawa asipokuwa nayo sawa pia, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema hapa ni suala la ukarabati sasa suala la ukarabati ni suala la *priority*. Najua kwamba Mheshimiwa ana swali lake ameuliza *sijali-study* vizuri nitakwenda kuangalia, nitakwenda kuangalia pia na suala la ukarabati. Ukarabati ni suala ambalo Halmashauri yenye we inatakiwa iangalie, tutaona jinsi ambavyo tutasaidiana katika jambo hilo.

SPIKA: Ahsante sana, naomba tuendelee na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa sababu muda wetu haujaka vizuri, Mheshimiwa James Francis Mbatia, atauliza swali linalofuata.

Uhifadhi wa Mazingira Endelevu

MHE. JAMES FRANCIS MBATIA aliuliza:-

Baadhi ya miundombinu ya majitaka iliyopo katika Jiji la Dar es Salaam, Mji wa Mtwara, Tanga, Lindi, Mwanza, Musoma, Bukoba na kadhalika ni vyanzo vya uchafuzi wa Mazingira ya baharini na maziwa yaliyopo katika miji hiyo:-

Je, Serikali imeweka mifumo kazi gani endelevu na sahihi ya utekelezaji wa uhifadhi wa Mazingira endelevu?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Francis Mbatia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya maji na usafi wa mazingira katika miji mikuu ya Mikoa zimeainishwa katika Sheria ya *Water Supply and Sanitation Act* Namba 12 ya mwaka 2009 iliyofuta Sheria Namba 8 ya mwaka 1997 kwa lengo la kusambaza maji safi na uondoaji wa maji taka.

Kabla ya mwaka 1997 karibu miji yote haikuwa na miundo mbinu ya maji taka isipokuwa miji michache ya Dar es Salaam na Tanga iliyorithi miundombinu kutoka kwa mkoloni. Hivyo kuanzia mwaka 1998 Serikali ilianza kuhimiza uendelezaji wa huduma za uondoaji wa maji taka kwa kurakabati, kujenga mabwawa na kutibu au kusafisha maji taka na kuunganisha mabomba ya maji taka kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na gharama kubwa za kujenga miundombinu hiyo miji kumi na moja tu ikiwemo Dar es Salaam, Tanga, Arusha, Moshi, Morogoro, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Tabora, Songea na Iringa ndiyo yenyewe miundombinu ya maji taka. Aidha kuititia *program* ya uendelezaji wa sekta ya maji Serikali imeweka mifumo kazi imara na endelevu kuimarisha huduma za maji taka kwa kuboresha mifumo iliyopo na upanuzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwekezaji unaoendelea Serikali inaendelea kuhamasisha wananchi kuhifadhi mazingira yanayozunguka vyanzo vya maji na kusimamia viwango vya maji taka yanayotiririka kwenye vyanzo hivyo.

Serikali kuititia *NEMC* inafanya tathimini ya kila mwaka kwa mamlaka za maji Mjini na kwa wawekezaji, kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 kipengele cha 122 mpaka 129 pamoja na Kanuni Namba 8 Kanuni za Ubora wa Maji ya mwaka 2007 zimeeweka sharti la Maji Taka kutibiwa au kusafishwa kwa kiwango stahiki kabla ya kumwaga na umwagaji Maji Taka karibu na maeneo ya maji safi au sehemu ya burudani kama ufukweni yaani *recreation areas* umepigwa marufuku.

Mheshimiwa Spika, hivyo ningependa kuendelea kusitiza na kuhimiza Halmashauri za Miji, Wafanyabiashara wakubwa kwa mfano mahoteli, migodi na viwanda kuboresha mifumo ya Maji Taka kwa kuzingatia Sheria na kanuni za mazingira ili kulinda afya ya binadamu pamoja na mazingira.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa James Francis Mbatia, swali la nyongeza.

MHE. JAMES FRANCIS MBATIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa upo ushahidi wa wazi wa kwamba baadhi ya miji yetu hususani Jiji la Dar es Salaam Maji Taka yanayotoka kwenye baadhi viwanda yanaenda moja kwa moja baharini ikiweko eneo la Mikocheni daraja la Mlalakua na maji taka haya yanayoenda baharini yana Kemikali za Zebaki na Kemikali hizi zinaliwa na samaki wadogo na samaki wadogo wanaliwa na samaki wakubwa na samaki wakubwa wanaliwa na binadamu. Hivyo husababisha madhara makubwa kwa binadamu na ikiweko na uchafu unaotoka kwenye baadhi ya mahotelii Dar es Salaam moja kwa moja ikiingia baharini bila kuchujwa.

(a) Je, athari zinazotokana na uzembe wa wenyewe viwanda hivi kutokuhifadhi mazingira inavyotakiwa kwa mujibu wa sheria wamechukuliwa hatua gani za wazi ili kukomesha ukiukaji mkubwa wa sheria?

(b) Suala la mazingira ni suala la hulka, ni suala la tabia tupongeze Manispaa ya Moshi kwa kuwa safi na kuendelea kuwa kielelezo.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kutoa elimu kuanzia kwenye shule, majumbani na kutumia vyombo vya habari ili kila mwanadamu aweze kujua umuhimu wa kulinda mazingira kuanzia yeeye binafsi, familia yake na jamii kwa ujumla?

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, ahsante sana nichukue fursa hii kuwatachia heri ya mwaka mpya na ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa James Francis Mbatia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana naye kwamba ni kweli upo ushahidi kwamba baadhi ya Maji Taka yanamwagwa baharini lakini niseme tu kwamba tunapajaribu kuangalia haya matatizo lazima tuyaangalie kwa kina kwa sababu kuna biashara nyingine zilanzishwa kabla ya sheria ya mazingira ya mwaka 2004.

Kwa hiyo, lazima tuangalie kwa mapana na ndiyo maana tunapajaribu kuwaelimisha watu tunaainisha pia na wale watu ambao waliweka miradi yao au uwekezaji kabla ya mwaka 2004 kwamba wajitahidi kuweka miundo mbini ya kusafisha maji taka na ndiyo maana *NEMC* inafanya ukaguzi mara kwa mara kuhakikisha hata wale ambao walikuwa wameweka uwekezaji kabla ya sheria waweze kutekeleza na kuweka miundombini inayolingana na sheria ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, kama mlivyoona mwishoni mwa mwaka jana mimi mwenyewe pamoja na Naibu Waziri, pamoja na Halmashauri tulikuwa pamoja kufanya ukaguzi kwenye mahotelii na ratiba hii ni *Action Plan* ya mwaka huu 2013. Kwa hiyo tutaendelea kufanya ukaguzi na wale wote ambao watakuwa wamekiuka Sheria ya mazingira basi hatua zitachukuliwa mara moja itafanyika palepale kama tulivyo fanya *Double Tree*. Kwa hiyo tutafunga kwa muda fulani mpaka watakapotekeliza sheria ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, suala la mazingira ni kweli ni tabia kwa sababu ni suala linalohusu zaidi usafi. Mimi nichukue fursa hii tu kuwapongeza Halmashauri ya Moshi kwa tabia nzuri waliyoyijengea. Lakini sasa hivi siyo Halmashauri ya Moshi tu tangu tuanze kampeni ya usafi kuna Miji zaidi. Kwa mfano Arusha wamefanya vizuri na wanaendelea kufanya vizuri, Mwanza wanajitahidi, Morogoro, Iringa na Ruvuma. Kwa hiyo kuna Mikoa ambayo tayari imeshaanza ku-*pick up*. Kwa hiyo mimi niwaombe tu Halmashauri zote tujifunze hii tabia ya usafi na tutekeleze sheria ya mazingira kama inavyotutaka. Ahsante sana. (*Makof*)

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi pamoja na majibu mazuri ya Waziri lakini tunashuhudia wenyewe katika Jiji la Dar es Salaam katika mitaa ya Kariakoo, mitaa ya ile barabara ya akiba, mvua kidogo tu au wakati mwagine hata mvua hamna lakini maji takya yanavyobubujika katika yale makaro kiasi kwamba harufu inakua ni kero katika Jiji.

Je, pale pale usoni kwa nchi kuhusu mazingira Serikali inatuambia nini katika kuboresha mazingira ya Jiji la Dar es Salaam iwe kiangazi iwe wakati wa mvua?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, ahsante sana napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli miundombinu yetu siyo mizuri sana lakini Halmashauri za Dar es Salaam pamoja na Manispaa, pamoja na Jiji la Dar es Salaam wanajitahidi kiasi wanachowenza tatizo kubwa la Dar es Salaam ni mlundikano mkubwa wa Wananchi na mitaa yetu kutokopangwa sawasawa.

Lakini kwa jitihada za Wizara ya Ardhi inajitahidi sana kufanya marekebisho na ukipita katika mitaa mbalimbali mimi mwenyewe binafsi nimeshapita kuna miradi mbalimbali inayoendelea ya kupanua mitaro ya maji machafu.

Pia kuweka miundombinu, kwa hiyo siyo kitu ambacho kinaweza kufanya kwa mara moja lakini Serikali ina mikakati kwa kushirikiana pamoja na Halmashauri zetu za mitaa kuweza kuweka miundombinu yetu vizuri kama ambavyo swali la msingi lilivyojibiwa. Ahsante sana.

SPIKA: Tunaendelea muda jamani, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, atauliza swali hilo kwa niaba yake Mheshimiwa Yahya Kassim Issa.

Na. 32

Balozi za Tanzania Nje ya Nchi

MHE. YAHYA KASSIM ISSA (K.n.y. MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID aliuliza:-

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inahusiana Kibalozi na nchi mbalimbali duniani:-

- (a) Je, jumla ya mabalozi waliopo nje ni wangapi?
- (b) Je, kati ya mabalozi hao wangapi wanatoka Zanzibar?
- (c) Je, kuna balozi ngapi za heshima na zipo nchi gani?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina jumla ya Balozi 32 nje ya nchi na balozi ndogo yaani *Consulate General* tatu. Kati ya balozi 32 tunao mabalozi 27, wanaoiwakilisha nchi yetu nje ya nchi. Aidha balozi zetu sita kwa sasa hazina mabalozi kwa kuwa mabalozi waliokuwepo wamestaafu hivi karibuni baada ya muda wao kuisha na wengine bado hawajateuliwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, sehemu (b) kati ya mabalozi 27 walioko hivi sasa mabalozi wanne ndiyo wanaotoka upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, sehemu (c) Tanzania vilevile inabalozi za heshima katika baadhi ya nchi ambazo hatuna ubalozi na katika baadhi ya miji muhimu kibiashara na kiuchumi. Mpaka sasa Tanzania ina balozi za heshima 16 kama ifuatavyo;

Mbabane, Swaziland; Tel Aviv, Israel; Damascus, Syria; Illinois, Marekani; Istanbul, Uturuki; Ankara, Uturuki; Hong Kong, China; Perth, Australia; Melbourne, Australia; Adelaide, Australia; Osaka, Japan; Rotterdam, Netherlands; Luanda, Angola; Mauritius; Cyprus na Ufilipino. Ahsante sana.

SPIKA: Swali la nyongeza Mheshimiwa Yahya Kassim Issa.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni suala la muungano na tumeona kwamba katika mabalozi 27 Zanzibar inamabalozi wanne.

Je, kuna utaratibu gani mahususi juu ya uteuzi wa Mabalozi?

Kwa kuwa inasemekana katika Balozi zetu baadhi ya ofisi ambazo wanaishi mabalozi wetu si sehemu zetu si ofisi zetu.

Je, Serikali inautaratibu gani wa kujenga ofisi zetu ili kuepukana na gharama?

SPIKA: Nadhani umemuelewa, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sehemu (a) kwamba kuna mpango gani mahususi wa uteuzi wa mabalozi kwa vile Wizara ya Mambo ya Nje ni moja ya Wizara za Muungano. Hakuna utaratibu mahususi ni busara za mamlaka ya uteuzi ambayo ni Mheshimiwa Rais ambayo yeye mwenyewe anazingatia kwa busara zake kwa kutambua kwamba hii ni Wizara ya mambo ya muungano lakini hakuna muongozo maalum unaomtaka labda katika uteuzi huo Wazanzibari wawe wangapi na Watanzania bara wawe wangapi.

Mheshimiwa Spika, sehemu (b) swali la pili ni kwamba ni kweli tunaupungufu wa majengo katika balozi zetu mbalimbali na tumekuwa aidha tukijenga au kununua

kutegemeana na upatikanaji wa fedha lakini hali imekuwa siyo nzuri katika bajeti ya maendeleo. Ahsante sana.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kuwa balozi nyingi zinawakilishwa na mabalozi wanaume na kwa kuwa sisi wanawake wa Tanzania tunaweza wengi wetu kati yetu ni wasomi wazuri.

Je Serikali itakubaliana nami sasa balozi hizi ziwekwe sawa kwa sawa wanawake na wanaume fity fity? (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri karibu, huo unaitwa ushabiki wa kijinsia.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa spika, ningemshauri Mheshimiwa Mbunge na hili kama hakuwahi kutoa pia alipendekeze katika Tume ya mabadiliko ya Katiba ili liingie kwenye Katiba mpya.

SPIKA: Tunaendelea mabalozi ni mabalozi kwanza balozi zenyewe hazijakaa vizuri. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa David Ernest Silinde atauliza swali hilo.

Na. 33

Watuhumiwa Kulipa Mafuta ya gari la Polisi

MHE. DAVID ERNEST SILINDE aliuliza:-

Jeshi la polisi limekuwa na vituo vidogo vijijini ambavyo vimeduwa vikisaidia zoezi la usalama:-

(a) Je, kwa nini washtakiwa wakikamatwa vijijini hususani Jimbo la Mbozi Magharibi wamekuwa wanatakiwa kulipia gharama za mafuta ya gari la Polisi, posho za mgambo na chakula kwa watuhumiwa bila risiti kwenda katika jeshi la Polisi?

(b) Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya hali hiyo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde Mbunge wa Mbozi magharibi lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za jeshi la Polisi, jukumu la kulinda na kusafirisha watuhumiwa kutoka eneo moja kwenda jingine liko mikononi mwa Polisi mpaka wanapofikishwa mahakamani.

Mheshimiwa Spika, suala hilo siyo jukumu la raia kulipia gharama za mafuta ya usafiri, posho ya mgambo wala chakula kwa mahabusu anayetakiwa kusafirishwa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyininge.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo na kwa sababu ya ufinyu ya Jeshi la Polisi, nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kutumia nafasi zenu kwa kushirikiana na

Halmashauri za Majimbo yenu kutenga fungu la ulinzi na usalama kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura 287 na 288 sheria iliyorejewa mwaka 2002.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa Serikali imekiri wazi kwamba, Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi zinakataza wananchi kulipia mafuta, gharama za chakula pamoja na posho za migambo. Je, ikitokea Kituo chochote cha Polisi ama Askari Polisi yoyote kakiuka kanuni hizo kwa mara nyingine wananchi wachukue hatua gani juu ya jeshi hilo ama Askari Polisi huyo?

Pili, kwa kuwa kuna Vituo vingi sana nya Polisi vimeduwa vikikiuka Kanuni za Kudumu za Polisi. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuviamuru vituo hivyo ama Askari hao waliochukua fedha za wananchi waziresheshe mara moja ili kurudisha imani kwa jeshi hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ya kwanza kama itatokea mimi nafikiri Jeshi la Polisi ni moja kati ya Taasisi ambazo zimeundwa kwa muundo mzuri, unaanza Kata, unakuja Wilaya, unakuja Mkoa. Kwa hiyo, ikitokea kwenye eneo la chini, basi taarifa hii ipelekwe kwenye ngazi inayofuata ya kiutawala ya Jeshi la Polisi na ushahidi na hatua zinachukuliwa.

Pili, Vituo vingine pengine vimehusika katika kuwatoza wananchi fedha na narudia kusema kwamba, hiyo itakuwa ni kinyume cha utaratibu na kama kuna ushahidi wa kutosha wa hili kabla hatujazungumzia kurejesha, tungeupata tukaufanya uchunguzi na kama tutagundua, tutaamua kuchukua hatua zinazofaa.

SPIKA: Na kwa sababu yule alisema kwa niaba ya wananchi wa Mbozi, basi kuna Mbunge mwininge wa Mbozi, Mheshimiwa Zambi.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swalii moja. Ni ukweli kwamba, swali la msingi lina ukweli kwamba wakati mwininge Askari Polisi hulazimika kuwataka mahabusu au wanaokamatwa walipe gharama za mafuta. Lakini hiyo husababishwa pia na ukweli kwamba bajeti ya Polisi ni ndogo sana kwani wakati mmoja tumeambishiwa Polisi wanapewa lita 200 tu za mafuta kwa mwezi mzima. Je, katika mazingira hayo Serikali haioni sasa ili kutolidhalilisha Jeshi la Polisi, Polisi wapewe mafuta ya kutosha kwa ajili ya kufanya kazi katika maeneo yao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, bajeti ya mafuta kwa ajili ya Jeshi la Polisi ni ndogo na ni kweli kwamba, mafuta wanayopewa pengine yasingetosheleza. Lakini pamoja na yote hawatakiwi kukiuka sheria za kazi. Kwenye hili la kuongeza bajeti, bajeti tunaiomba Bungeni na naomba Wabunge tushirikiane ili kuhakikisha kwamba bajeti ya mafuta ya Jeshi la Polisi inakuwa ya kutosha. (*Makofii*)

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tatizo la Vituo nya Polisi kwa mfano cha Mbozi, linafanana kabisa na tatizo la Vituo nya Polisi nya Hungumarwa na Ngudu; je, Serikali inafikiri vituo hivi vitafanya vipi kazi kama wanashindwa kuwawezesha hata kuwapatia mafuta ya kutumia?

SPIKA: Mbona unarudia swalii? Basi naomba Mheshimiwa Naibu Waziri ujibu tu hivyo hivyo.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, mahitaji ya Vituo nya Polisi yana umuhimu mkubwa katika kuhakikisha kwamba wananchi wanasogezewa huduma kule. Ni kweli kwamba, kuna changamoto ya kutosheleza kila mahitaji ya kuendesha kazi kwa

ufanisi, naomba tushirikiane kuhakikisha kwamba, bajeti inaongezeka na njia nyingine za halali zinatumika katika kuhakikisha kwamba vituo hivi vinapata mafuta ya kutosha. Polisi Jamii njia hiyo ipo lakini pia tumeanzisha Mfuko amba wananchi wote wanaweza kuchangia katika kuliondoa tatizo hili kubwa. Wabunge ndiyo tunaopitisha bajeti, nawaomba tuhakikishe kwamba tunavipa Vituo vya Ngudu na vingine mafuta ya kutosha.

Na. 34

Mashambulio Dhidi ya Viongozi wa Dini

MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA aliuliza:-

Hivi karibuni kumejitokeza tatizo la viongozi wa dini kushambuliwa na watu wasiojulikana huko Zanzibar ambapo katibu wa Mufti Sheikh Fadhili Soraga alimwagiwa tindikali na kujeruhiwa vibaya sana na Padri Ambrose Mkenda wa Kanisa Katoliki kupigwa risasi:-

- (i) Je, Serikali imechukua hatua gani za kuwalinda viongozi hao wa kidini dhidi ya mashambulio hayo?
- (ii) Je, ni watu wangapi wamekamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria?
- (iii) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwashudumia kwa matibabu na huduma nyingine wahanga hao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mbunge wa Dole, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hivi karibuni kumejitokeza matukio ya mashambulizi ya watu wenye nyadhifa za kidini hapa nchini. Uchunguzi wa awali umeonesha kuwa matukio haya hayana mahusiano yoyote na suala la kidini bali yalifanywa na wahalifu kwa malengo yao binafsi. Kufuatia matukio hayo, Jeshi la Polisi lilichukua hatua ya kuimarisha doria na kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama katika maeneo mbalimbali. Aidha, kazi ya kuwafuatilia na kuwakamata wahalifu sambamba na kuelimisha na jamii juu ya umuhimu wa kuwafichua wahalifu unaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika matukio hayo mawili jumla ya watuhumiwa watano walishakamatwa, watuhumiwa watatu wakihuishwa na tukio la kumwagiwa tindikali Sheikh Fadhil Soraga, Katibu Mufti wa Zanzibar na wawili wakihuishwa na tukio la kupigwa risasi Padre Ambrose Mkenda. Mara upelelezi utakapokamilika, wahutuhumiwa hao watafikishwa mahakamani. Aidha, wahanga wote wawili walipatiwa huduma za matibabu na Serikali.

MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na maswali mawili, ni ukweli kwamba nchi yetu sasa hivi inaelekea pabaya kwamba vurugu za kidini zimejitokeza sehemu mbalimbali nchini. Serikali ina kauli gani kupitia kwa Naibu Waziri kuhusu suala hili ambalo linaelekea kuondoa amani ya nchi yetu.

Pili, kwa vile katika maelezo ya Waziri Mkuu hivi punde tu asubuhi, ameelezea wahanga wa Mtwara watapata fidia kwa vitu ambayo vimeharibiwa. Je, taasisi za dini ambazo mali zimeharibiwa kutokana na matukio mbalimbali, Serikali itatoa fidia kwa taasisi hizo? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, la kwanza ni kwamba, Serikali haitaki na haitavumilia machafuko yoyote ambayo yanahusishwa na dini na nawaomba wote wanaoshiriki katika mambo haya kuyaacha mara moja ili Tanzania iendelee kuwa kisiwa cha amani Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, kuna mikakati mbalimbali ambayo pamoja na tamko hilo tunachukua, lakini kubwa ni kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata elimu, elimu ya kujua umuhimu wa amani na hasara pale tutakapoikosa. Lakini jambo lingine ambalo litaendelea kufanyiwa kazi ni kuchukua sheria kwa wale ambao watathubutu kuchezea amani tuliyonayo. Tunaendelea pia kwa sababu mambo haya hasa yanayohusu taasisi za dini yanahusiana na pengine mkono kutoka nje. Chunguzi tunazifanya kuhakikisha kwamba, nani wana fadhili kama zinafadhiliwa kutoka nje na hatua za kufuata zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwamba, tunafanya uchunguzi kwa zile taasisi ambazo zitaonekana kujihusisha na mambo haya kwa mfululizo na tukizigundua basi kwa sababu zimesajiliwa tutachukua hatua za kuwafutia usajili.

Kuhusu fidia, fidia katika makosa ya jinai kwa mujibu wa sheria haitangazwi moja kwa moja na inatokana na amri ya Mahakama. Kwa hiyo, upande huu na kwa sababu tuna watuhumiwa tayari tuiachie Mahakama ikisema walipwe fidia pia itaelekeza nani alipwe fidia na zitatolewa.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa muda umebakia dakika kumi tu na maswali yamezidi. Sasa tujielekeze Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, Mheshimiwa Rita Louise Mlaki atauliza swali linalohusika.

Na. 35

**Mfumo wa Kujunga na Vyuo Vilivyosajiliwa
na *NACTE***

MHE. RITA L. MLAKI aliuliza:-

Serikali iliruhusu uanzishaji wa vyuo vya watu binafsi vinavyotoa certificate na diploma, na vyuo vya Serikali kama *IDM*, *IFM* na *CBE* havitoshi kulingana na wingi wa wanafunzi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaelekeza wanafunzi walio wengi ambao wana sifa za kujunga na vyuo vikuu lakini hawakuchaguliwa na vyuo vikubwa ili wajunge na vyuo vilivyosajiliwa na *NACTE*?

(b) Je, Serikali ina mpango gani kuititia *NACTE* kuwasaidia wanafunzi kujunga na vyuo vilivyosajiliwa na *NACTE* kama ilivyo kwa *TCU* inavyosaidiwa wanafunzi wanaokosa kujunga na vyuo vikuu vya Serikali kujunga na vyuo binafsi?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani za kuhamasisha mfumo huu wa kuingia chuo kikuu kuititia "Technical Education" ambao wengi hawaufahamu na hatimaye kurudia mtihani mara kadhaa?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Mbunge wa Viti Maalum, swalii lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Baraza la Elimu ya Ufundu yaani *NACTE* huandaa na kutoa orodha ya vyuo vyenye sifa ili kuwawezesha wahitaji wanafunzi kuvitambua vyuo vyote hivyo kwa lengo la kuepusha kuijunga na vyuo visivyo na sifa vikiwemo vile vya binafsi. Aidha, kwa kuwa vyuo hivyo vinajiendesha kiutendaji yaani *full autonomous* vina wajibu wa kujitangaza vyenyewe ili wale wenye sifa ambaa hawakuchaguliwa na vyuo vya ufundu vikubwa waweze kuijunga na vyuo hivyo.

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu, *NACTE*, kupitia tovuti yake, majarida mbalimbali na maonyesho huwaelekeza wanafunzi wanaokosa nafasi kwenye vyuo vikubwa kuomba kuijunga kwenye vyuo viliviyosajiliwa na *NACTE* vikiwemo vile vya binafsi.

(b) Mheshimiwa Spika, Baraza la Elimu, *NACTE* kwa kushirikiana na Tume ya Vyuo Vikuu yaani *TCU* hutoa taarifa za udahili kwa wanafunzi kuhusu vyuo vya elimu ya ufundu vyenye nafasi vikiwemo vya binafsi ili kujaza nafasi zilizo wazi baada ya awamu ya kwanza ya udahili kukamilika. Kwa njia hii wanafunzi wenye sifa ambaa hawakuchaguliwa awamu ya kwanza kupata nafasi ya kudahiliwa kwenye vyuo vya ufundu kama ilivyo kwa vyuo vikuu bila kujali ni vyuo vya umma ama vya binafsi.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha utaratibu wa kuelimisha wananchi wote kuhusu mfumo wa kuijunga na chuo kikuu kupitia *Technical Education* kwa kutumia fursa zinazojitokeza kwenye maonyesho mbalimbali kupitia tovuti ya Wizara, vyombo vya habari, vipeperushi na majarida yanayoandalialiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu yaani *NACTE*.

MHE. RITA L. MLAKI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, lakini kabla sijaauliza maswali yangu mawili ya nyongeza naomba *ku-declare interest* kwamba mimi ni mdau wa elimu. Nimeitika wito wa Serikali wa kuanzisha vyuo binafsi, nimeanzisha chuo kinachoitwa *Dar es Salaam Institute of Business Management. (Makof)*

Mheshimiwa Spika, ili sera hii nzuri sana ambayo Serikali imeleta ya kuanzisha vyuo binafsi iweze kufanikiwa, kuna wanafunzi zaidi ya 80,000 wanaomba vyuo binafsi kama *CBE, IFM, IDM* kwenda kuchukua mafunzo ya *Certificate* na *Diploma* na kati ya hao wanaoweza kuingia ni asilimia 20 tu. Je, Serikali haioni kwamba, kuna umuhimu wa kutoa *circular* kwa vyuo vya Serikali kama hivi vya *CBE, IFM, IDM* na vinginevyo kuwa wakishachagua wale wanafunzi wao waliohitimu, waliobaki wayapeleke haya majina *NACTE*, ili *NACTE* iweze kuyapanga au kuyatoa kwa vyuo binafsi ambavyo vimesajiliwa na vinakubalika na pia iwasaidie *NACTE software* ya kuweza kufanya kazi hiyo?

Mheshimiwa Spika, pili, binafsi nimetembelea zaidi ya wanafunzi 6,000 na wazazi 6,000 waliomaliza *form four* ili kuwaelekeza kwamba, wanaweza wakaenda chuo kikuu kupitia *diploma* na nimekuta wengi sana hawajui.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia tovuti, vyombo vya habari, pamoja na matangazo mbalimbali haioni kuwa umefikia wakati sasa bado hao wazazi na wanafunzi

hawajajua, itumie kupeleka hizi habari kwa kuititia mashulenii wanakomaliza *form four* na *form six?* (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Mbunge hapa ni sahihi kabisa, lakini nataka tu kufafanua kwamba hivi vyuo vinavyosajiliwa na *NACTE* kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba ni *full autonomous* kwamba, vinajitegemea katika kusajili vyenyewe na vinajiendesha vyenyewe na hata kujitangaza vyenyewe kwa ajili ya wanafunzi kuijunga kwenye vyuo hivyo kama wanavyofanya shule za sekondari za binafsi, wanatoa matangazo kwenye redio, magazeti, majarida mbalimbali halafu wanafunzi wanajunga pale kutokana na ubora wa shule yenewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata hivi vyuo vinavyosajiliwa na *NACTE* vinatakiwa kutumia mtindo huo. Lakini ushauri aliota Mheshimiwa ni kwamba *NACTE* hawa kwa sababu kidato cha nne wamekuwa ni wengi na wengi kama anavyosema wanakosa nafasi, tutakachojaribu sisi ni kuangalia uwezekano wa *NACTE* wapeleke orodha ya vyuo hivi vyote vilivyosajiliwa na *NACTE* kwenye shule za sekondari pale wanafunzi wanapokuwa wanajaza *SEL form* ili vilevile waweze kuona na vyuo vya *NACTE* ambavyo baada ya kumaliza *form four* wanafunzi wanaweza wakajunga pale. Ushauri wake ni mzuri na sisi tunauchukua.

SPIKA: Kutokana na muda tunaendelea swali linalofuata Mheshimiwa Susan Jerome Lyimo.

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibisha swali langu ningependa kufanya masahihisho kidogo, badala ya neno mchepuo lisomeke tahasusi ambalo ni *subject combination*. Baada ya marekebisho hayo, naomba sasa swali langu namba 36 lipitiwe majibu.

SPIKA: Tunasahihisha wapi mchepuo?

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Kwenye kipengele (a) popote pale linapoonekana.

Na. 36

**Michepuo Inayoendana na Kilimo
Kwanza TEHAMA**

MHE. SUSAN A.J. LYIMO aliuliza:-

Mapendekezo ya wadau mbalimbali kuhusu michepuo inayoendana na Sera ya Kilimo Kwanza na TEHAMA yalikubaliwa na Wizara na michepuo hiyo kuingizwa katika fomu za uchaguzi wa masomo ya kidato cha tano mwaka 2013. Utungaji na usahihishaji wa mitihani ya Taifa huzingatia zaidi masomo badala ya michepuo.

(a) Je, ni kitu gani kilisukuma Serikali kufuta michepuo hiyo?

(b) Je, ni sababu gani zilizosababisha Serikali izuie shule kujitengenezea michepuo yao ya masomo iliyoidhinishwa?

(c) Je, Serikali haioni kwamba kufuta michepuo hiyo ni kuwafanya wasomi wetu washindwe kwenda sambamba na sera ya kilimo kwanza na ushindani na utandawazi inayoendana na TEHAMA?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Jerome Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sababu naye amerekebisha hapo, lakini tuliliona hilo, lakini kiswahili cha neno hilo alilokuwa ametamka la tahasusi, linaendana na suala tu la michepwo na hata sisi tumelijibia kwa kutumia michepwo ili wananchi waweze kuelewa tunaongelea kitu gani.

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ilipokea mapendekeo ya michepwo mipywa inayoendana na TEHAMA yaani hizo tahasusi na sera ya kilimo kwanza. Kabla ya kuanza utekelezaji wa kutumia michepwo ushirikishwaji wa wadau mbalimbali ulianza kufanyika. Lengo lilikuwa ni kuanza kutumia michepwo mipywa mwaka 2013 yaani mwaka huu. Kama mchakato wa kushirikisha wadau kuhusu michepwo hiyo kama ungekamilika.

Mheshimiwa Spika, michepwo mipywa hiyo kabla haijakamilika ilingizwa katika fomu za uchaguzi wa masomo ya kidato yaani *SEL form*, kwa ajili ya wanafunzi kuchagua masomo ya kidato cha tano mwaka huu 2013 kabla ya kufanyika mitihani ya kidato cha nne mwaka 2012 kama zilivyo taratibu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia michepwo hiyo, ilionekana kuwa isianze kutumika mwaka 2013 ili kuruhusu ushirikishwaji wa wadau hao. Lengo hasa ni kuwa na uhakika wa mahitaji ya kozi zitakazosomwa na wanafunzi husika katika Elimu ya Juu na mahitaji ya kozi hizo katika soko la ajira. Wadau watakaoshirikishwa ni pamoja na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, yaani *TCU*, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu, yaani *NACTE* na Waajiri mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, Serikali haijafuta michepwo hiyo iliyopendekezwa. Ushirikishwaji wa wadau unaendelea, ukikamilika michepwo hiyo itanza mara moja.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali isingeweza kuziruhusu shule kujitengenezea michepwo yao kwa sababu shule zote za Serikali na binafsi zinatoa elimu kwa kuzingatia sera moja ya Elimu na Mafunzo na miongozo mbalimbali chini ya Wizara moja, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu. Ushirikishwaji wa wadau kuhusu matumizi ya michepwo mipywa, unazihu shule zote za Serikali na zisizo za Serikali zitakazokuwa tayari kuanzisha michepwo hiyo, kwa kuzingatia upatikanaji wa Walimu, vifaa na miundombinu husika, baada ya zoezi la ushirikishwaji wadau kukamilika.

(c) Mheshimiwa Spika, michepwo mipywa iliyopendekezwa haijafutwa kama nilivyosema, bali haijaanza kutumika, kwa sababu ushirikishwaji zaidi wa wadau unaendelea. Aidha, kuhusu suala la wasomi wetu kupata fursa ya kuendana na Sera ya Kilimo Kwanza na Utandawazi, unaoendana na TEHAMA, fursa hiyo ipo kwa kuendelea na masomo ya Elimu ya Juu katika fani za kilimo na TEHAMA kwa kutumia michepwo iliyopo sasa, ikiwemo *PCM* yaani (*Physics, Chemistry na Mathematics*) *PGM*, yaani (*Physics, Geography na Mathematics*) kwa wanaosoma kozi za TEHAMA na *CBA* yaani (*Chemistry, Biology na Agriculture*), kwa wanaosoma kozi za kilimo ngazi ya Elimu ya Juu.

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, Mheshimiwa Philipo A. Mulugo, ameeleza umuhimu wa michepwo hii na kwa kuwa ucheleweshaji huu umetokana na kutokishirikishwa kwa wadau, kwa hiyo Serikali ina lengo la kuendelea kushirikisha wadau wengi zaidi. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, Mheshimiwa Philipo A. Mulugo, anaweza kulieleza Bunge hili, mpaka sasa hivi,

wameshafanya vikao vingapi na wadau ili kuhakikisha kwamba michepuo hii, inakuwa tayari haraka iwezekanavyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa michepuo hii, ni muhimu sana hasa ikizingatiwa kwamba, sasa hivi tunakwenda kwenye dunia mpya ya Sayansi na Teknolojia na vile vile soko la ajira. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Philipo A. Mulugo, ni lini basi michepuo hii itaanza rasmi?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa ameuliza kwamba ni wadau wangapi wamehusishwa katika taasisi hizi na wanaoendelea kuhusishwa.

Mheshimiwa Spika, wakati ule tulikuwa hatujawashirikisha Wahadhiri wa Vyuo Vikuu, maana yake hawa ndiyo wa kazi kubwa baada ya hizo *combination* kukamilika. Wanafunzi wanapomaliza *form six lazima* wawe tayari kuandaa zile *program* kwa wanafunzi watakaosoma Elimu ya Juu. Vile vile watu wa *TAMOSCO* yaani Mameneja na wale wanaomiliki shule binafsi hapa nchini na wenyewe lazima tuwashirikishe, lakini vile vile *NECTA* na *TCU*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hao wote ni wadau ambao tutawashirikisha pamoja ili tuweze kuwa na *combination* zilizo nzuri. Hata Walimu kwa ajili ya kufundisha masomo hayo mapya kama ya *Computer* na kadhalika, mambo ya TEHAMA. Lazima tuandae Walimu huko kwenye Vyuo vya Walimu, tupate Walimu watakaokwenda kufundisha shule za binafsi na Sekondari za Serikali kwa pamoja, kwa sababu watoto ni wa Watanzania wote kwa pamoja.

Swali la pili la kwamba, michepuo hiyo itaanza lini, kama nilivyosema, tukishakamilisha kukutana na hawa wadau, tutaanza mara moja, lakini sio mwaka 2013.

Na. 37

Ahadi ya Rais Kupeleka Umeme Malangali

MHE. MENDRAD L. KIGOLA aliuliza:-

(a) Je, ahadi ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Kikwete ya kupeleka umeme Malangali itatekelezwa lini?

(b) Je, Serikali haioni kuwa huu ni wakati muafaka wa kupeleka umeme Malangali ili kutimiza ahadi hiyo iliyotolewa na Serikali kuititia Waziri wa Nishati na Madini Bungeni kuwa, ifikapo mwaka 2015 asilimia 75 ya Watanzania watakuwa wamepata umeme?

(c) Je, Waziri wa Nishati na Madini yupo tayari kufika Kata ya Malangali na kuongea na wananchi juu ya mpango wa kupeleka umeme kwenye Kata hiyo yenye ahadi ya Rais na hasa ikizingatiwa nguzo za umeme zinazalishwa Jimbo la Mufindi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibuu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Profesa Sospeter M. Muhongo, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Menrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipengele (a) na (b) vya swali hili, vinauliza kitu kimoja, kwa hiyo naomba kuvitolea majibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kutekeleza mradi wa kupeleka Umeme kwenye Kata ya Malangali, utafadhiliwa na Serikali kuititia Wakala wa Nishati Vijiji na utaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2012/2013 na kukamilika mwaka wa fedha 2013/2014, chini ya mpango kabambe wa kupeleka umeme vijiji. Aidha, napenda kufafanua takwimu za Mheshimiwa Mbunge kuwa lengo la Serikali ni kufikia 30% ya Watanzania wenyе umeme ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, kazi hiyo itajumuisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 yenyе urefu wa kilomita 46.9, njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenyе urefu wa kilomita 16, ufungaji wa transfoma sita, mbili za kilovoti 50 na nne za kilovoti 100, ili kuwaunganisha umeme wateja wapatao 310. Gharama za mradi huu, zinakadiriwa kufikia shilingi bilioni moja milioni mia tisa arobaini (1,940,000,000).

Mheshimiwa Spika, kuhusu kufika Malangali, nakubali kuwa niko tayari wakati wowote nitakapopata nafasi.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, nipende kuishukuru Serikali kwa kutoa majibu mazuri, na wameeleza kabisa kwamba, kwa bajeti inayokuja Kata ya Malangali inaweza kupewa umeme na najua kabisa Vijiji vile vya jirani vya Nyigo, Mbalamaziwa na Vijiji vingine vinaweza kupata umeme. Sasa kwa vile jibu limekuwa zuri. Je, tunaweza tukawaambia wananchi wa Kata ile waanje kuweka *wiring* kwenye nyumba zao?

Mheshimiwa Spika, suala la pili, kuna tatizo limejitokeza pale Muamati, pale umeme upo na sasa hivi ni miezi mitatu imepita ile transfoma imeharibika. Je, Naibu Waziri anaweza kuwaambia ni lini transfoma itapelekwa pale kwenye Kijiji cha Muamati ili wananchi wale waweze kuendelea na kazi za kila siku?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) Mheshimiwa Spika, bahati nzuri nilifika Mufindi na Mheshimiwa Mbunge Mendrad Lutengano Kigola tulionana, lakini tulikosa tu nafasi ya kufika Malangali, nataka niwahakikishie wananchi wa Malangali na Vijiji vyote vya kuelekea ukanda ule, Mbalamaziwa na vingine, kwamba, katika mwaka huu wa fedha, tayari mradi wao huu umeshatangazwa kwenye tenda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati wowote, ukamilishaji wa tenda utakapokuwa umekamilika na Mkandarasi amepatikana, tutaanza kuutekeleza. Kwa hiyo, siyo habari ya kusema haina uhakika, ina uhakika kabisa na wawe tayari kuanza kufanya *wiring* kwenye nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu transfoma ya kwenye Kijiji alichokitaja Mheshimiwa Mbunge, Mendrad Lutengano Kigola, tutajaribu kuwasiliana tuone ni namna gani tutatatua suala hili. Kweli tunayo changamoto kubwa, kwamba baada ya kushusha bei ya gharama za kuingiza umeme, basi wahitaji na watu wanaoomba kuwekewa ni wengi na kwa hivyo tuna changamoto za vifaa. Tutajitahidi tuone ni namna gani tutaweza kutatua tatizo la transfoma kwenye kijiji tulichokitaja.

Na. 38

**Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya
Namtumbo – Tunduru**

MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. VITA R.M. KAWAWA) aliuliza:-

Kumekuwa na uchelewaji wa mradi wa barabara kutoka Namtumbo hadi Tunduru inayojengwa na kampuni ya *Progressive* ambayo ilipewa *lots* tatu zenye urefu wa zaidi ya kilomita 190 na mradi huo unatakiwa kumalizika mwaka 2013 lakini mpaka Desemba, 2012 ni asilimia tano (5%) tu ya kazi iliyofanyika:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za kumsimamisha Mkandarasi huyo aliyeonesha kushindwa?

(b) Je, Serikali ipo tayari kugawa vipande hivyo vya barabara kwa kampuni nyingine zilizoonyesha uwezo wa ujenzi kwenye barabara nyingine chini ili mradi huo ukamilike?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. John P. J. Magufuli, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashidi Vita Mfaume Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa barabara ya Namtumbo hadi Tunduru yenye urefu wa kilomita 187.6 unagharimiwa kwa pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Ushirkiano wa Kimataifa Japan (*JICA*) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ili kuharakisha utekelezaji, mradi uligawanywa katika sehemu tatu ambazo ni *lot A*: Namtumbo – Kilimasera (km 60.70), *Lot B*: Kilimasera – Matemanga (km 68.20) na *Lot C*: Matemanga – Tunduru (km 58.70).

Mheshimiwa Spika, katika zabuni, kampuni ya *Progressive Higleig JV* ya India ilishinda zabuni zote tatu na kusaini mkataba na Mwajiri (*TANROADS*) mnamo tarehe 14/3/2011 kwa ajili ya kutekeleza mradi kwa muda usiozidi miezi 29.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji, Kampuni hii ya *Progressive Higleig JV* ilishindwa kutekeleza mradi kulingana na mkataba. Hatua mbalimbali za kumshauri, kumhimiza na kumkemea ili kurekebisha upungufu aliokuwa nao ukiwa ni pamoja na upungufu wa wataalam na vifaa zilishindwa kubadilisha utendaji kazi wa Mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, baada ya juhudzi zote hizi kushindwa kuzaa matunda na ili kunusuru mradi Wakala wa Barabara (*TANROADS*), Kwa ridhaa ya Serikali na wafadhili wa mradi waliamua kuchukua hatua stahiki ya kumfukuza Mkandarasi kulingana na vifungu vya mkataba kuanzia tarehe 8/1/2013.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya kumfukuza Mkandarasi, taratibu za kupata Wakandarasi wengine wa kumalizia kazi zinaendelea kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Dokta *Engineer Gerson H. Lwenge*, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkandarasi huyu aliyechelewesha ujenzi wa barabara hii, kwa maeneo yote matatu, amefukuzwa na kwa kuwa amechelewesha barabara hii kwa kiwango kikubwa na kuleta hasara, kwa maana ya ongezeko la gharama. Je, Serikali itakuwa

tayari kumshtaki ili aweze kufidia gharama ambayo itakuwa imeongezeka baada ya kufukuzwa?

Mheshimiwa Spika, swal la pili, kwa kuwa Serikali imeshatangaza upya ujenzi wa barabara hizi zote tatu; Je, Serikali, itakuwa tayari kusema, ujenzi wa barabara hii, utatumia muda ule uliokuwa umekadiriwa awamu ya kwanza au muda utakuwa umeongezeka? Kama utakuwa umeongezeka, je, itamalizika lini?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kulingana na Sheria na Mkataba, tunapomfukuza Mkandarasi, kitu cha kwanza tunamnyang'anya vifaa vyote, magari, mitambo na kila kitu ambacho kiko kwene *site*, hiyo ndiyo hatua ya kwanza Serikali inachukua.

Pili, tunachukua ile dhamana kuna kitu kinaitwa Benki *guarantee* ya *performance* ya Mkandarasi, ambayo benki huwa inamdhamin na hiyo fedha tunaichukua. Hivyo, tutakapovichukua vitu vyote hivi, kama kutaonekana bado kuna kitu cha kumdai Mkandarasi, basi hatua nyingine inafuata.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumtoa huyu Mkandarasi, hatua ambazo zinaendelea sasa, tunatangaza tenda. Hatujatangaza tenda bado, inabidi tuainishe kazi ambazo zimebakia, tuweke vizuri tenda *documents*, tutangaze Kandarasi kwa yule atakayepatikana.

Mheshimiwa Spika, hayo yanakuwa ni masharti mengine, huwezi ukasema amalize kwa muda uliobaki, kwa sababu muda uliobaki ni mdogo kulingana na kazi yenewe ambayo ni kilomita 187.6. Kwa hiyo, kama muda uliobaki ni miezi mitatu, huwezi kusema Mkandarasi anayepata ajenge kwa miezi mitatu kilomita 187.9. Hivyo vingine vitafuata vigezo na stahiki ambazo unaweza ukamaliza kilomita 187.

Na. 39

Pori la Hifadhi ya Burigi

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA aliuliza:-

Jimbo la Biharamulo Magharibi lipo katika Wilaya zinazozunguka Pori la Hifadhi ya Burigi:-

- (a) Je, ni huduma zipi za kijamii zimechangiwa na hifadhi hiyo?
- (b) Je, ni wananchi wangapi wamewahi kulipwa fidia ya uharibifu wa mashamba yao utokanao na wanyama kama tembo katika pori hili?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Balozi Khamis J. Kagasheki, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Dkt. Antony Gervase Mbassa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Wizara hutoa fedha kiasi cha 25% zinazotokana na mapato ya uwindaji wa kitalii katika Mapori yote ya Akiba nchini, yakiwemo Mapori ya Akiba ya Burigi, Biharamulo na Kimisi kila mwaka. Fedha hizo hupelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya husika kwa ajili ya maendeleo ya jamii. Kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2001 hadi 2012, jumla ya Sh. 24,985,527/= zilipelekwa kwenye Wilaya zinazozunguka mapori hayo kwa ajili ya maendeleo ya jamii.

Aidha, kila mwaka Kampuni za Uwindaji wa Kitalii huchangia dola za Kimarekani elfu tano, yaani (\$5,000) kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya jamii. Pia Wizara imejenga Kituo cha Askari wa kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu katika Kata ya Nyakakita, Wilayani Karagwe ili kuwapunguzia wananchi athari wanazopata kutoka na wanyamapori waharibifu.

(b) Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2005/2012, Wizara iliwalipa jumla ya Sh. 1,250,000/= wananchi nane (8) fedha za kifuta machozi kutokana na madhara waliyopata kutokana na wanyamapori wakali katika Wilaya za Ngara na Karagwe. Fedha hizi zililipwa kwa familia za marehemu watano (5) waliouawa na tembo na wananchi watatu (3) waliojeruhiwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mwaka 2011/2012 Wizara imelipa jumla ya Sh. 26,000,000/= kwa wananchi 277 walioharibiwa mazao yao na wanyamapori katika Wilaya ya Karagwe kwa ajili ya kifuta jasho kwa mashamba yenye jumla ya hekari 605.5.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa muda ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa masikitiko kwani ni mara ya pili naleta humu Bungeni, lakini halijapata majibu mazuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Nane niliuliza suala hili na halikuwa na *element* ya jibu hata moja linalohusisha Wilaya ya Biharamulo. Hali kadhalika majibu haya yako vilevile, sasa naomba nimuulize Naibu Waziri, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, katika hili na juzi alikuwa Jimboni kwangu nashukuru tuliwasiliana. Je, anaweza akanitaja angalau hata kijiji kimoja tu ambacho kimenufaika na hizi fedha ambazo zimetolewa zinazosemekana hapa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili la kusikitisha, baada ya kupata majibu haya nimeongea na Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, naye anashangaa kule Karagwe fedha hii haijui, bahati mbaya Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina sijamwona hapa na ye ye nilitaka nimwulize; sasa taarifa hizi zinatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba nipate majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Antony Gervase Mbassa, nilizungumza naye wakati nafanya ziara yangu katika haya maeneo ya Pirigi, Biharamulo na Ngara na ilikuwa ni katika kujionea tu changamoto ambazo tunazo.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo muhimu sana ambayo ningependa kuyaweka wazi mbele ya Bunge lako Tukufu:-

(a) Kwa malipo ambayo fedha zimetolewa na Wizara, tangu mwaka 2011/2012, kwamba ni Sh. 24,000,000/= ambazo ni sawa na asilimia 25 ya pato ambalo linatokana na Kampuni za Uwindaji. Ukweli ni kwamba, hakuna kabisa biashara ya uwindaji katika haya mapori ambayo ni mazuri sana. Kwa sababu, fedha hizo ni kidogo sana kwa miaka hiyo niliyoitaja. Karibu miaka kumi, Sh. 24,000,000/= kwa vijiji vyote vinavyozunguka, hakuna fedha kabisa.

(b) Suala la pili, uwindaji umeathiriwa sana na tatizo kubwa sana la ujangili katika haya mapori, vitalu vyote ambavyo vimegawiwa, vingi ya hivyo vitalu, wawindaji hawajaweza kwenda kwa sababu tatizo la ujangili ni janga la Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, katika yale mapori ambayo niliyatemelea juzi, ndani ya hiyo Misitu, wamehamia majangili wakubwa wanaotumia silaha za kivita, wanatumia hata *greenhead loncha* na wengine wana mabomu. Pia taarifa tunazozipata hapa, baadhi ya mapori yale, kuna baadhi ya waasi wanaofanya biashara haramu ya nyama za mwitu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema kwamba, tatizo hili ni kubwa, Serikali inaliangalia kwa ujumla wake ili kuona ni jinsi gani tutapambana na ujangili.

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme kwamba, mara tutakapokamilisha mchakato mpya tunaofanya wa kupambana upya na ujangili, na hasa ujangili unaotokana na kuingiliana na mipaka ya nchi jirani, tutaweza kuongeza kipato na 25% ya fedha tutakazozipata yatakuwa ni mamilioni ya fedha ili wananchi wa maeneo haya waweze kufaidika.

SPIKA: Kwa hiyo, hizo Sh. 24,000,000/= unaweza kusema zilikwenda wapi kwa wakati ule na wakati muafaka?

NAIBU WAZIRI WA MALI ASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, labda nimhakikishie tu kwamba, kwa sababu ni miaka kama 10, Serikali iko tayari kukutafutia mchanganuo unaoonesha kwamba hizi shilingi milioni 26 zilikwenda kwenye Kijiji gani kwa Mradi gani na kwa wakati gani.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge muda umekwisha, umekwisha sana. Kwanza naomba niwatambue wageni tulionao:-

Kwanza kabisa wageni walioko kwenye jukwaa la Spika, ni wageni kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*), amba ni: Ndugu Habbi Gunze, Mkurugenzi wa Utangazaji *TCRA*, naomba usimame, ahsante. Mwingine ni Ndugu Innocent Mungy, Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma *TCRA*, na hawa wageni wetu wamekuja kwa ajili ya zoezi la kuzima Mitambo ya Analojia hapa Dodoma na kuwashaa Dijitali kuanzia leo usiku, saa sita kamilii. Kwa hiyo, Dodoma usiku wa leo utaingia katika mfumo wa utangazaji wa Dijitali, kwa hiyo, jamaa wa Dodoma naamini mmeshajiandaa vizuri kupokea huyo mgeni Dijitali na kuagana na Analojia.

Wageni wengine waliokuja hapa kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 86 kutoka Chuo cha Biashara Dodoma (*CBE*), naomba wasimame hapo walipo wote, *okay*, ahsante, nyinyi ni majirani zetu wa karibu sana, karibuni sana. Tunaomba mtumie nafasi hii kusoma kwa bidii kweli kwa sababu dunia ni ya ushindani.

Tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kuna Bi. Zaituni Abubakary, mwanafunzi kutoka *UDOM*, yuko wapi yeye, yuko hapo, huyu amekuja kuwatemelea akina Mheshimiwa Moses J. Machali.

Kuna mwingine anamgeni wake nafikiri amemkuta hapo kwenye *corridor* tu, kama angekuwa amefika angekuwa ameandika rasmi, mgeni wa Mheshimiwa David E. Silinde, wamekutana hapo *corridor*, basi ameleta kwa maandishi ya mkono, huyu ni Mwenyekiti wa Vijana wa CHADEMA Jimbo la Mbozi Magharibi, Immanuel Mkwamu, hebu naomba usimame, karibu sana na ahsante sana.

Matangazo ya kazi, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Edward. N. Lowassa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati yao leo saa saba mchana, katika ukumbi

wa Msekwa B, tulitangaza jana lakini ukumbi huo jana ukatumika kwa kikao kingine, kwa hiyo, leo mnatangaziwa kwamba mtakutana ukumbi wa Msekwa B.

Halafu, Katibu wa Wabunge wa *CUF*, anaitwa Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wa *CUF* kwamba, kutakuwa na kikao cha pamoja saa kumi kamili katika ukumbi wa Msekwa C.

Ofisi ya Spika wanatangaza kwamba, wanaomba niwatangazie Wabunge kwamba, Maafisa wa *NMB*, wako kwenye uwanja wa maonyesho ya Bunge kwa ajili ya kuwapa maelezo Wabunge juu ya *Mortgage Financing*, kwa ajili ya mikopo ya nyumba.

Wakati huo huo kuna Maafisa wa *Star Times* na *Agape Television Network*, wanaonesha na kutoa elimu juu ya matumizi ya ving'amuvi na wote mnakaribishwa kupata maelezo hayo, ili mnufaika na huduma hizo, kwa hiyo, kuna mafunzo ya ving'amuvi hapo chini, lakini pia kuna *Mortgage Financing* pale, *NMB* ndiyo wanaonesha mambo ya *Mortgage Financing*. Nafikiri hii ya *Mortgage Financing* ni vizuri Waheshimiwa Wabunge mkasikiliza, kwa sababu ni muhimu sana kuwaelimisha wananchi huko mnakotoka.

Waheshimiwa Wabunge pia ningeomba kusema ifuatavyo:-

Tarehe 29 tulipoanza Bunge hili, kutokana na wasiwasi ambao ulikuwepo kati ya Wabunge wengi kutaka kuleta hoja ya kuzungumza jambo la dharura linalotokana na yaliyokuwa yanatokea Mtwara, nilikuwa nimeeleza kwamba pengine tutakuwa na Tume ndogo kwenda kuwasikiliza wananchi, lakini napenda nichukue nafasi hii kusema kwamba, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa safari aliokwenda. (*Makof*)

Pia napenda kuwashukuru wananchi wa Mtwara kwa kuwa wawazi kwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, sisi wenyewe tumepata faida ya kujua tatizo lilikuwa nini kule. Kupitia Waziri Mkuu na sisi tunaomba kabisa kabisa, Tanzania tujifunze, kama kuna matatizo mazito namna hii, ujumbe ukaenda wakajadiliana hata vipi, tutapata majibu jamani! Kwa hiyo, tunaomba sana tuwashukuru wananchi wa Mtwara kwa kuwakilishwa na makundi yao, kwa kuweza kujitekeza Waziri Mkuu alipofika na kueleza kilichokuwa kinajiri kule na pengine kufikia maelewano.

Sasa ukisikiliza hayo maelewano, kuna ahadi ambazo zimefanywa na Serikali katika maeneo yale, kwa hiyo, sisi Wabunge kazi yetu ni kuona kwamba zile ahadi zilizoleezwa zinatekelezwa na bahati nzuri, tutakapokutana mara nyingine tutakuwa tumeunda Kamati zinazohusika na pengine kazi ya Kamati hiyo itafanya kazi hiyo. Tunafahamu Sera ya Gesi pia haijakuja, kwa hiyo, tutakuwa na nafasi nzuri sana ya kuichambua Sera na kuchukua mafunzo haya tuliyoyapata kutokana na tatizo la Mtwara.

Kwa hiyo, nawashukuru wananchi wa Mtwara kwa kuja kumsikiliza Waziri Mkuu, tunaomba amani hii iendelee, kusudi maendeleo yapatikane Mtwara na ahadi zile ilizofanya Serikali kupitia kwa Waziri Mkuu, sisi Wabunge wenu tufanye kazi ya kuzisimamia na kuona kweli zinatekelezwa kama ambavyo imepangwa. Kwa hiyo, uundaji wa ile Kamati hatutafanya, kwa sababu itakuwa kama tunafanya *dublication* ya mambo, kwa hiyo, nawashukuru sana, kwa hiyo, tutaunda Kamati zenyewe. Katibu!

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), nikitaka kufahamu, kwa sababu wakati Waziri Mkuu anajibu swali la kiongozi wa Upinzani Bungeni leo, amesema hii Mikataba ya Madini, Gesi na kadhalika inaweza kupatikana,

Iakini Kanuni zetu za Bunge, henzielezi ni utaratibu gani Mbunge anaweza kuutumia kuiptata Mikataba hii. Sasa kama haya aliyojasema ni kweli, mimi nataka kupata Mwongozo wako kama tunaweza Wabunge kuanza kuiona Mikataba hii ya Gesi, ili tujue haya aliyojasema ni kweli na utupatie utaratibu ili siku Mbunge yejote atakapohitaji Mkataba, afuate utaratibu gani kama Waziri Mkuu alivyokiri leo.

SPIKA: Mheshimiwa Felix F. Mkosamali, tunao utaratibu toka muda mrefu kwa sababu hatuwaambii kwamba italetwa Bungeni, iakini utaratibu upo na Ofisi ya Katibu wa Bunge ipo, kama wewe unahitaji kitu cha namna hiyo, unaandika kwa Katibu wa Bunge kwamba naomba Mkataba wa aina fulani, watakupa, hiyo inafanyika wakati wowote, labda kama hamkutumia ninyi, iakini ukiuhitaji watakupa Mkataba ule, halafu utausoma kwa matumizi yatakayohusika. Mpaka sasa ndiyo utaratibu tulionao.

Tunaendelea Katibu! Jamani tusiendelee kubishana Mwongozo ni mmoja halafu tunakaa, haya tunaendelea, Katibu!

HOJA BINAFSI ZA WABUNGE

Udhaifu Ulioko Katika Sekta ya Elimu Nchini

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii niweze kuwasilisha hoja binafsi kuhusu udhaifu uliopo katika Sector ya elimu hapa Tanzania, kabla sijatoa hoja hiyo niwatakie Walimu wote heri ya sikukuu yao, siku ya leo, ni sikukuu ya Walimu duniani ya Mlezi wao *Saint Don Bosco, Salesians of Don Bosco*, alifanya kazi nzuri na kubwa katika kuboresha elimu katika bara la Ulaya, ambayo tunaona leo hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo na hoja binafsi katika Bunge lako Tukufu kuhusu udhaifu ulioko katika Sekta ya Elimu hapa nchini, naitoa chini ya Kanuni ya 54, fasili ya kwanza na 56 fasili ya pili ya Kanuni za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa upendo mkubwa alionao kwetu sisi, tulioweza kufika siku ya leo tukiwa na siha njema. Aidha, kwa moyo mkunjufu na unyenyekevu nikushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote, Katibu wa Bunge, uongozi wote wa Bunge letu Tukufu na wadau wote katika Sekta ya Elimu hapa Tanzania, kwa ushirikiano mkubwa walionipatia katika mchakato mzima wa kuandaa hoja hii ninayoiwasilisha sasa katika Bunge lako Tukufu, kwa maslahi ya pamoja ya Taifa letu, nasema ahsanteni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nianze na muktadha wa hoja yenye:-

KWA KUWA tangu Taifa letu lipate uhuru mwaka 1961 kwa upande wa Tanganyika na mwaka 1964 kwa upande wa Mapinduzi ya Zanzibar, tulitambua umuhimu wa kufuta ujinga kwa kuelimisha wananchi ili tujiletee maendeleo na hadi sasa kazi kubwa imefanyika katika kukuza elimu hapa nchini Tanzania;

KWA KUWA katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 tunataja pamoja mambo mengine makubwa, ifikapo mwaka 2025 tuwe tumejenga Taifa la watu walioelimika kwa upeo wa juu katika nyanja mbalimbali;

KWA KUWA Tanzania ni mionganini mwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa, ambao una malengo nane ya Millenia, lengo la nne likiwa ni upatikanaji wa elimu bora kwa wote;

KWA KUWA ifikapo mwaka 2015, takribani miaka miwili kutoka sasa, tutalazimika kama Taifa, kupima utekelezaji wa malengo hayo ya Millenia ili kuendana na viwango vya Kimataifa na kwa kuwa kwa muda mrefu kumekuwa na viashiria vingi vinavyoonesha kwamba, ubora wa elimu itolewayo hapa nchini Tanzania, katika ngazi zote hauidhishi;

HIVYO BASI ipo haja ya kutathmini kwa undani hali ya elimu nchini Tanzania na kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ombi na uhalali wa kutoa hii, kwa mujibu wa Kanuni ya 56(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kutoa hoja binafsi kuhusu udhaifu uliopo katika Sekta ya Elimu hapa nchini Tanzania na namna ya kuondoa udhaifu huo. Pamoja na kutambua kazi kubwa ambayo Serikali kuititia Wizara ya Elimu imefanikiwa kuifanya kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hivi sasa, elimu itolewayo katika Taifa letu, ina udhaifu mkubwa sana, udhaifu huo unajidhihirisha katika sura mbalimbali, ambazo mionganini mwake ni zifuatazo:-

- (i) Tabia ya Watanzania walio wengi kutothamini muda;
- (ii) Kupotoka kwa Mila, Desturi na Utamaduni wa jamii ya Watanzania;
- (iii) Kumomonyoka kwa Maadili mionganini mwa Watumishi wa Umma na Kada nyiningeizo;
- (iv) Kuporomoka kwa uwajibikaji;
- (v) Kuporomoka kwa kiwango cha utii wa Sheria na Kanuni mbalimbali;
- (vi) Kutokuthamini Rasilimali za Taifa;
- (vii) Kukithiri kwa ukiukwaji wa haki za binadamu;
- (viii) Kukua kwa utamaduni wa ukupe;
- (ix) Kupungua kwa uzalendo kwa baadhi ya wananchi;
- (x) Kutojiamini kwa Watanzania wanaohitimu elimu katika ngazi mbali mbali; na
- (xi) Kukua na kukomaa kwa migogoro ya mara kwa mara katika Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, sura tajwa hapo juu, ndicho chanzo kikuu cha matatizo tuliyonayo katika utoaji wa huduma na shughuli za uzalishaji. Matatizo hayo ni kama yafuatayo:-

- (i) Uduni wa elimu itolewayo katika ngazi mbalimbali za elimu nchini unaojidhihirisha katika viwango vya chini vya ufaulu wa wanafunzi katika mitihani pamoja na uelewa mdogo wa wahitimu;
- (ii) Huduma mbovu zitolewazo katika Sekta mbalimbali;

- (iii) Viwango duni vya ubora na bidhaa za Viwandani, majengo na Miundombinu;
- (iv) Uzalishaji usiotosheleza tena usioridhisha wa bidhaa za mashambani;
- (v) Uharibifu na uchafuzi wa mazingira;
- (vi) Udhafi katika kukabiliana na majanga mbalimbali kama vile mafuriko na temeko la ardhi;
- (vii) Udhafi katika kuzuia na kudhibiti ajali zinazoweza kuzulika kama vile ajali za vyombo vya usafiri, moto na milipuko ya silaha;
- (viii) Udhafi katika kukabiliana na athari za kiafya kwa binadamu na wanyama vitokanavyo na uchimbaji migodini na usafirishaji au uhifadhi wa kemikali;
- (ix) Migomo ya Walimu, Wanafunzi, Wanataluma pamoja na makundi ya kijamii inayojitokeza katika ngazi mbalimbali;
- (x) Ukosefu wa nidhamu ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), mfano matumizi ya simu za mkononi (*Mobile phones*) na mitandao ya kijamii katika kazi bila kuzingatia umakini wa kazi anayoifanya mtu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhaifu katika mfumo rasmi wa elimu. Udhafi ulioko katika Sekta ya Elimu hususan mfumo wa utoaji elimu ndicho kirusi kilichoambukiza udhaifu kwenye Sekta nyingine zote katika Taifa letu. Sababu za msingi za kusema hayo ni kama zifuatazo:-

- (a) Maendeleo ya Taifa lolote kijamii, kiteknolojia, kiuchumi na kisiasa ni tunda la mfumo wake wa elimu; na
- (b) Uhai wa Taifa lolote hutegemea wingi wa matumizi ya wananchi wake walioelimika vyema.

Kwa lugha nyingine, upo uhusiano sababishi kati ya elimu duni na ukengeufu katika jamii na hatimaye utendaji dhaifu katika uchumi na siasa za nchi, uhusiano huu umethibitika kitaalam.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya kuokoa muda nitazungumuzia sehemu ndogo tu ya udhaifu ulioko katika mfumo wetu rasmi wa elimu.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utafiti nilioufanya kwa takriban miaka 18 sasa, yanaonesha ya kwamba udhaifu wa mfumo wetu rasmi wa elimu unatokana na mambo makuu matatu, ambayo hapa nchini imekuwa ni nadra kuyaangalia kwa undani tunapoendelea kutafuta ni kwa nini tumekwama katika masuala mbalimbali ya kimaendeleo, mambo hayo ni kama yafuatayo:-

- (i) Sera ya Elimu ya mwaka 1995 na Sera nyinginezo;
- (ii) Mitaala ya Elimu ya Shule za Msingi na Sekondari; na
- (iii) Mihtasari ya masomo na vitabu vya kiada na ziada vitumikavyo katika shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Sera ya Elimu ya Tanzania inayotumika kwa sasa imekuweko kwa muda mrefu, ukweli huo watosha kuwa na haja ya kuifanyia utafiti mkubwa Sera hiyo ili licha ya kuangalia nini tumetekeleza na nini hatujatekeleza, tuifanye iendane na mahitaji yetu ya sasa, natambua hatua ambazo zimeshachukuliwa na Wizara husika, lakini kusudio la kusema kuwa na Sera mpya ambayo inajenga kizazi cha Watanzania katika misingi ya ubora halijafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, mionganoni mwa mambo yaliyo bayana kwa sasa ni kwamba, masuala mengi ya kisera katika elimu tunayofuata hapa nchini yametokana na masharti na au maelekezo tuliyopewa na vyombo vya Kimataifa kama vile Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Dunia (*IMF*).

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, maelezo ya vyombo hivi badala ya kutusaidia kuinua ubora wa elimu hapa Tanzania yametuletea matukio yasiyokuwa mazuri na yanayotuyumbisha. Mathalani miaka ya 1980, vyombo hivi vilitutaka tupunguze matumizi ya rasilimali za umma katika kugharamia huduma za kijamii ikiwemo elimu. Jambo ambalo limechangia kwa kiasi kikubwa uduni wa shule za umma hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kana kwamba haitoshi, vyombo hivi viliwahi kutufanya tuelekeze zaidi rasilimali zetu katika elimu ya msingi tu, kutambua kwamba elimu ya juu ni anasa, lakini miaka ya hivi karibuni vimebadili ushauri huo na kudai rasilimali zaidi zielekezwe katika elimu ya juu. Ni kana kwamba tumegeuzwa kuwa sampuli ya kufanya majoribio katika maabara za sera ya elimu, bila kujali athari ambazo zinatokana na majoribio haya.

Mheshimiwa Spika, kama taifa tunapaswa kutumia sera ambazo zimethibitika kitaalam, kwamba zinaleta matunda yanayotakiwa. Tusiendelee kuyumbishwa na vyombo ambavyo Sera zinazosimamia siyo za maslahi kwetu, kwa sababu tu sisi ni wahitaji wa misaada yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la Mitaala; sanjari na matatizo haya ya Sera ya Elimu nchini, ni jambo la kusikitisha sana kwamba, hadi mwaka 2011 nchi yetu haikuwahi kuwa na Mitaala rasmi. Nasisitiza kuwepo na Mitaala rasmi ya Kitaifa kwa ajili ya elimu ya shule za msingi na sekondari. Ijapokuwa, wanasiasa, wanaharakati na wanataaluma mbalimbali wamekuwa wakiilalamikia Wizara ya Elimu kuwa na Mitaala mibovu na Mitaala inayobadilishwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 ya mwezi wa 11 mwaka jana, niliuliza swali Bungeni na nikaomba Serikali ilete Mitaala ya elimu hapa Bungeni, kwenye Bunge hili na mpaka leo hii hawajaleta. Niko tayari kwa *challenge* hiyo, nasema Serikali yetu haina Mitaala.

Mheshimiwa Spika, nitoe angalizo pia kwamba nyaraka za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji, zina ainisho la dhana ya Mitaala, ambalo kwa kiasi fulani ainisho hilo nalo linatoa mtazamo usioelezeka kutambua mitaala tunayotakiwa kuwa nayo na kwa mapana yake.

Mheshimiwa Spika, aidha, ainisho hili na maudhui yake (*purpose*) ya utoaji wa elimu halifafanui mchakato wa utoaji wa elimu, hivyo unatufanya na tusielewe vigezo na namna ya kupima na ufikiriaji wa malengo hayo ya elimu hapa nchini kwetu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika nchi nyingi duniani wazazi au walezi wa kila mtoto aendaye shule wana haki ya kujua mitaala ya masomo husika ya shule hizo. Kwa kuzingatia haki hiyo, vyombo vya elimu huwajibika kumpatia kila mzazi au mlezi nakala ya mitaala inayoonesha wazi

sababu za mwanaye kupatiwa elimu na kiwango husika, elimu hiyo inapatikana katika mchakato gani na nini kinachotarajiwa kwa badiliko la mtoto baada ya kupatiwa elimu hiyo na badiliko hilo litapimwa kwa namna gani.

Mheshimiwa Spika, tazito katika mihtasari. Kwa kuwa, mitaala ndiyo inayotaja malengo ya elimu yanayoongoza uandaaji wa miongozo ya mihtasari ya masomo licha ya kwamba mitaala hatuna, mihtasari iliyopo hivi sasa haina malengo yanayoeleweka vema na imekosa viwango yya kitaalum vinavyokubalika kitaalam. Mihtasari yote iliyopo inaonesha kwamba kama Taifa tumeshindwa kutofautisha madhumuni na malengo ya Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, mihtasari hiyo inaonesha kwamba tumeshindwa kutumia vema lugha rasmi za Taifa yaani Kiswahili na Kiingereza katika kubainisha malengo hayo. Kwa mfano, katika nyaraka za Wizara ya Elimu na Mafunzo yaani mihutasari ilioandikwa kwa lugha ya Kiswahili malengo ya elimu hapa nchini Tanzania yapo 10 wakati ilioandikwa kwa lugha ya Kiingereza yapo tisa tu.

Mheshimiwa Spika, katika malengo hayo kuna sentensi za Kiingereza ya kiunganisha *and* yaani *and, and* mara sita na sentensi hizi zimekuwa zikitumika hivyo tangu mwaka 1995 zilipoandikwa katika Sera ya Elimu ya Taifa. Malengo ya elimu ya msingi kwa lugha ya Kiswahili yapo 18 wakati kwa lugha ya Kiingereza yapo 10 tu. Ni aina gani basi ya elimu tuliyonayo kama malengo yake yanatofautiana kwa kiasi hicho na ubabaishaji wa hali ya juu kwa kiasi hicho?

Mheshimiwa Spika, udhaifu katika vitabu yya Kiada na Ziada. Licha ya matatizo ya kimkakati tuliyonayo katika nyaraka zinazoongoza elimu, kuna udhaifu mkubwa katika utendaji wake kiuwezo na kimaadili. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kitengo kilichopo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii kinachotoa ithibati kwa vitabu yya Kiada na Ziada yaani *Educational Material Approval Committee* kimeshindwa kutekeleza wajibu wake kama ipasavyo, kitengo hiki kimesababisha mafuriko ya vitabu vinavyopotosha dhana nzima ya elimu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, si tu kwamba vitabu vingi yya Kiada vimepewa ithibati na *EMAC* vina makosa mengi ya kitaaluma, bali hata mfumo wa uandaaji na usambazaji wa vitabu hivyo una harufu ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mfano kuhusu hayo ninayoeleza hapa. Mnamo mwaka 2009 kuititia mpango uitwao *The Teaching and Learning Material Program*, Taifa letu lilipata msaada wa dola za Kimarekani milioni 13 ambazo ni takribani shilingi bilioni 20.4 za Kitanzania kutoka *USAID* kwa ajili ya kuandika na kuchapisha vitabu na kugharamia vifaa yya kufundishia masomo ya Hisabati, Fizikia, Kemia na Baiolojia kwa idadi ya vitabu visivyopungua 2,250,000.

Mheshimiwa Spika, makosa lukuki yaliyopo katika vitabu vilivyochapishwa kutokana na mradi huo yanatisha na kusikitisha hasa ikizingatiwa kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii ilipata uvezeshwaji wa jopo la Wataalamu kutoka *South Carolina State University* mathalan katika vitabu yya *Mathematics for Secondary Schools Volume I, II, III and IV* vilivyoratibiwa na *EMAC* kama inavyoonekana kwenye utangulizi wake.

Mheshimiwa Spika, Mwandishi Mkuu ndiye huyo huyo Mhariri Mkuu na ndiye huyohuyo Mhakiki Mkuu, wakati taaluma na maadili ya uandishi wa vitabu inazuia mtu kuandaa, kuhariri na kuhakiki andiko lake mwenyewe. Wataalam walioshiriki kuandaa vitabu hivyo walikuwa na majukumu mengi ikiwamo kuandika, kuhariri na kuhakiki vitabu walivyoviandaa wao wenyewe chini ya uratibu wa *EMAC*.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu kengeufu ultumika pia na Wataalam wa masomo mengine yote yaliyoandaliwa wakati huo chini ya uratibu wa *EMAC*. Dosari hii haikubaliki duniani kote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, harufu ya rushwa ninayoitaja inatokana na mgongano wa kimaslahi na mgongano huu unajitokeza moja kwa moja kwa watendaji wa *EMAC* kushiriki kuratibu na kuandika vitabu ambavyo baadaye wao wenyewe wanavipatia ithibati. Utayarishaji wa andiko yaani *typesetting* ulifanyika Malaysia na kuchapisha au *printing* kufanyikia nchini Kenya. Hakuna uwiano mzuri wa Waandishi wa vitabu hivyo baina ya Watanzania na wageni kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, machapisho ya vitabu hivyo yanayodhihirisha upungufu mkubwa wa kitaaluma, lugha na muktadha wa elimu inayotakiwa kwa Mtanzania kwa sasa. Hili ni jambo ambalo linapotosha wanafunzi na kuwafanya wasielewe mada au maudhui yaliyokusudiwa ikiwa ni pamoja na matumizi ya lugha isiyo rasmi ya Kiingereza katika vitabu hivyo.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni mifano michache tu niliyoitoa, lakini kabla sijatoa hoja wenyewe, naomba nitoe mifano michache:-

Mheshimiwa Spika, ninavyo vitabu vingi hapa lakini labda ningepewa zaidi ya saa 12 ndiyo naweza nikawasilisha vizuri, lakini nitatoa mifano michache. Hiki ni kitabu cha Hisabati kinachotumika kwenye shule zetu, nitatoa mfano mmoja tu katika kitabu hiki. Swali la 15, kwenye ukurasa wa tatu maelezo yanasema hivi;

"Dada aliuza mboga kwa mwenye hoteli kama ifuatavyo: Jumatatu kilogram 114, Jumanne kilogram 125, Jumatano kilogram 213 na Jumamosi kilogram 818. Kaka aliuza jumla ya kilogram ngapi katika mboga?". Maelezo ni Dada, lakini swali ni Kaka! Kitabu hiki hapa!

Sasa kaka aliuza jumla ya kilogram ngapi za mboga katika siku hizo nne? Kitabu cha hisabati, Taasisi ya Elimu Tanzania. Kitabu hiki cha darasa la saba; hao hao ndiyo Waandishi na hao hao ndiyo Wahariri na majina yao yapo hapa na kimepewa ithibati.

Mheshimiwa Spika, kitabu kingine tuangalie muhtasari, hii ni silabasi iliyotoka Wizara ya Elimu wenyewe, lakini Serikali yetu hata jina la Wizara ya Elimu hawalijui. Hapa juu imeandikwa *Ministry of Education and Vocational Training*, lakini ukiingia ndani kimeandikwa *Ministry of Education and Culture*. Silabasi hiyo! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, unakuka kwenye vitabu hivi ambavyo Wamarekani wametoa dola milioni 13 wanasema *This book is written using curriculum developed and approved for the United Republic of Tanzania* ya mwaka 2005. Naomba wanipe hiyo mitaala ya mwaka 2005 waliyoisema kwenye Bunge lako Tukufu iko wapi? Na wakiweza kuionesha hapa nitajiuzulu Ubunge wangu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ipo haja kwani ukiangalia vitabu vyote ninavyovieleza hapa, kwa mfano, cha Hisabati ambapo ninavyo na vya Jiografia, Kiswahili na Historia. Unaweza kuona kitabu hiki ni cha *form three*, ni Toleo la mwaka 2008, lakini kitabu cha *form one* ni toleo la mwaka 2010, yaani inaanza *form three* ndiyo inakuja *form one*. Sasa ukiangalia yote haya kwa nia njema kabisa yapo mambo mengi ambayo yanositisha.

Mheshimiwa Spika, twende kwenye *Education and Training Policy* ya mwaka 1995 ambayo mpaka leo hii ndiyo inayotumika na wameinakili, kwa hiyo, mihtasari yote wanakokotoa huko. Lakini lengo la Elimu hapa linasema; "*To develop and promote self*

confidence and an enquiring mind and understanding and respect for human dignity and human right and a readiness to work hard for professional self advancement and National improvement". And, and, and, and!

Mheshimiwa Spika, hapa ukiangalia vitabu vyote vilivyopo mbele ya Bunge lako Tukufu hata mihtasari yenewe inatia wasiwaso mkubwa na ninachoomba hapa ni kwamba, hata Bunge lako Tukufu mwezi wa 11 mwaka jana Serikali ilitoa kauli ambazo siyo za ukweli kwamba wataleta mitaala kwenye Bunge hili na hawakuweza kufanya hivyo na hiyo mitaala haipo na wakuza mitaala wapo kabla ya mwaka 2005 mpaka leo hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, naomba kwa moyo mkunjufu niwasilishe hoja yenewe kwa mujibu wa kanuni ya 54 na 56 (1) ya Kanuni za Bunge lako Tukufu kama ifuatavyo na naomba nitoe hoja hii tukiwa juu ya itikadi za Vyama vya Siasa kwa kuwa nchi hii ni yetu sote.

KWA KUWA kuzorota kwa elimu ya Tanzania kumesababishwa na mambo yafuatayo:-

- (i) Udhifu wa mifumo ya elimu inayotokana na sera na mitaala ni mihtasari;
 - (ii) Kupitwa kwa wakati kwa sera ya Elimu ya Taifa;
 - (iii) Kukosekana kwa mitaala rasmi ya Kitaifa ya elimu.
- (iv) Mihtasari iliyopo ni ya mazoea tu ya uwepo wa mifumo ya elimu na haina malengo yanayoleweka vema na hivyo kukosa viwango vya kitaaluma visivyokubalika kitaalam na kupelekeea Taifa kushindwa kutumia lugha rasmi za Kitaifa katika kubainisha malengo hayo; na

(v) Udhifu katika vitabu vya Kiada na Ziada ambao unatokana na udhaifu mkubwa katika utendaji kiuwezo wa ukiukwaji wa maadili wa kuidhinisha vitabu vyenewe vyenye makosa kutumika mashule na hivyo kuleta hisia kuwa udhaifu huu una harufu ya ufisadi.

NA KWA KUWA matokeo ya udhaifu huu na matatizo ya kisera ya elimu, mitaala, mihtasari na vitabu vya Kiada na Ziada imeleta matatizo mengi ambayo nimeyataja kwenye maelezo yangu ya msingi. Maelezo hayo ni kwamba:-

- (i) Tabia ya Watanzania wengi kutothamini rasilimali muda;
- (ii) Kuporomoka kwa mila, desturi na tamaduni ndani ya jamii ya Kitanzania;
- (iii) Kumomonyoka kwa uadilifu mionganini mwa watumishi wa umma na kada nyiningezo;
- (iv) Kuporomoka kwa uwajibikaji;
- (v) Kuporomoka kwa kiwango cha utii wa sheria na kanuni mbalimbali;
- (vi) Kutokuthamini rasilimali za Taifa;
- (vii) Kukithiri kwa ukiukwaji wa haki za binadamu;

- (viii) Kukua kwa utamaduni wa ukupe;
- (ix) Kupungua kwa uzalendo kwa baadhi ya wananchi;
- (x) Kutokujiamini kwa Watanzania wanaohitimu elimu katika ngazi mbalimbali;
- (xi) Kukua na kukomaa kwa migogoro ya mara kwa mara katika Sekta ya Elimu;

NA KWA KUWA kuporomoka kwa kiwango cha elimu kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na kitengo kilicho chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis kinachotoa ithibati kwa vitabu vya Kiada na Ziada kimeshindwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo kwa kusababisha mafuriko ya vitabu vinavyopotosha elimu kwa Taifa letu, kwa mfano, vitabu vingi vya Kiada vilivypewa ithibati na *EMAC* vina makosa mengi ya kitaaluma na mfumo wa uandaaji na usambazaji wa vitabu hivyo.

NA KWA KUWA mnamo mwaka 2009 kuititia mpango uitwao *Teaching and Learning Material* Taifa letu lilipata fedha kutoka Marekani zaidi ya shilingi bilioni 20.4 kutoka Shirika la *United States Agents for International Development* yaani *USAID* kwa ajili ya kuandika na kuchapisha vitabu na kugharamia vifaa vya kufundishia masomo ya Hisabati, Fizikia, Kemia na Bailojia kwa idadi isiyopungua 2,250,000 pamoja na Wizara kupata uwezeshwaji wa jopo la Wataalam kutoka *South Carolina State University*. Mathalan, katika vitabu vya Hisabati, Fizikia, Kemia na Baiolojia, vitabu hivyo vina upungufu mwangi.

NA KWA KUWA utungaji wa vitabu haukuftutana na kanuni za kiuandishi kwani Mwandishi Mkuu ndiye huyohuyo Mhariri Mkuu na Mhakiki Mkuu.

NA KWA KUWA kitaaluma na kimaadili mtu haruhusiwi kuandaa, kuhariri na kuhakiki andiko lake Mwenyewe. Utaratibu huu kengeufu ultumika pia kwa wataalam wa masomo mengine yote yanayoandalialiwa chini ya utaratibu wa *EMAC*. Dosari hii haikubaliki duniani kote.

NA KWA KUWA udhaifu huu umesababishwa na matatizo mengi kama mgongano wa kimaslahi, utayarishaji wa jopo la wataalam usiowiana, kukosekana kwa uwiano wa waandishi kwa waandishi wa vitabu hivyo.

NA KWA KUWA elimu inayopangwa na sera bora na mitaala bora pekee yenye mihtasari na vitabu vilivytayarishwa kwa umakini mkubwa na uadilifu ndiyo vyenye uwezo wa kujenga Taifa la watu waadilifu, Wazalendo, wachapakazi, watambuzi wa haki na wajibu wao katika jamii.

NA KWA KUWA, elimu ni mapigo ya moyo ya Taifa lolote lile, narudia, kwa kuwa elimu ni mapigo ya moyo ya Taifa lolote lile, mapigo ya moyo yakienda kinyume na asili yake uhai huweza kupotea. Tuna wajibu wa kuokoa uhai huu.

Mheshimiwa Spika, kwa uchungu mkubwa kabisa na kwa kusononeka, vitabu hivi ukivisoma ukurasa wa pili, inaanandikwa ni *Ministry of Education and Vocational Training Zanzibar*, 2010 lakini ukisoma kule mwisho ni *Ministry of Education and Vocational Training of United Republic of Tanzania*. Vitabu vyote vilivypewa msaada na *State University* vikiwemo vya Fizikia, Baiolojia na hiki ninachokisoma ni cha Hisabati. Yaani hata kubadilisha jina tu, vitabu ni vya Wizara lakini kubadilisha tu, kwenye ujisadi huu imeshindikana? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana na jambo hili tuliweke juu ya itikadi zetu na tuhakikishe kwamba Bunge lako Tukufu kwa mujibu wa Ibara ya 163 tunachukua wajibu wetu kwa kuisimamia na kuishauri Serikali.

HIVYO BASI kwa mujibu wa kanuni ya 117 fasili ya (1) na ya (3) ya Kanuni za Kudumu ya Bunge lako Tukufu, naliomba Bunge lako Tukufu kuunda Kamati Teule ya Bunge ya kuchunguza kina cha udhaifu huo wa kimfumo katika sekta ya elimu hapa nchini na kupendekeza hatua za kuchukua ili Taifa letu liondokane na aibu ya udhaifu huo hatarishi katika mfumo wetu wa elimu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa unyenyekevu naomba kutoa hoja. (*Makof*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, naafiki!

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Ahsante, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kabla ya ya kutoa ufanuzi wa hoja binafsi ya Mheshimiwa James Francis Mbatia, Mbunge wa Kuteuliwa kuhusu udhaifu katika sekta ya elimu nchini, naomba nieleze kwa ufupi kuhusu uendeshaji wa elimu hapa nchini kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo na mitaala iliyopo sasa.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa elimu na mafunzo nchini Tanzania umekuwa ukiongozwa na sera kubwa tatu ambazo ni Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Sera ya Elimu ya Ufundii na Mafunzo ya Mwaka 1996 na Sera ya Taifa ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo, Serikali ilianzisha *program* ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu ama *Education Sector Development Program* ya mwaka 1997. Madhumuni ya *Program* ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu yalikuwa ni kutekeleza malengo ya sera ambayo ni kama ifuatavyo:-

Moja, kuongeza fursa za utoaji wa elimu. Pili, kuinua ubora wa elimu itolewayo. Tatu, kuhakikisha usawa katika utoaji wa elimu na nne kuimarisha mbinu bora za uongozi, utawala, ugharamiaji wa elimu na mafunzo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na programu hiyo, mipango mbalimbali iliandaliwa na kuanza kutekelezwa. Mipango hiyo ni pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MEM), Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES) na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Juu (MMEJU).

Mheshimiwa Spika, kutokana na utekelezaji wa Sera hizi kumekuwa na mafanikio mbalimbali, moja ni ongezeko la Shule za Msingi kutoka shule 10,927 mwaka ...

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Naomba asome kwanza mpaka amalize...

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Mheshimiwa Spika, nataka kujua anachosoma kinaruhusiwa na Kanuni?

SPIKA: Amesambaza!

MHE. TUNDU A.M. LISSU: *No!* Anaruhusiwa kutoa maelezo kubadilisha...

SPIKA: Ndiyo maelezo ya upande wa pili, ukitoa hoja ya Serikali Kamati inajibu...

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Ndicho ninachotaka kujua, kanuni zinasema hivyo?

SPIKA: Zinaruhusu!

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Kanuni zinasema hivyo?

SPIKA: Tunafanya! Endelea Mheshimiwa Waziri! Ninyi wote mbona mnaendesha kikao kwa niaba yangu? Hapana, naendesha mimi peke yangu.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kutokana na utekelezaji wa Sera hizi, kumekuwa na mafanikio mbalimbali:-

Kwanza, ongezeko la shule za msingi kutoka 10,927 mwaka 1995 hadi shule 16,331 mwaka 2012, za Serikali zikiwa 15, 525 na ongezeko la shule za sekondari kutoka 595 mwaka 1995 hadi shule 4,528 za Serikali zikiwa 3,508 mwaka 2012. Aidha, uandikishaji wa wanafunzi wa Shule za Msingi umeongezeka kutoka wanafunzi 3,877,643 mwaka 1995 hadi wanafunzi 8,247,172 mwaka 2012. Idadi ya uandikishaji katika Shule za Sekondari Kidato cha I – VI pia imeongezeka kutoka wanafunzi 196,375 mwaka 1995 hadi kufikia wanafunzi 1,884,272 mwaka 2012.

Pili, Vyuo vya Elimu ya Ufundu vimeongezeka kutoka 16 mwaka 1995 hadi Vyuo 248 mwaka 2012, vya Serikali vikiwa 139 vikiwezesha ongezeko la Wanachuo kutoka 4,820 mwaka 1995 hadi Wanachuo 112,447 mwaka 2012. Aidha, Vyuo vya Elimu ya Ufundu Stadi vimeongezeka kutoka Vyuo 343 mwaka 1995 hadi kufikia Vyuo 750 mwaka 2012, vya Serikali vikiwa 164 na kuongeza udahili wa Wanachuo kutoka 28,560 mwaka 1995 hadi Wanachuo 121,348 mwaka 2012.

Tatu, Vyuo vya Ualimu hali kadhalika vimeongezeka kutoka 31 mwaka 1995 hadi Vyuo 105 mwaka 2012, vya Serikali vikiwa 34 na kuwezesha ongezeko la Wanachuo kutoka 13,381 mwaka 1995 hadi Wanachuo 43,258 mwaka 2012.

Nne, ongezeko la Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki kutoka Vyuo 12 mwaka 1995 hadi 49 mwaka 2012, vya Serikali vikiwa 11 na ongezeko la udahili wa wanachuo kutoka 9,042, mwaka 1995 hadi wanachuo 166,488 mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, changamoto zifuatazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sera:-

Moja, upatikanaji wa Walimu na Wahadhiri wa kutosha;

Mbili, kukidhi mahitaji makubwa ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu;

Tatu, ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika Shule, Vyuo na Taasisi za Elimu; na

Nne, uwezo wa kugharamia elimu hususan Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hizi, Serikali inaendelea kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Elimu ambapo mkazo uko katika kuinua ubora wa elimu itolewayo hususan kuongeza idadi ya vyuo na udahili katika vyuo vya mafunzo ya ualimu. Kuendelea kutoa kipauumbele cha mikopo kwa wanaosoma shahada ya ualimu wa sayansi na hisabati. Kuimarisha ufuatiliaji na ufundishaji shulenii, kuendelea kutoa mafunzo ya walimu na wahadhiri kazini ili kuimarisha ufundishaji, kuongeza kasi ya ujenzi wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kupata nguvukazi yenye ujuzi na maarifa, ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu, ununuzi wa vitabu vya kiada na ziada na kuimarisha Mabaraza ya Udhhibit wa Ubora wa Elimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba kujibu Hoja Binafsi ya Mheshimiwa James Mbatia kuhusu vipengele mbalimbali vilivyoainishwa katika hoja hiyo kama ifuatavyo:-

Kwanza, hoja kuhusu Sera ya Elimu iliyopo kuwa ya muda mrefu. Kwa kuwa kumekuwepo na matukio mbalimbali ndani na nje ya nchi yakiwemo Tanzania kuridhia Maazimio, Itifaki na Mikataba mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa ambayo inahitaji kuzingatiwa, Wizara yangu ilianzisha mchakato wa kuhuisha Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995 na nyinginezo ili ziendane na mabadiliko haya.

Hadi sasa wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Walimu na Wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari, Wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu, Wahadhiri wa Vyuo Vikuu, Watendaji mbalimbali wa Mikoa na Halmashauri, Taasisi mbalimbali na Asasi za Kiraia, wamepitishwa katika Rasimu ya Awali na kutoa maoni yao kati ya mwezi Juni mwaka 2009 na Septemba mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu walipitia Rasimu ya Sera tarehe 24 mpaka 25 Aprili, mwaka 2010 na tarehe 13 Novemba, mwaka 2011.

Maoni ya Waheshimiwa Wabunge na Wadau wengine yamejumuishwa katika Rasimu ya Mwisho ya Sera na maandalizi ya mkakati wa utekelezaji wa Sera hiyo yapo katika hatua za mwisho ambavyo vitawasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri mwishoni mwa mwezi Machi, mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili kuhusu kutokuwepo kwa mitaala rasmi ya kitaifa kwa ajili ya elimu ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ufanuzi kuhusu maana ya mtaala na jinsi unavyotofautiana na muhtasari kwa sababu hivi ni vitu viwili tofauti, ambavyo mara kwa mara hutumika kama vina maana moja wakati vina maana tofauti. Mtaala ni utaratibu mzima wa elimu pamoja na vitendo vyote katika shule au chuo vyenye malengo maalum. Aidha, mtaala ni mwongozo mpana unaoweka viwango vya utoaji elimu kwa kuzingatia maeneo yafuatayo:-

Moja, mambo watakayojifunza wanafunzi, yaani maarifa, stadi na mwelekeo wa kila rika;

Mbili, ni njia za kufundishia na kujifunzia zitakazotumika katika utekelezaji wa mtaala;

Tatu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinavyohitajika;

Nne, upimaji, ufuatiliaji na tathmini ya mtaala vinavyoendana na rika husika;

Tano, sifa za mwalimu atakayeweza mtaala husika;

Sita, miundombinu muhimu itakayeweza utekelezaji fanisi wa mitaala; na

Saba, muda utakaotumika katika ufundishaji au utekelezaji wa mitaala. Kwa mfano, miaka saba kwa elimu ya msingi.

Muhtasari wa somo ni orodha ya mada zinazokusudiwa kufundishwa ili kukamilisha kiwango fulani cha elimu.

Mheshimiwa Spika, ufanuzi zaidi wa mitaala na muhtasari uko katika ukurasa wa sita wa taarifa ambayo imesambazwa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa na mitaala rasmi tangu Uhuru. Hata hivyo, mitaala hiyo imekuwa ikitumiwa na wataalam kama mwongozo wa kuandaa mihtasari ya masomo husika. Kwa kawaida mitaala haitumiki moja kwa moja darasani kwa ajili kufundishia. Kwa sababu hiyo, mitaala imekuwa haisambazi shulenii. Mihtasari ya masomo mbalimbali ndio huwa inasambazwa shulenii na kwa wadau mbalimbali wa elimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mabadiliko ya mitaala, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, mabadiliko yamefanyika mara nne tangu tupate Uhuru. Mabadiliko hayo yalifanyika kwa mara ya kwanza mwaka 1967 baada ya kuzaliwa kwa Azimio la Arusha na falsafa ya elimu ya kujitegemea. Mihtasari mipy ya shule iliandaliwa na kuingizwa mada zinazojenga uzalendo, kupenda kazi na kuoanisha elimu iliyotolewa na kazi za mikono hususan uzalishaji mali.

Mabadiliko ya pili yalifanyika mwaka 1979 na yalihusisha uanzishwaji wa shule za michepuo ili kutekeleza kwa vitendo Elimu ya Kujitegemea na Siasa ni Kilimo.

Mabadiliko ya tatu ya mitaala yalifanyika mwaka 1997 na yalifanyika kwa kupunguza wingi wa masomo ya elimu ya msingi kutoka 13 hadi masomo saba. Baadhi ya masomo yaliunganishwa na kuandaa mihtasari mipy. Kwa mfano; masomo ya Uraia, Jiografia na Historia yaliunganishwa na kuwa somo moja la Maarifa ya Jamii.

Mabadiliko ya nne ya mitaala yalifanyika mwaka 2004 – 2009 na yalihusu ufundishaji wa kuzingatia ujenzi wa maarifa na ujuzi ama *competency based training*.

Mheshimiwa Spika, ingawa mitaala imebadilika mara nne tu, wadau wengi wamejenga hisia kuwa mitaala imebadilika mara kwa mara, sababu ya kuchanganya mitaala na muhtasari. Kwa mfano, kabla ya mwaka 1995 masomo ya Fizikia na Kemia yalikuwa na mihtasari tofauti inayojitegemea na kufundishwa kama masomo tofauti, lakini mwaka 1995 masomo hayo yaliunganishwa na kuandaliwa muhtasari mmoja wa somo la Fizikia pamoja na Kemia (*Physics and Chemistry*). Kilichobadii hapa ni kuunganishwa kwa mihtasari ya masomo haya mawili na siyo kubadilisha mitaala.

Mwaka 2006 masomo ya Fizikia na Kemia yalitenganishwa katika masomo mawili tofauti na kuwa na mihtasari yake inayojitegemea kama ilivyokuwa awali. Aidha, mabadiliko mengine yalihusu somo la Maarifa ya Jamii ambalo lilivunjwa na kuwa masomo matatu; somo la Uraia, Jiografia na Historia ambapo ilibidi kuandaa mihtasari mitatu tofauti.

Mheshimiwa Spika, ingawa kila badiliko lilioainishwa hapo juu lilihusisha mihtasari, bado kulikuwa na hisia vilevile kwamba mabadiliko haya ni ya mara kwa mara na ni mabadiliko ya mitaala ambavyo sivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, nchi yetu ina mitaala rasmi. Mheshimiwa mtoha hoja akasema hatuna mtaala wa Sekondari.

(*Hapa Mheshimiwa Waziri alionesha Vitabu husika*)

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, Kitabu hiki kinasomeka *Curriculum for Ordinary Level Secondary Education, 2005*. Kitabu hiki ni *Curriculum for Advanced Level Secondary Education, 2009*. Kitabu hiki ni *Curriculum for Diploma in Teacher Education Programs, 2007*. Kitabu hiki ni *Curriculum for Certificate in Teacher Education Programs, 2007*. Hivi ni katika vitabu vichache ambavyo nimemudu kuvikusanya na kuja navyo hapa.

Vitabu vile vilivyoandikwa kwa msaada wa *USAID* na vikitaja *Curriculum* ya Sekondari ya mwaka 2005, maana yake ni *Curriculum* ya Sekondari ya Mwaka 2005, ni hii hapa nimjulisho Mheshimiwa mtoha hoja.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu kuhusu udhaifu katika vitabu vyatia kiada na ziada. Vitabu vyote vyatia kiada na ziada vinavyotumika katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vyatia Ualimu, hupitishwa na Kamati ya Machapisho na Vifaa vyatia Kielimu (*Educational Materials Approval Committee - EMAC*). *EMAC* ilianzishwa kwa Waraka wa Elimu, Na. 2 wa Mwaka 1998 na Waraka huo ulirekebishwa kwa Waraka Na. 7 wa Mwaka 2005. Malengo ya kuanzisha Kamati hii ni kupitia na kuidhinisha matumizi ya machapisho na vifaa mbalimbali vyatia Kielimu katika Shule na Vyuo vyatia Ualimu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utaratibu uliopo, ni jukumu la Sekretarieti ya *EMAC* kupokea machapisho yote yanayotoka kwa wachapishaji na kuhakikisha kuwa hayana alama yoyote ya utambulisho wa mchapishaji, mwandishi au mtu ye yeyote aliyechangia kwenye chapisho hilo. Kabla ya machapisho kupitiwa na kuidhinishwa na *EMAC*, hupewa namba za siri ambazo ndizo hutumika katika mchakato wa utathmini badala ya jina la mchapishaji. Kwa kawaida chapisho moja hupewa watathmini watatu na kila mmoja hupewa nakala yake na kuifanya kazi kwa muda wa siku 14. Aidha, watathmini huandika taarifa ambayo huiwasilisha kwenye Kikao cha Kamati ya *EMAC* kwa maamuzi. Maamuzi ya kuidhinisha machapisho hufanywa na Wajumbe wote na si jukumu la Mjumbe mmoja.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wanaounda Kamati ya Machapisho ama *EMAC*, hutoka ndani na nje ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Wajumbe kutoka nje ya Wizara ni Chama cha Wauza Vitabu, Katibu Mtendaji wa Chama cha Wachapishaji wa Vitabu, Mtendaji Mkuu wa Chama cha Hakimiliki Tanzania, Mwakilishi wa Shule zisizo za Serikali na Mwakilishi kutoka Vyuo Vikuu vyenye Shule au Kitivo cha Elimu. Kwa sasa kuna Mwakilishi kutoka Shule ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nne ni kuhusu vitabu vilivyotolewa na *USAID*. Mnamo mwaka 2009, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliomba msaada wa Vitabu vyatia Sayansi na Hisabati kutoka Serikali ya Marekani. Serikali ya Marekani kupitia *USAID*, ilitoa msaada huo chini ya usimamizi wa Chuo Kikuu cha Jimbo la South Carolina, ambacho kilisimamia na kuratibu msaada huo. Wakati huo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilikuwa imeshapata msaada huo kwa masomo ya Sayansi. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ilikubaliana na Chuo Kikuu cha Jimbo la South Carolina na *USAID* kutumia vitabu vilivyoandikwa Tanzania Zanzibar.

Kwa kuwa Wizara yangu ina utaratibu wa kutathmini vitabu kabla ya kuanza kutumika shulenii, vitabu hivyo vilifanyiwa tathmini na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia uliokuwa unafadhiliwa na USAID ulitekelezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, ambapo jukumu kubwa la Wizara lilikuwa ni kuhakikisha kuwa Wachapishaji wamechapa vitabu, kuvipokea na kuvipeleka shulenii. Malipo kwa wachapishaji yalifanywa na Chuo Kikuu cha Jimbo la South Carolina na USAID moja kwa moja kwa wachapishaji. Hakuna fedha yoyote kwenye Mradi huo iliyopokelewa na Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, Wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Jimbo la South Carolina waligawanyika katika makundi mbalimbali ya kitaalam; walikuwepo Wahariri, Wataalam wa Masomo, Wataalam wa Lughu, Vielelezo na Michoro. Wataalam na Walimu wetu ndio waliokuwa na jukumu la kuhakiki maudhui ya somo walilokuwa wanatathmini. Kila somo lilikuwa na Wataalam wasiopungua wane; Walimu watatu kutoka Shule za Sekondari na Mkuza Mitaala mmoja kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania. Aidha, kila somo lilikuwa na Mtaalam mmoja wa Maudhui kutoka Chuo Kikuu cha Jimbo la South Carolina na alikuwa ni mshauri tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la utayarishaji wa andiko na uchapishaji kufanya nje ya nchi; napenda kueleza kuwa Serikali ilikwishajitoa kwenye masuala ya uchapishaji vitabu na kwa sasa suala hilo limebaki kwa wachapishaji binafsi. Kutokana na uwepo wa soko huria, mchapishaji anayo haki ya kuchagua kiwanda, nchi ama sehemu anayotaka kazi zake za uchapishaji zifanyike.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tayari Serikali imeanza kufanya mapitio na marekebisho makubwa ya Sera ya Elimu kama nilivyoyaeleza hapo awali na kwa kuwa Sera ya Elimu ndio mhimili mkuu wa mfumo wa elimu na kwa mujibu wa Kanuni ya 57(1)(a) ya Kanuni za Bunge, Toleo ya Mwaka 2007, naomba kutoa hoja ya mabadiliko ya Hoja Binafsi kuhusu udhaifu ulioko katika Sekta ya Elimu, aya ya 5, kwa kuondoa maneno: "Ninaomba Bunge lako Tukufu kuunda Kamati Teule ya Bunge ya kuchunguza kina cha udhaifu huu wa kimfumo katika Sekta ya Elimu hapa nchini. Aidha, ikiwezekana Kamati hiyo ipendekeze hatua za kuchukuliwa ili Taifa liondokane na udhaifu huo hatari" na kuingiza maneno mapya yafuatayo: "Naomba Bunge lako Tukufu liitake Serikali kuzingatia hoja zilizotolewa kwenye hoja hii na kuzifanyia kazi kwa kina wakati ikikamilisha mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo."

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja ya awali lilikuwa inasema hivi: Kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) na (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ninaomba kutoa hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge ya kuchunguza kina cha udhaifu huu wa kimfumo katika Sekta ya Elimu hapa nchini. Aidha, ikiwezekana Kamati hiyo ipendekeze hatua za kuchukuliwa ili Taifa liondokane na udhaifu huo hatari.

Hii ndio hoja ya msingi ya Mheshimiwa Mbatia. Huyo anayeleta hoja nyingine ya kufanya mabadiliko inaruhusiwa Kikanuni, yeche anatumia kifungu hicho lakini amenakiri kama nilivyosema halafu anasema tuondoe maneno hayo na kuingiza maneno mapya yafuatayo: "Naomba Bunge lako Tukufu liitake Serikali kuzingatia hoja zilizotolewa kwenye hoja hii na kuzifanyia kazi kwa kina wakati ikikamilisha mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo."

Hizi ndizo hoja mbili; kwa sababu kama nilivyosema jana, unapokuwa na hoja binafsi unakuwa na jambo ambalo unataka tulifanyie kazi. Una jambo ambalo unatushawishi sisi wote tuamue kwamba tujadili hilo halafu tufikie uamuzi wake. Sasa jambo hilo ndilo hili ambalo limefanyiwa mabadiliko sasa ili tuwe pamoja maana tukiacha bila kuamua sasa hatutakuwa tunajadili, tunajadili nini.

Kwa hiyo, ndiyo maana inabidi kabla hatujafanya hivyo tufanye hayo mabadiliko kuona ni hoja gani sasa tunayo, pia tunataka kusema nini na tunapotaka kuamua tujue tunasema nini. Kwa hiyo, kwa sababu Kanuni hiyo ya 57 inaruhusu kufanya mabadiliko kwenye hoja, sasa nitawahoji wanaofikiria mabadiliko yaliyoletwa hapa yakubalike watasema ndiyo na ambao wanafikiria kwamba mabadiliko yaliyoletwa na Serikali yasikubaliwe basi watasema siyo.

TAARIFA

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa, ngoja mimi niseme kwanza, halafu utaseme taarifa. Utani-*interrupt* wakati ninaelekeza. Sasa tukishafika kama hoja iliyotolewa na Serikali itakataliwa tunaendelea na hoja ya msingi. Kama hoja iliyotolewa na Serikali itakubalika basi ile hoja ya Mheshimiwa James Mbatia itabadiishwa kwa lugha iliyopo hapa. Kwa hiyo, ningependa Mheshimiwa James Mbatia azungumze kwanza.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 57(3) inasema; kila badiliko linalopendekezwa sharti liwiane na hoja inayokusudiwa kufanyiwa mabadiliko na pia iungwe mkono na lisilingizwe jambo lolote ambalo kwa maoni ya Spika linaweza kuwasilisha kwa hoja maalum. Fasili ya nne inasema, badiliko lolote halitarhusiwa kama kwa maoni ya Spika linapingana moja kwa moja na hoja ya msingi iliyotolewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, badiliko linalotolewa na Serikali linapingana moja kwa moja na hoja ya msingi, kwa maoni yangu na nasema hivyo nikizingatia kwamba, Serikali hii hii tarehe 30 Oktoba, 2012, hii ni *Hansard* ya Bunge lako Tukufu, tukiwa tunazungumzia mitaala hapa hapa Waziri akasema naomba kunukuu: "Mheshimiwa James Mbatia aliuliza maswali ya nyongeza mawili, nitasema lile la kwanza tu. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameliambia Bunge lako Tukufu kwamba, mtaala unaotumika sasa ni ule wa mwaka 2005; na kwa kuwa kuna hisia kwenye jamii kwamba mitaala hii imekuwa ni jambo la siri wakati elimu siyo jambo la siri wala siyo jambo la kuficha; je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuleta mitaala ili kila Mbunge apate kopi yake katika Mkutano huu wa Bunge ili Waheshimiwa Wabunge waweze kufuatilia mitaala hii kwa urahisi katika Shule hasa za Sekondari na za Msingi."

Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu alijibu hivi; Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa James Mbatia, Mbunge wa Kuteuliwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, labda nieleze dhana halisi ya neno *curriculum* na *syllabus*, yaani mtaala na muhtasari. Mtaala ni neno pana, ni dhana kubwa, lakini *syllabus* ndiyo hizo ambazo zinatumika kwa walimu kwa ajili ya kutengeneza miongozo ya kufundishia madarasani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anapenda kuliomba Bunge lako Tukufu liridhie Wizara ya Elimu isambaze mitaala kwa kila Mbunge kwenye Bunge hili, mimi sina matatizo na hilo. Lakini basi ninaahidi kwenye Bunge ijalo, yaani Bunge hili, yaani Mkutano huu, kwamba

tutachapisha mitaala hiyo ya elimu ya mwaka 2005 na tutawagawia Wabunge waweze kuona dhana kamili ya neno mtaala (*curriculum*), kuna nini ndani yake halafu baadaye tuje tuone namna walimu wanavyochukua mtaala kwenda kwenye mihtasari, *curriculum to syllabus* ndipo angalau tuweze kuelewa jambo halisi." Haya ni majibu ya Serikali hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ninaamini nina akili timamu, hoja iliyopo mbele yetu ninaliomba Bunge lako Tukufu liridhie, ni wajibu wetu wa Kikatiba kwa mujibu wa Ibara ya 163.

Mheshimiwa Spika, haya tuliyoyasema hapa ni machache na ndijo tunaomba yafanyiwe maamuzi. Mheshimiwa Waziri amesema, Mheshimiwa Rais aliomba msaada kutoka *South Carolina University*; je, nikimwuliza msaada alioomba mwaka 2006 kutoka UNESCO na zikapatikana dola milioni 4.7 fedha hizo ziko wapi? Je, nikiuliza Wizara fedha za *Radar* dola milioni 55 zipo kwenye utaratibu gani?

Mheshimiwa Spika, yapo mengi na yanasicitisha sana, ndijo maana mimi kwa moyo wangu, historia ituhukumu, nina-quote maneno ya Marehemu Mwalimu Nyerere ya mwaka 1958 alisema, Wakoloni wameshindwa kuondoa ujinga, maradhi na umaskini, tunataka Uhuru ili tupambane na adui maradhi, ujinga na umaskini. Kama Mkoloni akikataa, tutamshtaki kwa Mwenyezi Mungu na kama Mwenyezi Mungu akikataa tutamshtaki kwa shetani, tupo tayari kwa mapigano; maneno ya Mwalimu Nyerere. Naomba tulitendee Taifa letu haki, sikubaliani na hoja ya Serikali kubadilisha hoja yangu. (*Makof*)

SPIKA: Naomba tuweke sawa, tunachojadili hapa tunajadiliana juu ya hoja hizi mbili kusudi tupate uamuzi wa kupata hoja moja. Kwa hiyo, ninaruhusu mjadala kama tunakubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na Serikali au tunakubaliana na mapendekezo yaliyokuwa yametolewa na Mheshimiwa James Mbatia. Hii ndijo hoja ya sasa. Kwa hiyo, msichanganye kuanza kujadili kwamba ilikwishaibiwa, vikaenda wapi, hapana. Tunajadili hii kwanza tufikie maamuzi hapa halafu tuendelee.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, mwongozo.

SPIKA: Si ninafikiri nakuita useme sasa mwongozo tena. Tunajadili hoja, nilikuwa nina-refer tunachojadili sasa. Hatujadili yale maudhui yote, tunajadili haya mawili; kuna hoja ya Mheshimiwa James Mbatia na kuna hoja ya Serikali, ndicho tunachojadili.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, kabla hatujadili kati ya hizo hoja mbili, tunapaswa tupate uamuzi kama hoja ya Serikali ya mabadiliko ni halali.

SPIKA: Ndicho tunachofanya sasa.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kanuni ya 57(1)(a), inaruhusu hoja kufanyiwa marekebisho kwa kuondoa maneno fulani kwa ajili ya kuingiza maneno mengine na alichofanya Mheshimiwa Waziri ni kupendekeza kuondoa maneno na kuingiza maneno mengine.

Mheshimiwa Spika, lakini Fasili ya (3) na ya (4) ya Kanuni hiyo ya 57, inaweka masharti juu ya maneno yanayoweza kuingizwa au kutolewa kwenye hoja ya msingi. Fasili ya (3) inaweka wazi kabisa kila jambo linalopendekezwa la mabadiliko sharti liwiane na hoja inayokusudiwa kufanyiwa marekebisho. Kwenye mjadala huu hoja ni kwamba, Bunge liunde Kamati Teule

kuchunguza hii habari ya mitaala. Hiyo ndiyo hoja ya msingi. Hoja ya Waziri inatakiwa iwiiane na hoja hiyo ya kuunda Kamati Teule ya Bunge. (*Makof*)

Fasili ya (4) inasema badiliko lolote la kuingiza maneno au kuondoa maneno, halitaruhusiwa kama kwa maoni yako Mheshimiwa Spika linapingana moja kwa moja na hoja ya msingi iliyotolewa. Hoja ya msingi ni kuunda Kamati Teule ya Bunge hili, hoja ya mabadiliko ya Mheshimiwa Waziri ni kuondoa Kamati Teule, inapingana moja kwa moja na hoja ya msingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ni vizuri wewe Mheshimiwa Spika, utuambie kama hoja ya Waziri haipingani na hoja ya msingi ya Mheshimiwa James Mbatia.

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo, utakuwa ume-*preside over ukiukwaji* wa Kanuni za Bunge hili Tukufu na hiyo haiko sawasawa.

Pili, hoja ya mwisho, Fasili ya (7) inasema hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja nyingine ya mabadiliko sharti ihusiane na hoja ya kwanza ya mabadiliko na itatolewa, itajadiliwa na kuamuliwa kabla ya ile hoja ya kwanza ya mabadiliko kufanyiwa uamuzi. Kwenye hatua hii, tunatakiwa tujadili hoja ya mabadiliko ya Serikali siyo tuamue ipi ndiyo halali. Tuamue kwanza hii ya Serikali ni halali, inaruhusiwa na Kanuni; kama inaruhusiwa na Kanuni *then* tuiamue halafu ndiyo twende kwenye hoja ya Mheshimiwa James Mbatia. Tufuate Kanuni za Bunge hili Tukufu kama tunataka kutenda haki kwa Watanzania walioleta hapa. Haiwezekani mambo yanaletwa kienyeji kienyeji kinyume cha Kanuni.

SPIKA: Ondoa maneno ya kienyeji kienyeji.

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Ahsante, ninayaondoa maneno ya kienyeji kienyeji, lakini hoja zinaletwa kinyume cha Kanuni.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kwenye kufanya mabadiliko ya hoja hakuna mahali popote ambapo Mheshimiwa Waziri ana ruhusa ya kujibu hoja. Mheshimiwa Waziri ametumia karibu nusu saa hapa anajibu hoja kifungu kwa kifungu badala ya kuleta hoja yake ya mabadiliko, hairuhusiwi na Kanuni.

Mheshimiwa Spika, Kanuni zinavunjwa unaruhusu, hii si sawa sawa; Mawaziri hawako juu ya Kanuni hizi, kila mmoja wetu hapa amefungwa na hizi Kanuni, haiwezekani wakawa wanavunja Kanuni halafu Mheshimiwa Spika unawanyamazia. Nashukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Ezekia Wenje, naomba ukae.

Kwanza, ile ya kusema kwamba hatujadili kwa mujibu wa Sheria si sahihi. Halafu ya pili ya kwamba, Spika anavunja Kanuni si sahihi kwa sababu Kanuni ya pili inamruhusu Spika kuona mwenendo mzuri wa kujadili ndani ya Bunge hili.

Waheshimiwa Wabunge, maswali hata jana tulifanya hivi kwa sababu mambo tunayozungumza siyo ya utani haya na ukiangalia hoja ya Mheshimiwa James Mbatia ni nzito, anazungumzia udhaifu mzima katika Sekta ya Elimu, siyo jambo zuri akawa Mheshimiwa James Mbatia amesema halafu upande wa pili hatujasikia. Sasa tuna *position* nzuri sisi ya kuendelea kujadili kwa sababu tumesikia aliyosema Mheshimiwa James Mbatia, tumesikia pia na wengine wanafanya nini. Sasa katika sisi tunaozungumza tujue hasa hapa katikati ukweli udhaifu uko wapi. Vinginevyo, ukisema useme halafu na mwingine asijibu siyo sahihi. Hoja ikiletwaa na Serikali huwa Kamati inaanza kusema, Kambi ya Upinzani inatoa maoni, hivi hivi hoja ameileta

mwenzetu, upande unaosimamia hiyo hoja ni vizuri nao wakajieleza wanavyofanya na hiyo haiondoi kwamba hoja ya Mheshimiwa Mbunge inafutika kwa sababu Waziri amejibu, ni utaratibu mzuri tu wa kufanya kazi.

Sasa toka mwanzo nilikuwa nina shida kuhusu hoja hii ya kuunda Kamati Teule, maana ni Sekta nzima ya Elimu iliyojaa udhaifu; unaona hapo. Sasa Kamati Teule mara nydingi ina kitu *specific*, ndiyo maana nikaona kwamba hii hoja ya Serikali haivurugani na hoja ya Mheshimiwa James Mbatia, kwa sababu wanachokisema kwamba haya kama ni udhaifu ni lazima waangalie kwenye Sera tu. Huwezi kuangalia udhaifu kwa Kamati Teule. Mimi sijaona kama mabadiliko ya Serikali yanavunja hoja ya msingi. Kwa hiyo, hii kwangu mimi ni halali. Bado tunajadiliana kwamba tunaondoa hoja gani na tunabakia na ipi. (*Makofii*)

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niwe mchangiaji wa kwanza.

SPIKA: Siyo mchangiaji wa kwanza, bado hatujaanza kuchangia. Tunabishana kwamba, tuunde Kamati Teule kufuatana na hoja ya Mheshimiwa James Mbatia au tutafute utaratibu mwagine kufuatana na hoja ya Mheshimiwa Waziri, ndicho tunachoongea sasa, hatujadili bado.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba tukubaliane Waheshimiwa Wabunge kwamba, mabadiliko ya Serikali tuyakubali kwa sababu hii kazi ni kubwa na itachukua muda mrefu wakati Kamati Teule inaweza ikawa ya muda mfupi. Naomba Waheshimiwa Wabunge, tukubaliane kazi ifanywe vizuri na Serikali, kwa sababu tayari ilishaanza. (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, Serikali imeleta mapendekezo haya siyo kwamba inadharau hoja ya Mheshimiwa James Mbatia, hoja ya Mheshimiwa James Mbatia ni ya msingi sana, ni mambo makubwa, yapo mambo ya ukweli na mambo sahihi. Yote anayoyazungumza Mheshimiwa James Mbatia yapo kama kumi na tano hapa, yote ni ya kisera. Sasa ukiunda Kamati Teule, kwa *nature* ya Kamati Teule kwa masuala haya yote ya Kisera ambayo yatahusisha Wizara zaidi ya nne, kwa *terms* za Kamati Teule tunaweza tukalionea Bunge lako Tukufu, haitakamilisha kazi hiyo.

Kwa hiyo, ndiyo maana tukasema kwa kuwa Bunge hili limekuwa na tabia ya ushirikiano, maelekezo na hoja za Mheshimiwa James Mbatia, zichukuliwe na zitiliwe manani katika kazi ambayo Serikali imekwishaanza ya marekebisho ya sera ya msingi, lakini hoja za Mheshimiwa James Mbatia zichukuliwe maanani.

Mheshimiwa Spika, lakini hivi sasa umeunda Kamati na kesho kutwa utaunda Kamati nyiningine itashughulikia masuala yote ya elimu, inayoshughulikia elimu ya msingi na nini. Kamati zako kwa kawaida zitashirikiana na Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba, hoja za Mheshimiwa James Mbatia zinatiliwa maanani katika Muundo wa Sera ile, kwa kutumia Muundo wa Kamati za Kudumu za Bunge ambazo ni za miaka mitano. Kamati Teule inaundwa kwa jambo moja mahususi na kufa. Tunazo Kamati za Kudumu za Bunge ambazo zinadumu kwa miaka miwili na nusu, hizi ndizo zingekuwa na jukumu la kuhakikisha kwamba, haya mambo ya Mheshimiwa James Mbatia na mambo ya Serikali yamezingatiwa katika sera hii mpya. Kwa hiyo, ndiyo maana tulikuwa tunafikiria siyo kwamba tunaondoa hiyo hoja, lakini tunajua ndani yake ingawa hatuku-mention Kamati yako ya Kudumu itahusika moja kwa moja kwa sababu ndiyo inasimamia utendaji na uendeshaji wa Wizara ya Elimu. (*Makofii*)

Kwa hiyo, mimi ninapendekeza, Mheshimiwa James Mbatia, kwa busara alizozileta anatumia muda mrefu sana ku-study na ninampenda sana kwa jinsi alivyoeleza vizuri, lakini akubaliane na yeye atakuwa ni sehemu na Kamati ya Kudumu ya Bunge, itakuwa ni sehemu ingawa haikutajwa lakini ndiyo utendaji wa lazima, Kamati ya Bunge itamwona Waziri na kuhakikisha kwamba zile sera na kama tulivyokaa ndani ya Bunge imeelezwa hapa tulizingatia wote hata rasimu ile ya marekebisho ya sera.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninapendekeza Waheshimiwa Wabunge wakubali Serikali iendelee na kwa sababu Serikali inasimamiwa na Bunge katika hatua zote, itaendelea kusimamiwa na Kamati ya Kudumu utakayoiunda kwa kusimamia masuala ya Elimu. (*Makofii*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

SPIKA: Mwongozo tena, ngoja nisome ile Kanuni ya Kamati Teule. Kanuni ya Kamati Teule ni ya 117(1). Kamati Teule inaweza kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalum, kwa hoja mahususi itakayotolewa na kuafikiwa. Sasa ninachokisema ni kwamba, hoja ya Serikali ni halali kwa sababu ukiangalia hii hoja alioitoa Mheshimiwa James Mbatia, ina vitu vingi ambavyo katika Kamati Teule siyo *precise*, ndiyo maana nasema bado kuna uhalali na nikifika hapo tutapiga kura ipi hoja tuweze kuifanyia kazi. Nilimwona Mheshimiwa Ezekia Wenje kwa muda mrefu.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nilikuwa naomba utaratibu kuhusu Kanuni ya 57, Fasili ya (7).

Mheshimiwa Spika, toka nimekuja kwenye hili Bunge, kwa utaratibu ninaoufahamu mimi na ukiangalia hii iliyotoka Serikalini, walikuwa wanajibu hoja halafu mwisho wakaleta *Schedule of Amendment*. Mimi ninavyoufahamu utaratibu wa Bunge wa majadiliano tunavyofanya hapa, mara nydingi hoja ikiletwa, *Schedule of Amendment* inakuja mwisho pale ambapo tumefanya mjadala, pale tunapomalizia kuelekea kwenye kuamua ile hoja ya mwisho. Ukitosha Kanuni ya 57 inasema kwamba, ni wakati gani mtu anaruhusiwa kuleta *Schedule of Amendment*.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa hatua hii ...

SPIKA: Soma hicho unachokisema kiko wapi?

MHE. EZEKIA D. WENJE: Kanuni ya 57(7), sasa itakuwa ni *subject to interpretation*.

SPIKA: Soma.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Inasema hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja nydingine ya mabadiliko.

TAARIFA

MBUNGE FULANI: Taarifa.

SPIKA: Naomba mwache mmoja amalize, halafu tutaangalia taarifa, maana inakuwa taarifa mnafikiria kichwani. Mheshimiwa Wenje, endelea.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, naomba nisomE. Inasema; hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja nyingine ya mabadiliko sharti ihusiane na hoja ya kwanza ya mabadiliko na itatolewa, itajadiliwa na kuamuliwa kabla ya ile hoja ya kwanza ya mabadiliko kufanyiwa uamuzi.

SPIKA: Ninavyofanya sasa.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, ndio maana nimesema hii ni *subject to interpretation*, kwa hiyo, tafsiri yangu na kuangalia mila na desturi ya Bunge hili jinsi tunavyofanya majadiliano katika *Schedule of Amendment* na hii ya Serikali ni kama *Schedule of Amendment* kwamba, ingeletwa mwisho baada ya sisi Wabunge kufanya majadiliano kuhusu hiyo hoja ya msingi ya Mheshimiwa James Mbatia.

SPIKA: Mheshimiwa Wenje, kama ni suala la mila na desturi, ninazo mila zaidi kuliko hata wewe; hizi ni hoja, kwa hiyo, hoja inaweza kufanyiwa mabadiliko mradi inalingana na hoja ya msingi ya Mheshimiwa Mbatia. Kinachotokea hapa, hatukatai hoja ya Mheshimiwa Mbatia, tunachokisema Kamati Teule tatizo lake liwe na jambo moja *specific*; ukiangalia hapa kuna mitaala, kuna nini, kuna wizi, kuna California, kuna mafisadi na mengine. Sasa haya yote ndio tunajadili nini hapa! Mtabadili sasa tunachokisema sisi badala ya kuwa na Kamati Teule ambayo itakuwa *limited*, hoja ya Serikali inatupa uwanja mkubwa zaidi, ndio hoja. Kwa hiyo, uhalali wa hoja ya Serikali upo. Sasa kwa ajili ya kutoendelea kubishana, nataka tupige kura.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, sitaki kwenda kwenye *technicalities* za Kanuni kwa sababu umeshazitolea uamuzi na Kanuni zetu zinaweka bayana kwamba, uamuzi wa kiti ni wa mwisho na katika hili hatuna haja ya kulumbana juu ya uamuzi ulioutoa, nakwenda kwenye hoja iliyotakiwa hapa kuwekewa utaratibu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya msingi ya Mheshimiwa James Mbatia, hakuna anayekataa kwamba haina msingi, ni hoja ambayo inatakiwa ifanyiwe utafiti wa kina na ni hoja ya kizalendo na yenye manufaa mapana kwa Taifa letu. Ninataka kusema kwa mujibu wa Kanuni zetu ukiunda Kamati Teule kama ulivysoma, inashughulikia jambo maalum na hapa Mheshimiwa Mbatia alivyoainisha na kutoa ushahidi, anaeleza udhaifu kwenye sera, mitaala na katika muhtasari na mengine ambayo yapo kwenye hoja ya Mheshimiwa Mbatia. Hayo ukiyaundia Kamati Teule, ninyi si mabingwa wa mambo ya mitaala wa masuala ya muhtasari, masuala ya elimu. Mimi nataka niseme wazi, kazi ya Bunge kama ingekuwa ni jambo *specific* tungeshughulika nalo kwa mujibu wa Kanuni.

TAARIFA

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nadhani wangeheshimu Kiti wakae.

SPIKA: Napenda kusikiliza anayeongea *so that I can make a proper ...*

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, taarifa kwa mujibu wa Kanuni.

SPIKA: Mwache aseme kwanza halafu nitakupa nafasi ya taarifa. Haya maliza.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, hoja yangu hapa ni kwamba, kwa jinsi hoja ilivyo muhimu, ni jukumu la upande wa Mhimili wa Utendaji kupata Tume

itakayoanza kuangalia masuala haya ya kisera na ya wataalam ambao wanaaminika katika masuala haya ya elimu na si masuala ya wanasiisa kwenda kuandaa mitaala na wala kuandaa mihtasari na wala kuandaa sera inayokuja katika upande ule. Watakuja kutoa maoni kwenye sera kama wadau na hatimaye Baraza la Mawaziri litapitisha sera.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kusema kama tutakubaliana na hoja ya kuunda Kamati Teule, jambo hili la jumla jumla maana yake Bunge linataka kupora mamlaka ya Mhimili mwininge wa Dola na kuingia katika shughuli za utaalam, ambayo si kazi yao. Hata kama tunaamini kwamba, ndani ya Bunge kuna wataalam na wasomi wazuri, lakini jukumu lile liko kwa wataalam, tuiachie Serikali iandae mitaala, sera na mihtasari, wataalam hao waweze kuleta na sisi kama wadau tutatoa maoni yetu. Kwa hiyo, naungana mkono na hoja ya Mheshimiwa Waziri kwamba, hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule katika hoja iliyoko hapa haistahili kwa mujibu wa uendeshaji bora wa Bunge. (*Makofii*)

SPIKA: Hakuna taarifa mnajadili tu hapa. Tunaendelea, Mheshimiwa Dkt. Kigwangala.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Waumini wa Kiislamu huwa wanatumia msahafu kuongoza shughuli zao. Ukitaka kuusoma vizuri na kuuelewa msahafu basi lazima uusome wote ili uelewe kila kitu kwa ukamilifu wake.

Mheshimiwa Spika, tunapozisoma hizi Kanuni na tukisoma nusu nusu tutapata tabu sana kuelewa maudhui yake. Sasa katika Kanuni ya 57 ambayo inaleta huu ugomvi uliopo hapa, sina ubishi na vipengele ambavyo amevigusia Mheshimiwa Tundu Lissu, kile cha kwanza na kile cha tatu na cha nne. Ninachelea kusema kwamba, Mheshimiwa Tundu Lissu, hakusoma kipengele cha tano kwa maana ya Fasili ya (5) ya Kanuni ya 57. Ukiisoma Fasili ya (5) basi huu mjadala wote pengine usingekuwepo hapa Bungeni, kwa sababu yenewe inasema, naomba niinukuu: "Iwapo hoja ya mabadiliko inapendekeza kuondoa maneno fulani na kuingiza maneno mengine, basi mjadala juu ya suala la kufanya mabadiliko unaweza kuangalia kwa pamoja yale maneno yanayopendekezwa yaondolewe na maneno ambayo yanapendekezwa yaingizwe."

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mjadala ambao tunatakiwa tuwe nao hapa sasa hivi ni mjadala juu ya maneno ambayo yanapendekezwa na Mheshimiwa Waziri kama yaingizwe ama yaondolewe. Huo ndiyo mjadala ambao tunapaswa kuwa nao hapa na si mjadala wa muktadha mzima wa hoja kwamba Kamati Teule ama siyo Kamati Teule. Hapo hatujafika bado kwa sababu ni hoja ya kwanza ambayo pengine tunetakiwa tufanyie maamuzi kama kusingekuwa kuna hoja ya pilii.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Kanuni hiyo hiyo ya 57, Fasili ya (7), ambayo Mheshimiwa Ezekia Wenje ameinukuu inasema kwamba; "Hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja nyingine ya mabadiliko, naomba ni *underline* maneno "Kufanya mabadiliko katika hoja nyingine ya mabadiliko. Hapa katika Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Spika, hakuna hoja nyingine ya mabadiliko. Tuna hoja ya kwanza ya Mheshimiwa Mbatia na kuna hoja ya pilii ambayo ni ya mabadiliko iliyoletwa na Mheshimiwa Waziri. Sasa hakuna hoja nyingine ya tatu ambayo inataka kufanya mabadiliko kwenye ile hoja ya pilii iliyoletwa na Mheshimiwa Waziri.

Kwa hiyo, nashindwa kuelewa kwa nini tunaendelea kujadili jambo ambalo halipo hata katika mambo ambayo tunayajadili hapa Bungeni kwa wakati huu. Ninaomba tu-stick katika Kanuni namba tano, turudi kujadili kama yale maneno yaliyoingizwa na Waziri yanafaa yaingizwe ama hayafai kuingizwa na nafikiri hilo ndiyo jambo la mjadala hapa Bungeni.

SPIKA: Na ndiyo hoja tunayojadili.

TAARIFA

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Taarifa.

SPIKA: Bwana taarifa nini, tunajadili wewe taarifa, jadili tu. Haya jadili siyo taarifa. Hapa mnadanganya taarifa halafu mnaongea. (*Kicheko*)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Swali langu kama ulivyosema, hoja aliyoleta Mheshimiwa Mbatia ni hoja ya msingi na ni muhimu sana kwa mustakabali wa Taifa. Ndugu zangu Wabunge, lazima tukumbuke kwamba, sisi hapa ni Wabunge, sisi siyo Serikali na tunatakiwa tufanye kazi za Kibunge.

SPIKA: Jadili hoja hii kama mabadiliko yanayoletwa na Serikali yakubalike au sivyo?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Ndio nakwenda huko Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Maana unatuambia tena sisi Wabunge kwani asijejua sisi ni Wabunge nani. Jadili, jadili.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, hawa unawapa nafasi kubwa. Unawapa nafasi kubwa wanajinafasi kidogo. Naomba nipate nafasi.

SPIKA: Jadili Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Okay. Ninachokata kukisema, kazi ya Bunge ni kuisimamia Serikali, Mheshimiwa Mbatia ameona udhaifu katika Serikali. Hoja za kusema kwamba, tukiunda Kamati kuna gharama, ndiyo *education is expensive*, kama tunataka tuwe na Taifa lenye maendeleo na kuwajibika ni lazima tugharimie elimu. Mabadiliko yanayoletwa na Serikali ni kuzima kazi ya Bunge isifanyike. Kwa hiyo, ninaomba tu-stick kwenye hoja tusitafute kichaka cha kujificha, tu-stick kwenye hoja ya Mheshimiwa Mbatia, iundwe Kamati tuchunguze tukokotoe madudu yote ambayo yako ndani ya Wizara hii ili tuboreshe elimu na Kamati Teule zina mamlaka, huwa zinaingia ndani zinaona uozo, zinaona ubabaishaji na ndiyo maana tuna Mawaziri wababaishaji hapa, wanaleta mambo ya ajabu kabisa, wamekuwa na shule zimefungiwa mahali fulani zinakuwa na mambo kama hayo.

SPIKA: Jadiini hoja, tatizo letu Waheshimiwa Wabunge, naomba ninyi nyote mliosimama make kwanza. Tatizo la Waheshimiwa Wabunge wangu ninyi ni kuchukua vitu *emotional* na kutokuelewa. Udhifu wa elimu *is a very broad subject*; kwa hiyo, kuiundia Kamati Teule *a broad subject* itakuwa ngumu.

Alichosema Mheshimiwa Mbatia hapa, mnaweza kuunda Kamati Teule kama sita hivi au saba, haiwezi kuwa moja. Haiwasaidii ninyi kunijibu, mimi naeleza. Kwa hiyo, tunachokisema lazima tutumie busara katika kufanya jambo fulani na lazima tutumie busara kusudi tupate kile tunachokitaka. Ukiunda Kamati Teule kama ilivyo hapa sijui utapata nini mwisho wake, lazima urudi kwenye sera tu. Kwa sababu *the whole thing* ni muundo na ndiyo maana nasema msihamaki, hoja ya Mheshimiwa Mbatia ina mantiki, hakuna anayebishana kwa hilo, ila ni namna gani tunatakiwa twende, hilo ndilo swal. Kwa hiyo, sasa nimwite nani; nimwite Mheshimiwa Mkosamali na uzungumze hoja siyo *feelings* zako.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru, nitazungumza hoja.

Mheshimiwa Spika, naanza na Kanuni ya 117(2) inasema; "Bila ya kuathiri masharti ya fasili ya kwanza.

SPIKA: Ya kwanza; sasa!

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Ya Kanuni hii, baada ya kujadili hoja yoyote Bunge linaweza kuunda Kamati Teule kwa madhumuni ya kushughulika na jambo lolote linalotokana na hoja hiyo kwa utaratibu ufuatao".

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ...

SPIKA: Usome na ya kwanza, inasema bila ya kuathiri masharti.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Ya kwanza inasema Kamati Teule inaweza kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalum, kwa hoja mahususi itakayotolewa au kuafikiwa. Lakini ya pili, sasa ...

SPIKA: *Underline* mahususi.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Naomba unisikilize sasa nifafanue.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya pili inasema, jambo lolote linalotokana na hoja mahususi linaweza kuundiwa Kamati Teule.

SPIKA: Soma tena. Soma ile unayotaka kusoma.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, huelewi nini? Labda nirudie ya kwanza na ya pili.

SPIKA: Wewe Mheshimiwa Tundu Lissu unahangaika, nasema usome, soma vizuri sana.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Narudia tena Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Ndiyo.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Naomba unisikilize; Kamati Teule inaweza kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalum, kwa hoja mahususi itakayotolewa au kuafikiwa. Hoja imetolewa na Mheshimiwa Mbatia, hiyo ndiyo hoja.

SPIKA: Endelea kusoma.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Ya pili inasema hivi: "Bila ya kuathiri masharti ya fasili ya kwanza ya Kanuni hii, baada ya kujadili hoja yoyote, Bunge linaweza kuunda Kamati Teule kwa madhumuni ya kushughulikia jambo lolote. Kwa hiyo, hilo jambo mahususi linaweza kuwa na mambo mengi. Tunaweza tukaunda Kamati Teule ambayo itashughulikia ujisadi uliopo humo ndani unaohusu mambo ya UNESCO na nini, tunaweza tukaunda kushughulikia hilo, tunaweza tukaunda kushughulikia mitaala na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pia nataka nikufahamishe watu hawajaelewa vizuri hii hoja, hoja ya Mheshimiwa Mbatia inasema hivi; ninaomba Bunge lako Tukufu kuunda Kamati Teule ya Bunge kuchunguza kina cha udhaifu huu wa kimfumo katika Sekta ya Elimu hapa nchini. Aidha,

ikiwezekana Kamati hiyo ipendekeze hatua za kuchukuliwa ili Taifa liondokane na udhaifu huu hatari. Tunataka Kamati hii ndiyo iende ichunguze, Serikali haiwezi kujichunguza. Hatuwezi tukaiachia Serikali iende kujichunguza na ndiyo maana hii hoja imetoka kwa Mbunge.

Kwa hiyo, lazima tuunde Kamati Teule ikachunguze kwa niaba ya Bunge itoe mapendekezo ni nini tukifanyi kutokana na udhaifu huu. Sasa watu hawajaelewa hoja inataka nini, inachotaka ni hicho, siyo kitu kingine. Siyo Sera, kuna mambo mengi; kuna ujisadi ambao umezungumzwa hapa, kuna vitabu vimechapishwa haieleweki kwa utaratibu gani, lazima tujue.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri wa Kazi.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, kama tulimsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri, alipokuwa anatoa maelezo, amezungumzia suala la Sera ya Elimu. Kwamba ni wakati mwafaka sasa Sera hii ikaletwa hapa ikafanyiwa mabadiliko makubwa, kwa sababu Sera ndiyo inayotoa mwongozo na mtazamo na *policy statements* ili sasa baada ya hapo muunde *curriculum*. *Curriculum* pamoja na *syllabus*, kwa wale tunaoelewa masuala ya elimu ni matokeo ya Sera.

Suala alilolizungumza Mheshimiwa Mbatia yeye ameji-*confine* kwenye vitabu na kwenye *curriculum* na katika kuchanganya pia hakueleza vizuri maana ya ile *curriculum*. Sasa Sera itakapokuwa imeshughulikiwa imebadilishwa, imefanyiwa marekebisho na hayo marekebisho tutapenda pia tufahamu Mheshimiwa Mbatia anasema nini, wadau wengine wanasema nini, Bunge linasema nini kuhusiana na mabadiliko ambayo tunafikiri sasa yataleta mwongozo wa kuleta *curriculum* ambayo itatengenezwa na Taasisi ya Elimu, lakini pia *syllabus* ambayo ndiyo inazaa vitabu na waandishi wa vitabu kubadilisha vitabu, kuweka *text book* moja na mambo kama hayo.

Kwa hiyo, nafikiri sasa kujadili badiliko la Mheshimiwa Waziri ili Serikali iendelee kuleta hayo mabadiliko ya Kisera, mabadiliko ya Kisera yalete mabadiliko ya *curriculum* kama kuna haja, lakini pia uandishi wa vitabu uweje na hayo yote yatakuwa yamekuwa *incorporated* katika masuala ambayo ameyaleta Mheshimiwa Mbatia. Kwa hiyo, nashauri kwamba, mabadiliko ya Mheshimiwa Waziri ni muhimu tuyatekeleze kwa sababu hiyo ni kazi ya Serikali. (*Makof*)

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi niweze kulijadili suala hili kidogo. Kwanza, naunga mkono maelezo ya kina aliyyoyatoa Mheshimiwa Waziri. Naunga mkono kwa sababu kwenye ule ukurasa wa tatu, ameelleza wazi kwamba, ile rasimu tayari imeshapitiwa mwezi Juni, 2009. Kwenye ukurasa wa tatu, samahani Waheshimiwa Wabunge, walipitia Rasimu ya Sera tarehe 24 na 25 Aprili, 2010 na tarehe 13 Novemba, 2011. Hii rasimu ya Sera ya Elimu tayari sisi tumeipitia, lakini wanasema tena kwamba, maoni ya Waheshimiwa Wabunge na Wadau wengine, yamejumuishwa katika rasimu ya mwisho ya sera na maandalizi ya mkakati wa utekelezaji wake yapo katika hatua za mwisho, ambavyo vitawasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri mwisho wa mwezi Machi, 2013. Hili jambo litakuja tena kwetu tutalipitia vizuri. Mimi nadhani tuiachie Serikali ifanye hivyo.

Katika eneo lile la pili, Kanuni zetu zinazeleza wazi kwamba, tunatakiwa tushughulikie suala ambalo ni maalum (*specific objective*). Kilichokuwa kimezungumzwa na Mheshimiwa Mbatia ni *general objective*. Wewe kama mwalimu unakuwa na *general objective* ambayo Mheshimiwa Mbatia ameizungumzia, lakini hiyo *general objective* unaweza kuwa na *specific objectives* zaidi ya tano. Sasa ukiangalia kwenye maelezo yake haya, yanaweza kuwa na *specific objective* kama uliyosema Mheshimiwa Spika zaidi ya nane zipo humu ndani, kama wewe ni mwalimu. Mimi ninayezungumza ni mwalimu; *specific objectives* zilizokuwa humu ni

nyingi mno na sisi kama Bunge kazi yetu kushughulikia *specific objective* na siyo *general objective*.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nasema tena, bado tuiachie Serikali ifanye kazi yake ilimradi ituletee baadaye tutaipitia tutaichambua, lakini siyo kuunda Tume kwa ajili ya kushughulikia *general objectives* siyo kazi yetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

SPIKA: Tumeongea, nimruhusu Mheshimiwa Jenista Mhagama.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kimsingi, ninachokiona mbele ya Bunge lako Tukufu leo ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge wote, wanajenga nyumba moja. Ninaposema wanajenga nyumba moja, nina maana gani Mheshimiwa Spika? Wabunge hapa kila aliyesimama hakuna ambaye hajakiri kwamba, yapo matatizo makubwa katika mfumo wa elimu katika Nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Kama hivyo ndivyo, hakuna Mbunge aliyesimama leo ndani ya Bunge lako Tukufu akasema kwamba, hoja ya Mheshimiwa Mbatia haina msingi, hayupo. Wote tumekubali kwamba, hoja hii ni ya msingi kabisa ili kuweza kuboresha mwenendo na mfumo mzima wa elimu katika nchi yetu kwa hatua iliyopo sasa na kwa hali tuliyofikia sasa. Baada ya sisi wote kukubaliana hilo, kwa maana ya kwamba Waheshimiwa Wabunge wote hapa ndani leo tumeshika fito zetu tukijenga nyumba moja ya kuimarisha na kuboresha mfumo wa elimu na tukizingatia yale maudhui yaliyokuja kwenye hoja ya Mheshimiwa Mbatia, kinachofuata hapa ni kutazama ni namna gani nia hii njema inaweza ikatimia ili kweli dhamira safi yetu sisi Waheshimiwa Wabunge itekelezwe na Serikali yetu ya kuboresha mfumo huu wa elimu.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ndizo zinazotugonganisha na kila mtu sasa anasimama kutafsiri Kanuni kwa kadiri anavyotaka hoja hii ichukuliwe leo. Hivyo, tunajikuta tunaondoka kwenye hoja ya msingi ya kuboresha elimu ya nchi yetu, tunaingia katika ubishani wa Kikanuni wa namna ya kila mtu anavyofikiri sasa hoja hii ifanyike. Naona kwetu sisi hii si busara sana lakini busara tungetizama nini ambacho kinaweza kikatusaidia.

Mheshimiwa Spika, ukituacha Wabunge sisi hapa ndani, Watanzania wote na wao wameinuka na wanajadili kwa kina suala la mustakabali wa elimu. Sasa basi nitaendelea kuongea na Kiti chako na nitaeleza haya ninayotaka kuchangia. Kwa kuwa hali iko hivyo ilivyo na ukiitazama hoja ya Mheshimiwa Mbatia kabla ya kuhitimisha hoja yake akiomba Bunge liunde Kamati Teule, ameinisha mambo bayana kadhaa. Kanuni hazimfungi Mbunge yeoyote sasa, baada ya kuyaona hata yale mambo kadhaa yaliyoainishwa kwenye hoja hii ya Mheshimiwa Mbatia kama yanahitaji kufanyiwa mapitio ya kina, upembuzi wa kina, Kanuni zinamruhusu sasa anao uwezo wa kuleta hoja yake hapa Bungeni ya kuomba Kamati Teule kwa jambo mahususi; na anaweza akateua kati ya haya mambo mazito yaliyosemwa na Mheshimiwa Mbatia, jambo gani mahususi anafikiri lifanyiwe kazi kwa kina. Kwa maana ya hoja yenewe nzima jinsi ilivyo, huwezi kuunda Kamati Teule kwa hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana Bunge hili lielewe ni namna gani nzuri ya kushughulikia hoja hii. Ninafikiri kuna umuhimu wa Wabunge kuendelea kuona na kuangalia michango tulioifanya katika kuboresha Sera ya Elimu, imizingatia vipi mambo haya yaliyosemwa na Mheshimiwa Mbatia na yanayosemwa na Watanzania wote. Hii inaweza ikafanyika tu kuititia Sera hii inayoboreshwa sasa hivi na siyo vinginevyo. Baada ya kuona hilo, mimi naendelea kushauri cha msingi hapa ni Watanzania wote kuitazama Sera yetu na kama tunaitazama Sera hiyo tutaifanya kazi hiyo kuititia Serikali na hata sisi Wabunge tukitaka tuna

uwezo wa kushirikiana kwa pamoja na jambo hili likafanyika. Vinginevyo, hoja zozote zilizoletwa hapa zinaweza kuundiwa Kamati Teule kwa mfumo wa Kikanuni tuliuouweka.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kumalizia kwa kuunga mkono suala hili liachwe kwa Serikali na sisi Wabunge tuisimamie Serikali kuhakikisha haya mambo yote yanafanyika. (*Makofii*)

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nashukuru sana kwa nafasi adimu sana ya mimi nami kujaribu kulitazama jambo hili. Jambo hili ni jema, tatizo lipo katika utaratibu tu. Kama ilivyoelezwa tuzisome vizuri Kanuni, kama yupo Mbunge anayeweza kunyanyuka na kitu mahususi katika yaliyopo hapa, kufuatana na Kanuni hilo linakubalika. Tatizo tu ni kwamba, jambo hili ni pana na Kanuni zinatuambia jambo liwe mahususi. Tukienda kwa lugha ile ya wenzetu wa Kiingereza kama alivyoeleza Mheshimiwa Marombwa kwamba, hapa Mheshimiwa Mbatia, alichoshughulika nacho ni *broad objective*.

Hoja ya kwanza iliyopo ukurasa wa tatu kuhusu Sera ya Elimu iliyopo kuwa ya muda mrefu, ukurasa wa tano hoja kuhusu udhaifu katika vitabu vya kiada na ziada, ukurasa wa sita anahoji kuhusu vitabu vilivyotolewa na *USAID* na hoja nyingine ziko *specific objective* nne kwa maana kwamba, katika mazingira ya kawaida zilitakiwa ziundwe Kamati Teule nne kwa wakati mmoja; kitu ambacho hakiwezekani kufuatana na Kanuni zetu.

Kwa hiyo, mimi nashauri tufuate tu Kanuni; vinginevyo, mahali alipofika Mheshimiwa Spika ni pa kuhoji tu tusonge mbele. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Nampa nafasi msemaji mmoja tu, Mheshimiwa Nassari.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru ingawa jirani zangu wanalamika kwamba, hujazingatia *gender* lakini nashukuru kwa kunipa nafasi. Ninachokiona mbele yetu ni Wabunge kukimbia kazi zetu za Kibunge, kwa sababu *we are watch dogs* kwa Serikali. Kazi ya Bunge ni kuisimamia Serikali, lakini nasikitika kwamba, baadhi ya Wabunge hapa leo wanakimbia majukumu yao, badala ya kuisimamia Serikali wanataka kuiachia Serikali ijisimamie yenye.

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye hoja. Anachosema Mheshimiwa Mbatia kwenye hoja yake na nafikiri Mheshimiwa Mkosamali amejaribu kuilezea vizuri sana, lakini bado tunaonekana hatumuelewi. Mheshimiwa Ole-Sendeka amesimama anasema kwamba, Bunge haliwezi kuunda Kamati Teule kwa sababu sisi Wabunge siyo wataalam wa mambo ya mitaala, mambo ya sera na mambo mengine. Mwaka 2007 kwenye Bunge hili iliundwa Kamati Teule hapa ikawa inaongozwa na Mheshimiwa Mwakyembe na Mheshimiwa Ole-Sendeka ulichangia kwa hisia kubwa sana kwenye sakata la Richmond. Kipindi kile ulikubali Kamati Teule iundwe wakati Bunge si TAKUKURU; kwa nini Bunge lilifanya kazi yake?

SPIKA: Ngoja nikusaidie hapo, hakusema hivyo.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Spika, leo mnakataa Bunge lisiunde Kamati Teule; kwa nini tunakimbia majukumu ya Bunge ya kuisimamia Serikali?

SPIKA: Hapana, nataka tumpate mwenzetu, Mheshimiwa Ole-Sendeka hakusema haiwezi kuundwa Kamati Teule.

WABUNGE FULANI: Alisema.

SPIKA: Hakusema hivyo, *Hansard* ipo.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Spika, niendelee lakini alichokisema alisema Wabunge si wataalam, kwa hiyo, hatuwezi. Ndicho alichokisema na *Hansard* zipo na kama kuna *record* ioneokane. Kwa hiyo, kinachofanyika hapa ni kwamba, tunakimbia majukumu yetu. Mheshimiwa Mbatia, ameweza wazi tu, ameeleza udhaifu uliopo kwenye sera, kwenye mitaala na amesema Bunge liunde Kamati Teule. Kwa nini tunakataa kuunda Kamati Teule? Kwa nini tunakataa kuisimamia Serikali; Serikali itajisimamia vipi yenye?

Mheshimiwa Spika, leo hii tunazalisha wasomi ambao hawajui kuhoji, tunazalisha watoto badala ya kuwa *job creators* wanakuwa *job seekers*. Juzi tumeona matokeo hapa ya darasa la saba, mpaka wanafunzi wenye D wanaingia Sekondari, tumeona juzi Serikali inawaongezea wanafunzi maksi ili waweze kufaulu kuendelea na Sekondari. Udhaifu wote huu mnaipa hiyo hiyo Serikali ambayo imeshindwa kuisimamia Sekta ya Elimu eti leo iende ikajisimamie yenye ijichunguze! Mimi sidhani kama kweli tumekuja Bungeni kufanya kazi yetu kama Wabunge na kwa namna hii kama tukienda hivi, haina maana ya sisi kuwepo hapa na wala haina maana ya wewe kuwepo kwenye hicho Kiti hapo. Nakushukuru. (*Makof!*)

SPIKA: Nataka nijitetee mwenyewe. Sikilizeni Waheshimiwa Wabunge, kitu ambacho mnabishana hapa wala hakipo; ni kwamba, ninyi nyote mnasema kitu kimoja kabisa kwa sababu udhaifu wa Wizara ya Elimu hakuna anayepinga. Sasa *how to do it*, ndio tunasema ukiunda Kamati Teule kwa mujibu wa maeleo yote aliyotoa Mheshimiwa Mbatia, zitakuwa Kamati Teule kama nane hivi. Kwa sababu...

MBUNGE FULANI: Toeni pesa.

SPIKA: Mheshimiwa Wenje, mimi nazungumza, *I don't even hear what you are saying in fact*. Kwa hiyo, tunachokisema hapa tuangalie *how best* tunaweza kuingia kwenye Wizara ya Elimu *totally* na kuiangalia yote. Sasa huwezi ukaipelea kwenye Kamati Teule, Kamati Teule inatawaliwa na kifungu cha 117, haitawaliwi na kifungu kingine chochote. Sasa mtoa hoja alikuwa Mheshimiwa Waziri, hebu Mheshimiwa Waziri wasilisha hoja yako tufanye maamuzi.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, nitangulize kutoa shukrani kwa michango yote ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge katika hili ambalo tunalijadili hivi sasa. Sisi Serikalini baada ya kuipokea hoja, tumeitafakari sana na kuona maeneo kadhaa bado yanahitaji kufanyiwa kazi, pamoja na mafanikio kadhaa ambayo tumepata kwa miaka mingi. Mafanikio ya kuringia na ambayo yanatolewa mifano duniani, lakini tumekiri kwamba, kuna maeneo kadhaa ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi. Haya tumeyaona kabla ya hoja hii na ndio sababu tukaanzisha mchakato wa kufanya mapitio makubwa katika Sera. Mapitio haya yamechukua muda mrefu kwa sababu masuala ya changamoto ambayo yametajwa katika hoja ya Mheshimiwa Mbatia ni mengi na ni mazito. Ndiyo maana Bunge lako liliipitia Sera hii kwa mara ya kwanza mwaka 2010, likapitia tena Novemba, 2011. Siyo jambo la kawaida Wabunge kupitia Sera moja au Rasimu ya Sera moja mara mbili.

Hivi sasa kuna wito kuwa Sera hii irudi tena Bungeni. Kwa hiyo, maudhui na mambo ambayo yamo yanahitaji kufanyiwa kazi; ni mambo makubwa ambayo yanatakiwa yafanywe kiukamilifu ili maeneo mengi haya katika ngazi mbalimbali, iwe elimu ya awali au elimu ya msingi au ya sekondari ama elimu ya juu, yote yaweze kukaa katika hali ambayo tunaitaka kama Watanzania na hali ambayo itatufikisha mwaka 2025 kufikia hadhi ya Taifa lenye uchumi wa kat.

Mheshimiwa Spika, kazi hii kubwa tayari imeshafanywa na Bunge na Wadau mbalimbali nchi nzima kama tulivyoainisha na tulichukua muda mrefu kubadilisha Sera. Nataka kuliomba Bunge lako Tukufu, liridhie mabadiliko haya ya Azimio kama tulivyoyawasilisha ili tuweze kufanya kazi hii kwa nguvu yetu yote na kwa uharaka tuweze kupata mafanikio ambayo yanatakiwa kuitia hoja ambayo Mheshimiwa Mbatia ameyataja hapa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

SPIKA: Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hoja ya Serikali imekubalika. Tukirudi saa kumi na moja jioni tutaanza kujadili.

Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(*Saa 6.33 mchana Bunge lilitifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia*)

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Mheshimiwa Mkuchika!

MHE. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Spika, nimesimama kuomba Mwongozo wako na nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64(g), kifungu hiki kinazungumzia mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. Asubuhi hii Mheshimiwa Msigwa, Mbunge wa Iringa Mjini wakati anajadili mada iliyoko mbele yetu alisema maneno yafuatayo:-

“Mawaziri wababaishaji”.

Mheshimiwa Spika, kifungu (g) kinasema Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kulalamika kuwa Mheshimiwa Msigwa, mimi ninamheshimu tena Reverend, Mchungaji, Baba Padri, sikutegemea Baba Padri atuite Mawaziri, Wabunge wenzie kuwa sisi ni wababaishaji.

Mheshimiwa Spika, ninavyofahamu mimi, Mawaziri wa nchi hii ni watu makini, wanamsaidia Rais kuendesha nchi hii na ndiyo maana tumevuka salama mpaka leo hii. Mimi nimetoka Addis Ababa kwenye mkutano wa APRM ambapo Tanzania tulikuwa tunajadiliwa na tumeonekana kuwa ni moja kati ya nchi za mfano bora katika Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mwongozo wako kwamba mimi kama Waziri na Wabunge wenzangu na wale tunaowaongoza, Mheshimiwa Msigwa ametudhalilisha kutuita wababaishaji, ninaomba Mwongozo wako.

SPIKA: Maneno haya ninakumbuka alisema lakini nilimwambia aende kwenye hoja na akasema anaenda kwenye hoja. Kwa hiyo, ni kweli yanaudhi lakini alirudi kwenye hoja.

Ninaomba tuendelee na Mheshimiwa Margaret Sitta, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika hoja muhimu sana aliyotoa Mheshimiwa Mbatia inayohusu udhaifu katika sekta ya elimu. Ninampongeza sana Mheshimiwa Mbatia kwa sababu ni ukweli usiopingika kwamba kuna haja ya kuangalia upungufu uliopo katika sekta ya elimu ili nchi yetu iweze kutoa elimu bora.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma ya Jamii na wenzangu ambao ni Wajumbe katika Kamati hii watakulaliana na mimi kwamba ni ukweli usiopingika pia kuwa wiki iliyopita tulikuwa na kikao na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu na katika mambo ambayo tuliyajadili kwa kina ni umuhimu wa kuleta Rasimu ya Sera ya Elimu iliyofanyiwa marekebisho. Tunajua kuwa Sera ya Elimu iliyopo sasa hivi imepitwa na wakati kwa sababu ni ya tangu mwaka 1995 na Sera lazima isaidie kujibu hoja na mahitaji ya kielimu ya muda uliopo sasa.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka Sera ya Elimu ifanyiwe kazi haraka iwezekanavyo na ndio maana nimempungeza Mheshimiwa Mbatia kwa sababu huu ni wakati muafaka wakati Kamati ya Huduma za Jamii ikihimiza Serikali kufanya kazi marekebisho ya Sera ya Elimu. Kwa kifupi ni kuleta Sera mpya ambayo kama nilivyosema itakwenda na wakati uliopo sasa hivi. Tumekuwa na vikao vitatu na Waheshimiwa Wabunge ninyi ni mashahidi kikao kimojawapo wote tulihuishwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kwa kupitia Rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo katika moja ya kumbi zetu za Pius Msekwa, tulipitia, tukatoa maoni yetu. Kwa hiyo, kwa kuwa ni wajibu wetu sisi Wabunge kusimamia Serikali, ni kuitaka Serikali ilete rasimu ya Sera ya Elimu ambayo itakuwa imezingatia maoni ambayo tulitoa na kama itakuwa hajazingatia maoni tuliyotoa bado tuna wakati wa kuitaka Serikali izingatie maoni ambayo tulitaka yaingizwe katika rasimu ya Sera ya Elimu.

Waheshimiwa Wabunge, tuitake Serikali pia kuwa katika Sera ya Elimu itakayoletwa yaani Rasimu, iwe na mkakati wa utekelezaji kwa mfano kama watasema kuwa wataimarisha elimu ya awali basi ionyeshe mkakati wa ambavyo itafikiwa azma hiyo ya kuimarisha elimu ya awali nchini mwetu. Kwa hiyo, tuitake Serikali ilete Sera ya Elimu yenye mkakati wa utekelezaji na kama kutakuwa na program zozote zitakazohusika basi zitajwe mle na pia tuitake Serikali kuonyesha muda itakayochukua kuleta hapa yaani kuwe na muda maalum wa kufanya kazi yaani *timeframe*. Tusiwaache hivihivi waelee tu. Tuwabane watupe muda kuwa ni lini watawasilisha rasimu mpya ya Sera ya Elimu ili na sisi tuone kama kweli tunayoyataka sasa hivi kwa mahitaji ya elimu ya sasa yanazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuwatake Serikali wapanue uwigo, ili wawahuushe wadau wengi zaidi. Ni kweli kabisa kuwa Wizara ya Elimu ilihuisha wadau lakini tuitake ihushe wadau wengi zaidi kwa sababu suala la elimu ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi hii. Tukiwa na Sera mpya maana yake tutakuwa na Mtaala mpya, tutakuwa na Muhtasari mpya kwa msingi huo Muhtasari pia utaeeleza hata aina ya vifaa vitakavyohitajika ili tufikie azma ya Sera kama itakavyotuelekeza.

Mheshimiwa Spika, haitoshi kama tutakuwa na Sera nzuri, Mtaala mzuri, Muhtasari mzuri, vifaa vizuri bila kuzingatia Walimu ambao ni watendaji. Kwa hiyo, tuwatake Serikali pamoja na kuleta Sera ya Elimu na mkakati wake ilete pia jinsi itakavyoboresha mfumo wa kutoa huduma kwa Walimu. Kwa sababu unapotafsiri shule maana yake ni Walimu na wanafunzi hayo mengine yote yanafuata kama vile madarasa, vitabu na mengineyo. Walimu tuwaangalie sana. Tuitake Serikali ije na mpango wa kuleta chombo kitakachohudumia Walimu.

Mheshimiwa Spika, tazama sasa hivi hali ilivyo, Walimu wanashindwa kupata haki zao kwa wakati kwa sababu *DED* au Halmashauri zinatoa mshahara, lakini anayepandisha madaraja na kuweka mkataba na Walimu ni *TSD* na *TSD* iko Utumishi. Anayeadhibu, anayesimamisha kazi, anayetoea *secondment* ni *TSD* ambayo imepunguzwa imekuwa ni Idara ndogo ndani ya Ofisi ya Rais, Utumishi. Kwa hiyo, tuitake Serikali irudishe *TSC* Tume ya Utumishi kwa Walimu ambayo ndiyo itakuwa inaweka mkataba na Mwalimu, inasajili, inaangalia taaluma yake na wakati huohuo inampa haki zake, inamuadhibu, inampa *secondment* na kadhalika. Hali ilivyo sasa hivi hali ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ukiangalia kutokana na mchanganyiko wa kuhudumia Walimu ulivyo, Walimu wa Urambo kwa mfano mpaka sasa hivi Walimu 363 hawajapandishwa madaraja, watafanyaje kazi hawa kwa moyo? Hata ukiwa na Mtaala na Sera mpya bila kuangalia Walimu, haiwezekani! Angalia Manispaa ya Tabora, Walimu 261 hawajapanda madaraja mpaka sasa, nimetoa mfano tu lakini Walimu wa Urambo ambao walipandishwa madaraja wanadai Serikali shilingi milioni 374 za *areas* za mshahara baada ya kupandishwa madaraja lakini wakati huohuo Manispaa nao wanadai shilingi milioni 270 za *areas*. Huo nimetoa mfano mdogo tu. Sasa kwa hali kama hii, wakati watu wanaotakiwa kutekeleza hiyo Sera mpya kwa vitendo watakuwa na unyonge kwa kuwa haki zao hazifiki kwa wakati, kutokana na mfumo mbaya wa kuhudumia Walimu uliopo ambao unaonyesha kuwa umeshindwa.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuibane Serikali ije na mfumo wa kuhudumia Walimu na sisi tunapendekeza irudishwe *TSC* na *TSC* kule ilipopotezwa ikaitwa *TSD* irudi. Serikali yetu ni sikivu na inakubali kujisahihisha, isikie kilio cha Walimu, irudishe *TSC* ipewe nguvu kama walivyo wenzetu nchi za jirani, wakaone nchi jirani zinavyofanya kazi kwa kuwa na chombo kimoja tu kinachomhudumia Mwalimu. Kutakuwa hakuna madeni yanayolimbikizwa kila mwaka, kutakuwa hakuna watu wanaodai madaraja yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Sera nzuri, Muhtasari mzuri na Walimu kuhudumiwa vizuri, kama hatutaimarisha ukaguzi ni kupoteza wakati. Tulikwenda Kinondoni wiki iliyopita tukifuatana na Naibu Mawaziri husika, tukakuta Wakaguzi wa shule 22 wako katika chumba kimoja, wanatoka jasho, wamekata tamaa lakini wakatuambia kuwa wamepata shilingi milioni moja na laki mbili tu kufanya ukaguzi wa shule 55, wakaweza kufanya ukaguzi wa shule nane (8) tu.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali yetu itadharau ukaguzi, ni nani atakayekwenda kuona kuwa hiyo Sera inatekelezwa vizuri, Mtaala unakwenda vizuri na Muhtasari nao unafanyiwa kazi vizuri. Mimi ombi langu ni kwamba pamoja na yote mazuri Serikali itakayoyafanya, suala la ukaguzi naomba mtuunge mkono sisi Kamati ya Huduma za Jamii, kuitakaWizara ya Elimu kuwa katika kikao chochote tutakachofanya nao sasa watuletee mkakati wa kuibadili Idara ya Ukaguzi iwe Wakala unaojitegemea ili waweze kupata fedha za kutosha na kufanya kazi vizuri, kwa sababu bila kuwafuatilia Walimu kwa karibu pia inakuwa vigumu kubaini upungufu uliopo.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kusema kuwa Waheshimiwa Wabunge tuazimie hapa, tuitake Serikali ituambie ni lini italeta Sera mpya yenye mkakati ambayo itatuonyesha Mtaala mpya, Muhtasari mpya na mambo yote yale. Kwa sababu watu bado wana wasiwasi kwa kuwa hata idadi ya vipindi kuna watu wanajadili hivi kweli darasa la kwanza linaweza kuwa na masomo12? Katoto ka-darasa la kwanza kanaweza kuwa na vipindi 12? Haya ndiyo mambo ya kuangaliwa. Vitabu vinapobadilishwa, vinapoletwa vitabu vipyta, zamani kulikuwa na utaratibu wa kufundisha Walimu kwanza. Walimu wana vituo vya Walimu. Zamani ilikuwa kama kuna mabadiliko yoyote hata kama ni madogo ya kitabu, wanaitwa Walimu, wanasaidiwa katika vituo vyao vya Walimu. Sasa haya ndiyo tuibane Serikali ituletee. Kwa hiyo, tunataka Sera yenye

mikakati ya utekelezaji ambayo itatufafanulia kila hatua ambayo watachukua ili kweli nchi yetu itoe elimu bora. Pamoja na kuangalia chombo cha Walimu kitakachowahudumia vizuri na pia kuimarisha ukaguzi kwa kuwa na chombo huru kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, ninaomba nirudie kumpongeza Mheshimiwa Mbatia,. Amefanya kazi nzuri, amechambua vizuri hoja, sasa tushirikiane wote kuibana Serikali ili itimize yale ambayo inapaswa kufanya ili nchi yetu itoe elimu bora, ninashukuru. (*Makof*)

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu. Kwanza, ninaungana na Mheshimiwa Sitta na Mheshimiwa Mbatia, kwa kazi kubwa na nzuri, kazi ya utafiti ambayo amefanya, wote ni mashahidi tumesoma alichokiandika. Ninachotaka kusema hapa, ni kweli Serikali imefanya kazi kubwa kupanua elimu ya msingi, hakuna mtu anayekataa, shule ni nydingi na pia ni kweli kuwa Serikali imefanya kazi kubwa ya kupanua elimu ya sekondari hasa ukizingatia shule hizi za Kata.

Mheshimiwa Spika, lakini ni kweli kuwa viwango vya elimu katika nchi hii vimeshuka sana kwenye *level* ya shule za msingi na katika *level* ya shule za sekondari. Baada ya kujenga shule nydingi na kuongeza idadi ya wanafunzi wa shule za msingi na pia kuongeza shule nydingi za sekondari na idadi ya wanafunzi wanaomaliza shule za sekondari tutaongezaje ubora wa elimu na ndiyo kinachogombaa hapa. Elimu yetu iwe ya hali ya juu kama ile ya zamani. Kwa hiyo, ni lazima tukubaliane na mambo aliopendekeza Mheshimiwa Mbatia na ningeomba Serikali iyatekeleze.

Mheshimiwa Spika, moja ambalo ninaweza kusema, zile dola milioni 20, zilizotolewa na *USAID* kwa Serikali ya Tanzania kwa ajili ya kuchapisha vitabu hivi, mimi katika Jimbo langu la Vunjo hivyo vitabu vya kiada na ziada sidhani kama viro vya kutosha katika kila shule. Je, ni kweli kuwa fedha zile zinafanya kazi? Tutaletewaje fedha kutoka Marekani sisi Watanzania halafu *type setting* tunafanya Malaysia! Ni kazi gani ambayo haiwezi kufanyika hapa Tanzania jamani mbona tunakuwa na wasiwasi? Ku-print vitabu Kenya maana yake ni kuzitoa nje ya Tanzania, unakwenda Malaysia unafanya hiyo *type setting* fedha zinalipwa kule, unaenda Kenya una *print* fedha zinaenda kule, kwa nini tunafanya hivyo?

Mheshimiwa Spika, hivi vitabu vya *Primary School* hatuwezi kuvisimamia na kuvichapa hapa nchini, zile dola milioni 20.4 zikabaki hapa ndani ya Tanzania? Au zile fedha tunazozungumza zinakwenda Uswisi ndizo hizi? Ushahidi si ndiyo huo! Kwa hiyo, mlivyosema kuwa Mbatia awe na *specific issue* kuna *specific issue* kuliko dola hizi milioni 20.4 ambazo wamesema zimetumika kifisadi? Kwa hiyo, ninaomba Serikali ituambie fedha zile zimekwenda wapi? Je, *CAG* amekagua hizo fedha kuwa ni kweli zimetumika kuchapa vitabu au ni porojo tunazoletewa hapa? Ndiyo ulikuwa wasiwasi wa mwenzetu, tunamuunga mkono na tunaitaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano ituambie kwa nini tunafanya hivi, kwa nini tunaletewa fedha nydingi milioni 20 halafu zinatolewa nje ya nchi kwa mambo ambayo tunaweza sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mimi ninakubaliana na Mheshimiwa Mbatia kwamba tutengeneze Sera nzuri na Serikali ifanye hivyo ileté hapa, mambo ya Mitaala na Muhtasari, vitabu vya kiada na ziada, tunaunga mkono, suala hili ni muhimu kama alivyoonyesha kwenye taarifa yake. Vitu hivyo vitengenezwe na visimamiwe, Serikali ivilete hapa tuone cha kufanya. Lakini hata kama ukiwa na Sera nzuri na Mitaala mizuri na hivi vitabu vyenyewe havitoshi bado ninaungana na Mheshimiwa Sitta kwamba mbona tuna matatizo mengi ya Walimu. Mimi nilitegemea haya matatizo ya Walimu hata leo pengine katika kuinua kiwango cha elimu ili kiweze kulingana na kule tulikotoka tungesema Walimu wetu tunawahudumia namna gani?

Mheshimiwa Spika, kwa mfano sasa hivi nimesikia juzi CWT bado inadai madeni ya shilingi bilioni 25 na wamesema ikifika mwezi wa tatu watagoma, hilo ni tishio tutaongezaje na utainuaje kiwango cha elimu Tanzania kama Walimu wanunung'unika kwamba ikifika mwezi wa tatu wanagoma? Ninaomba Serikali mtakapokuwa mna-*windup* mtuambie kuwa tutaachana lini na huu mgogoro wa Walimu kuwa wanadai fedha zao, wataendelea kudai mpaka lini? Madeni ya Vunjo kule ni zaidi ya shilingi bilioni moja, Walimu wale wanadai, kila siku wanunung'unika na kila siku wanalia, sasa wamlilie nani, hilo ni kwanza.

Mheshimiwa Spika, mishahara ya Walimu, bado tunaendelea kusema kuwa mishahara ya Walimu ni midogo. Kwa hiyo, hata kama tukiwa na Sera nzuri, Mitaala mizuri na vitabu pia lakini kama mishahara ndiyo hiihii, kama Walimu wanahamishwa, hawapati posho zao, wanalamika kila siku, tutainuaje kiwango cha Walimu? Kule kwangu kero zao ndiyo hizo, motisha kwa Walimu limesemwa hapa na Mheshimiwa Sitta, Walimu wangu wamepandishwa vyeo lakini wanaishia kupokea barua, fedha hawapati wanapopandishwa madaraja, kwa nini hawapati hizo fedha jamanii? Waziri atakapokuja hapa atuambie wale Walimu ambao wamepandishwa madaraja lakini fedha zao hawajapata, watapata lini?

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho kinarudisha maendeleo ya elimu nyuma ni pensheni. Pensheni ya Walimu ukienda kwenye *salary slip* zao unakuta Mwalimu baada ya kufanya kazi ya miaka 30 analipwa shilingi 40,000 kwa mwezi. Je, tutaendelea na Mwalimu wa namna hiyo kama Walimu wanajua *at the end of the day* fedha atakazopewa ndizo hizo watafanyaje kazi kwa bidii?

Mheshimiwa Spika, mafunzo kwa Walimu, bado ninaiomba Wizara itoe mafunzo ya mara kwa mara, Walimu wapelekwe, waelimishwe, wapewe stadi za kazi yao, kuboresha mazingira wanakofanya kazi Walimu. Kuna shule Walimu wanalala madarasani katika nchi hii, asubuhi Mwalimu anakusanya vitu vyake darasani, asubuhi hiyohiyo watoto wanaingia darasani wanasoma. Katika mazingira kama hayo itakuwaje, nyumba za Walimu hakuna? Kwa hiyo, pamoja na hizo sera nzuri ambazo Mheshimiwa Mbatia ametusaidia na Serikali imeziona, pamoja na yote haya tuliyoyasema bado mkazo mkubwa uwekwe kwa Walimu wetu. Nasema tena Walimu wetu wana matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mbatia na ninaomba wote tuitake Serikali itekeleze hoja hii kama ilivyoletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Moses Machali, atafuatiwa na Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa fursa ili kusudi niweze kuchangia kwenye hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa James Francis Mbatia.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimpongeze Mheshimiwa James Mbatia kwa hoja yake nzuri na *ni-declare* tu moja kwa moja kwamba ninapenda kutofautiana na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundis kwamba mtazamo uliokuwa umewasilishwa na Mheshimiwa Mbatia kwamba iundwe Kamati Teule kwenda kuchunguza udhaifu katika sekta ya elimu kwamba badala yake jukumu hili liachiwe Serikali. Sikubaliani na wazo la Waziri, nitaomba kwa kweli aniwie radhi, ni vema niweze kueleza ni kwa nini.

SPIKA: Samahani Mheshimiwa Machali, kama hukubaliani sawa lakini hiyo siyo hoja imeshabadiishwa, ndiyo hii tunayojadili, ni hoja ya Mbatia lakini fainali yake ndiyo hii. Sasa ile kujadili unaturudisha nyuma, wewe jadili tu yale unayoyaona kuhusu udhaifu wa mfumo wa elimu kama alivyowasilisha Mheshimiwa Mbatia.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, bado sijatoka nje ya mada kwa sababu ninachokisema sikubaliani na mtazamo ule, hizo zote ni *school of thought*.

SPIKA: Tulishakubaliana sisi.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, ndiyo sikukubaliana na mtazamo ule ndiyo maana naelekeea kwenye mada, kwa hiyo huu ndiyo mtizamo wangu na *stand* yangu.

Mheshimiwa Spika, sikubaliani kwa sababu kwa mujibu wa *principles of natural justice*, wale Wanasheria wanafahamu kwamba *a person cannot be a judge in his own case or in his own cause*. Mtu huwezi kuwa ni Hakimu kwenye kesi yako wewe mwenyewe. Kwa sababu umefanya makosa, huwezi ukaja kama ni mahali ambako unatakiwa uweze kujipa adhabu huwezi kujipa adhabu, au huwezi ukajikosoa vizuri kwa sababu *human personality, always* katika *human psychology* huwa inaweza ikawa *judged* na wale ambao wanamtazama mtu, ndiyo maana huwa tunatumia vioo kama msaada kwetu kuweza kujisahihisha pale ambapo tunaona kwamba tumekosea.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba changamoto ambazo zimeainishwa kwenye hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa James Mbatia haziwezi zikatatuliwa na Serikali ileile, watu walewale ambao tayari wana dhamana ya kuweza kuyaona matatizo ambayo yanaikabili sekta ya elimu na hatimaye kuangalia kwamba ni nini kifanyike, wameshindwa!

Mheshimiwa Spika, mtaalam mmoja katika masuala ya elimu, Mwalimu wangu ambaye alinifundisha wakati nikiwa Chuo Kikuu nafanya Digrii ya Kwanza, ye ye alipata kutuambia kwamba maana ya elimu halisi, akasema *education refers to the process of transferring desirable habits, knowledge, skills and attitudes that makes an individual fit into the society*. Kuna mambo mawili, kwanza, anazungumzia tabia kwa maana ya *habit*. Pili, anazungumzia kwamba ili mtu aweze kuelimika na kuweza *ku-fit* kwenye jamii yake, anazungumzia suala la *knowledge* kwa maana ya maarifa na tatu ni ujuzi amba ni *skills* na nne ni *attitudes*.

Mheshimiwa Spika, katika hoja ya Mheshimiwa Mbatia, amezungumza kwamba Taifa letu hivi sasa linakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo suala la kukosekana kwa maadili mionganoni mwa Viongozi na hata wasiokuwa Viongozi, Taifa ni kama linapoteza mwelekeo. Nimejaribu kuititia taarifa mbalimbali za Serikali kwa mfano, yapo matatizo mengi na Serikali imekuwa na mipango mbalimbali ambayo mingine ni mizuri tu lakini utekelezaji wake umekuwa ni shida.

Mheshimiwa Spika, mfano hapa nina *document* moja ya Serikali ambayo *title* yake ni *The Education and Training Centre Development Program, Document* hii *Final Draft* ni ya Agosti mwaka 2001. Serikali ilidhamiria ku-decentralize sekta hii ya elimu tangu mwaka 2001 lakini kumekuwa na matatizo mbalimbali, bado hajjaweza kufikia malengo hayo. Suala la kwanza, ku-decentralize masuala mbalimbali bado imekuwa ni matatizo ukienda katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, jukumu ambalo leo hii tunasema tuikabidhi Serikali ndio iende ikalifanyie kazi, hiki kitu naomba niseme tutakuwa tunadanganyana mahali hapa. Nasema hivyo kwa sababu imetolewa mifano asubuhi ya vitabu, mifano ya vitabu iko wazi, hii ni mifano ya vitabu, vitabu vimeandikwa kimaajabuajabu. Mfano mmoja ambao umetolewa asubuhi na mtoe hoja, watu waliohusika na utayarishaji wa vitabu wanatajwa, majina yao yapo hapa kwenye kitabu na haohao tena ndio wanakuwa kuwa ni warekebishi haji wa kitabu, wapi na wapi! Kwa mfano kuna mtu mmoja ambaye alihusika katika utayarishaji F.D. Sichizya na W.T Kwarazi, haohao wametajwa tena katika suala la kurekebisha kitabu. Narejea tena, *a person cannot be a judge in his own cause or in his own case*, huwezi ukawa ni hakimu wa kesi yako wewe mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, hivi vitabu, Waziri bila shaka mimi naamini alikuwa ameshaviona au hajaviona? Sasa kama hajaviona sijui anafanyaje kazi wakati mwingine, au washauri wake siyo wazuri, hawamwelezi nini kifanyike. Lakini suala hili kuna watu wamepata kuiandikia Wizara lakini Wizara bado haijaweza kuchukua hatua juu ya matatizo haya, leo wanaomba tena waweze kupewa dhamana waende wakafanye haya ambayo wanataka kufanya, mnaamini itaweza kusaidia.

Mheshimiwa Spika, shida moja ambayo naiona, walizungumza hapa wachangiaji asubuhi, kazi kubwa ya Bunge kama ilivyo kwenye Ibara ya 63 ni kuishauri na kuismamia Serikali. Hoja iliyokuwa mbele yetu ni kwamba mtoe hoja aliomba iundwe Kamati Teule lakini nasikitika sana kuona baadhi ya Wabunge wanaona hatari kwa hii haki ya Bunge ya kwenda kuchunguza, kuna tatizo wapi? Maana zimeibuka hapa mada kwamba hii hoja haiko-specific, *of course* ni haki ya kila binadamu kuwa na mtazamo wake lakini ukija kuniuliza mimi nitakuambia kwamba hoja hii ni specific. Kwanza hata ukiangalia kwa mujibu wa Kanuni zetu inaeleza kwamba ipo bayana, hakuna hoja ambayo itapelekwa ndani ya Bunge ambayo siyo mahsus, imepitia kwa watu ambao ndio mnawaita ni wataalam. Maana yake mmetuvua wengine na taaluma zetu kwamba siyo wataalam, wataalam ni wale ambao wapo ndani ya Executive! Huu ni mtazamo ambao kwa kweli unapaswa kipingwa vikali.

Mheshimiwa Spika, ninasikitika na kuwa na wasiwasi wakati mwingine na baadhi ya Wabunge ambao wanadiriki kusema tuwaachie wataalam, hivi humu ndani sisi hatukusoma? Hamkusoma? Mpo Ma-profesa humu ndani, wapo watu wana Shahada zao, wapo watu wana Diploma zao, inapokuja suala la kusema kwamba tuwaachie wataalam kana kwamba Bunge zima hili ni la watu labda ni Darasa la Saba peke yao, sijui ni Darasa la Nane peke yao, sijui ni Form Four peke yao! Nashindwa kuelewa watu ambao wanakuwa na mtazamo wa namna hii, kwamba tuwaachie wataalam.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuweza kufanya *reflection* kwenye namna ambavyo tumekuwa tunayatazama masuala haya. Kwa mfano, ukijaribu kupitia kwenye taarifa ambayo imewasilishwa na Waziri wa Elimu juu ya suala la kufanya *intergration* katika somo la Fizikia pamoja na Kemia, amesema hayakuwa mabadiliko ya mitaala, ni kweli ukiniuliza mtu kama mimi ambaye ni *profession* kwenye sekta hii ya elimu, naomba ku-declare kwamba nilisoma Grade A, nikafanya *First degree* katika *field* ya elimu na nikafanya Shahada ya Uzamili katika masuala ya elimu. Kwa hiyo, unapozungumzia kuhusiana na *curriculum* na mchakato mzima wa kufuata katika kufanya kitu kinachoitwa *curriculum*, ninaelewa ni kitu gani na ni ninaelewa ni *procedure* gani ambazo zinapaswa zifuatwe. Sasa ipo dosari hapa moja ambayo inajitokeza, wamefanya *intergration* mwenyewe Waziri ameleeza kwamba wali-intergrate lakini hayakuwa mabadiliko ya mitaala. Kwa kuwa mlifanya hivyo na hamkufanya mabadiliko ya mitaala, mlikiuka *principle* namba tatu katika ukuzaji wa mitaala, kwa sababu zinakwenda kwa *series*!

Mheshimiwa Spika, *principle* namba tatu katika *process* ya ukuzaji wa mitaala inatuambia kwamba ni *selection of content to be taught*. Kwa vyovyyote vile ukijaribu kuangalia hata wakati wameamua kuweza kuyaunganisha yale masomo ya Historia, Jiografia pamoja na Uraia, kuna vitu walivipunguza. *I have been teaching for almost more than seven years*, huwezi ukaniambia kwamba ile *content* iliyokuwa ya Historia, Jiografia pamoja na Uraia kwamba ndiyo *package* au dozi ambayo walikuwa wanapewa vijana wa shule za msingi kule, kuna vitu vingi walivipunguza na kuwafanya vijana au wadogo zetu ambao wamekuwa wakisoma kule kukosa ile dozi kama ambayo mliipata ninyi wazee wetu na ambayo baadhi tulipata sisi. Ni wazi kukiukwa kwa hii *principle* namba tatu, ni moja ya kitu ambacho kwa kweli Serikali inanifanya sina imani kwamba ninyi mtaweza kwenda kufanya kazi na kuweza kudhibiti huu uharibifu na uchakachuaji wa rasilimali kama vitabu ambao umefanywa na kuweza kudhibiriwa waziwazi.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa Serikali iepuke suala la kupora mamlaka ya Bunge lako, huko tunakokwenda inaonekana Bunge linapoteza mwelekeo. Suala la kuundwa kwa Kamati, ni suala ambalo ni *common* na ni wajibu wa Bunge. Sasa inanitia mashaka kwamba hawataki Kamati Teule ikaundwa, tukaweza kwenda kuona ujisadi mkubwa umejificha mahali gani.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba Waziri wewe ni Mbunge mwenzetu na Naibu Waziri, hebu acheni Kamati Teule ya Bunge iundwe, twende tuisaidie Serikali, hii Serikali siyo ya kwenu ninyi tu, Serikali ni ya kwetu, leo mnawenza kuona kwamba, maana yake hapa kuna mambo ya itikadi za vyama, kuna U-CCM, U-CHADEMA, U-NCCR, U-CUF. Hivi vyama nawaambia ndugu zangu haviwezi vikatusaidia na haipaswi kuwa ndiyo *first priority* kwetu. Ni lazima tuangalie kwanza maslahi ya Taifa, maslahi ya nchi yetu katika kufanya maamuzi kwenye masuala mbalimbali. Lakini hapa kinachoonekana kuna watu wa Wizara ya Elimu mnawaficha na Waziri wa Elimu kwa kweli / *I am sorry* kukuambia kwamba pengine ninakosa imani na mtazamo wa kusema kwamba Kamati Teule isiundwe kuweza kuja kulichunguza suala hili, ni dhahiri kwamba inawezekana kuna watu wengine mnataka kuwalinda huko ambao wamepelekea leo hii vinakuja kuandaliwa vitabu na kupitishwa vitabu ambavyo ni vya oyoovyo. Hivi vitabu naomba niseme tu kwamba ni vitabu vya oyoovyo kweli, hata ukijaribu kuangalia ile *Education and Training Policy* ya 1995, kwa mimi binafsi imepitwa na wakati. Yapo mambo ambayo tunahitaji kufanya mabadiliko kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaweza tukawa na aina ya mfumo wa elimu na elimu ambayo inaendana na wakati.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi tu ndugu zangu ambayo ni *factors muhimu* ambazo tunapaswa kuweza kuzizingatia katika kufanya *curriculum change au curriculum development*, mifumo ya kisasa inabadilika, zipo teknolojia mbalimbali ambazo sasa hivi zimegunduliwa hata ukija kuangalia mfumo ambao tunakwenda nao sasa hivi tume-base kwenye *centralized pattern curriculum design*, katika nchi yetu, haitusaidii, hii nchi ni kubwa. Nchi za wenzetu kama Marekani, Uingereza, Japan, Australia na kwingineko wameamua kufanya kitu kinachoitwa *decentralization of so called curriculum pattern design* ili kusudi watu ambao wapo kule chini waweze kuangalia kwamba ni jinsi gani...

(*Hapa kengele illilia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji*)

SPIKA: Haya ahsante, kengele ya pili.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, ungeniongezea muda kidogo. (*Kicheko*)

SPIKA: Hamna. (*Kicheko*)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika nashukuru, siungi mkono hoja ya Waziri. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba wanaokuja wajadili hoja. Sasa nitamwita Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, atafuatiwa na Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami naomba niungane na Wabunge waliotangulia kuweza kumpongeza Mheshimiwa Mbatia vilevile na kuipongeza Serikali kwa mambo ambayo imeweza kuyawasilisha ndani ya hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, naomba kwanza ni-*declare interest* kwamba mimi ni mchapishaji wa vitabu lakini ni vitabu bora ambayo vimesaidia sana kuinua elimu hapa Tanzania, wengi wamevisoma, Mheshimiwa Machali amevisoma, Mheshimiwa Mkosamali na wengi tu wamevisoma vitabu vyangu. Kwa hiyo, ukweli ni kwamba ndio vimewafikisha hapa walipo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile ni-*declare interest* kwamba kwa mwaka 2009 katika hii tenda na mimi nilijaribu ku-*tender* nilipata somo la Kemia kwa Kidato cha Kwanza na cha Pili. Nafikiri hata Mheshimiwa Mbatia kama amepitia hiyo tenda atakuta kwamba vitabu vyangu havikuwa na matatizo, viliidhinishwa na Wizara ya Elimu na vilikuwa vitabu safi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba nijikite katika hoja moja kwa moja. Kuna mambo ya msingi ambayo Wabunge na ambayo Taifa kama Taifa lifahamu kwamba mitaala kubadilika katika nchi yoyote ile ambayo inapiga hatua kimaendeleo, nchi yoyote ile ambayo imejipanga kuendela hatuna budi kukubali mabadiliko ya mitaala ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo makubwa manne ambayo yanababisha mitaala katika nchi yoyote ile ibadilike. Kwanza, ni mapito ya kihistoria mfano nchi kutoka katika ukoloni na kupata uhuru, ni lazima mtaala uweze kubadilika. Jambo la pili, ni Sera ya Elimu kubadilika kwa mfano Sera ya Elimu ambayo Mheshimiwa Mbatia sasa hivi anasema kwamba imechukua muda mrefu. Kwa hiyo, ni lazima tunapobadilisha Sera ya Elimu, ni lazima tubadilishe na mitaala ili kuendana na mazingira ambayo hiyo Sera ya Elimu inataka. Kingine ni maendeleo ya sayansi na teknolojia mfano sasa hivi kuna somo la TEHAMA, hili limekuja kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia ambayo inabidi watu watumie kompyuta na vitu vinginevyo. Haya yote yanababisha mitaala ibadilike na kingine ni mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni kwa mfano, utawala mmoja unaweza ukapita, utawala utakaofuata unaweza kuleta mawazo mengine ambayo yanaweza yakatumika, lakini hayo yote mambo manne yanatumika kufanya mitaala ibadilike katika nchi yoyote ile ambayo inapiga hatua ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sera ya Elimu ya mwaka 2010, mimi nimeisoma, naomba ni-*declare interest* kwamba nimeisoma na nimeshiriki kama mdau na ina mambo mengi mazuri ambayo hata leo asubuhi tulipokuwa na Mheshimiwa Mbatia nilimwambia kabisa kwamba aende aisome hii Sera ya Elimu ya mwaka 2010. Hii Sera kama itaharakishwa ikaja huku Bungeni, maana nasikia ilikuja huku Bungeni, Wabunge wengi waliegemea kuangalia umri kwamba eti umri wa kwenda shule za msingi iwe ni miaka sita badala ya miaka saba wakawa wanapinga lakini hawakusoma maudhui ya ile Sera. Ile Sera ina vitu vingi sana kwa mfano Sera ile inatamka mambo yafuatayo: inasema kwamba itaangalia ubora wa elimu, itaangalia lugha zitakazotumika kufundishia na inatamka kwamba ni Kiswahili na Kiingereza na mwisho inasema umuhimu wa kufundisha somo la uzalendo ambalo Mheshimiwa Mbatia amesema hayo. Katika

hayo, Sera inasema kwamba mtoto atafundishwa, Mtanzania ni nani, haki za Mtanzania, wajibu wa Mtanzania katika nchi yake, Mtanzania na watu wengine wa mataifa mengine, utamaduni wa asili wa Mtanzania na maadili ya Mtanzania ni yapi, haya yote hiyo Sera imeyaongelea. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijitahidi kufanya kila linalowezekana ilete ile Sera tuisome, tukishaisoma na sisi Wabunge tuchangie kama wadau na Serikali ipitishe. Ile Sera itatua matatizo mengi ambayo yapo katika mfumo wa elimu katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile niseme kwamba, hawa Mawaziri wa Elimu tunawaonea. Mfumo wa elimu katika nchi ya Tanzania uliharibika kuanzia mwaka 2005, wao hawakuwa Mawaziri. Mwaka 2005 wakati ambapo baadhi ya masomo yaliunganishwa na baadhi ya masomo katika shule za msingi yakaongezeka. Badala ya mwanafunzi wa darasa la kwanza na la pili kusoma mambo matatu, Kusoma, Kuandika na Kuhesabu, wakaingiza masomo mengine mengi. Nasema kwamba, hii Sera ya Elimu itamke hadharani kabisa kwamba, mwanafunzi katika elimu ya awali asome masomo matatu, ambayo katika dunia nzima ndivyo wanavyofanya, wanasoma Kuandika, Kuhesabu na Kusoma. Kuanzia darasa la tatu na kuendelea ndio masomo mengine yaje, kama somo la uzalendo, masomo ya siasa na masomo mengine ambayo yatajitekeza. Lakini mwisho wa yote ni kwamba, hawa Mawaziri wamejitalidi kwa sababu, wameona kwamba, mfumo wa elimu katika nchi yetu una matatizo ndio maana waliamua kwa dhati kuleta hii Sera ya Elimu, lakini tunataka wajitalidi kuileta mapema hii Sera, iweze kutumika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kingine kuna mambo mawili ambayo tunayachanganya katika elimu. Mitaala ndio inayotoa Mihtasari na hiyo Mihtasari ndio inayosambazwa katika shule, Walimu wanatumia ile Mihtasari kufundishia. Mitaala inaandaliwa na Taasisi ya Kukuza Mitaala, Taasisi ya Elimu, tunayo! Sasa mimi ninashangaa Mbunge mwenzangu Mbatia kusema kwamba hatuna Mitaala; hiyo Mitaala hata kama ipo na inaandaliwa, Mitaala ndio inayotoa dira. Tuseme Mitaala ndio inayoongoza ni nini Mwalimu afundishe na hiyo Mitaala ndio inayotoa Muhtasari amba unaweza kutumika. Hiyo Mitaala ndiyo inayotuongoza sisi waandika vitabu. Kwa hiyo, naomba kabisa kusema kwamba hayo ni mambo ya kushauriana, kujadiliana kwamba tunapotoa Mitaala ni vizuri tukapeleka kwa wadau mbalimbali, lakini hawa wadau ni kweli wanaipitia au wanaiangalia? Au ni Mwalimu anang'ang'ana na ule Muhtasari tu? Haya ni mambo ambayo kwa kweli inabidi tutoe somo kwa Watanzania waweze kuelewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, tunaomba Sera ya Elimu itamke ni lugha gani ya kufundishia? Hili ni tatizo kubwa sana ambalo linatukabili katika nchi yetu ya Tanzania. Mtoto anaanza kujifunza Kiswahili, akifika Sekondari anaanza kujifunza Kiingereza, inakuwa ni tatizo. Kama tunaamua kwamba, tunatumia Kiingereza, tutumie Kingereza; kama tunaamua kwamba, tutumie Kiswahili, tutuimie Kiswahili, lakini hatuwezi kuepuka Kiingereza. Mimi ninawataka Watanzania kokote kule walipo wajifunze lugha nydingi za kigeni, kiwe Kiingereza, kiwe Kifaransa au hata kiwe Kichina, hii itatusaidia kuwasiliana na watu wa Mataifa mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kazi ya Taasisi ya Elimu, ambayo imepewa jukumu la kukuza Mitaala hapa nchini. Naamini kabisa kwamba, kwa Waziri aliyejukupo kwenye dhamana ya elimu mwaka 2005, aliipokonya madaraka ile Taasisi akachukua vile vitabu vya Taasisi ya Elimu, akawapatia wachapishaji mbalimbali na wale wachapishaji ndio wametufikisha hapa tulipo. Sasa tunaomba kabisa kwamba, Sera itamke hadharani kazi zote za vitabu vya Ziada tuendelee kuandika ili watu waweze kujisomea, msije mkatunyima kula na wengine, lakini vitabu vya Kiada, Taasisi ya Elimu ndiyo iandike na huko Taasisi ya Elimu, wachaguliwe watu makini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama sasa hivi mimi kwa kweli ninasema kabisa hadharani kwamba, tumepata Kamishna wa Elimu, Profesa Mwalusesa, yule mama ni mzuri; tumpe ushirikiano,

naamini ataleta mabadiliko katika mfumo wa elimu katika nchi yetu ya Tanzania. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, mimi ninaamini kabisa kwamba, mkifanya mabadiliko na mkaipitia ile Taasisi ya Elimu nguvu, wakafahamu majukumu yao na wakatekeleza, badala ya kujandikia vitabu kama ambavyo Mheshimiwa Mbatia amevileta hapa na wale ambao wamehusika wakachukuliwa hatua kwa sababu, kama wengine hawapo, wengine wamestaafu nawafahamu lakini wengine wapo kule, hawa watu wote kama wameshindwa kuonesha uzalendo muwachukulie hatua. Mambo yote ambayo tunayalamikia kuhusu hivi vitabu hayatakuwepo tena. Lakini cha msingi kabisa, tuseme hadharani, Taasisi ya Elimu ipewe jukumu la kuandaa vitabu vyaa shule za msingi, vitabu vyaa Kiada. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninataka nilisemee ni kwamba, kwa sababu, sasa hivi tunataka kubadilisha Sera ya Elimu, ina maana kabisa kwamba, kama Sera itabadiili na Mtaala utabadiili na vitabu vitabadiili. Sasa kwa sababu, tulikuwa na hela za rada, zile hela badala ya kununua vitabu ambavyo sasa hivi tukibadilisha Sera na baadaye tutahitaji kuandika vitabu vingine vipyaa, tuangalie namna gani hiyo hela itumike kuandika vitabu ambavyo vitatumika katika muhtasari mpya, kupanga ni kuchagua. Hapo tutakuwa tumewapunguzia hata wazazi wetu hela za kununua vitabu kwa sababu, Taasisi itaandika vitabu, wapo wataalam mbalimbali, mnaweza mkaniambia hata mimi mwenyewe nikawapatia wataalam; kwa mfano Idara ya Elimu ya Watu Wazima, huwa ninawapatia wataalam wanawaandikia vitabu pale. Wananiomba, mimi nawapa wataalam wa Elimu ya Watu Wazima. Kwa hiyo, tuna wataalam ambao wamesoma na wamebobeaa na wanaandika vitabu ambavyo kwa kweli, vinatumika na vimebadilisha kiwango cha elimu katika nchi ya Tanzania. Kwa hiyo, mimi ninafikiri kabisa kwamba, hili jambo lote tulichukulie katika mjadala mpana, ili tuweze kuangalia ni namna gani tutaweza kutoa vitabu bora na si bora vitabu katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hili la mwisho, mimi ninasisitiza kwamba, Kitengo cha Ukaruzi katika shule za msingi na shule za sekondari, ni muhimu sana. Kwa sababu, mwaka 2005, Wizara ilibadilisha Mitaala ika-base katika *competent syllabus*, yaani Umilisi, bila kuwashirikisha wadau na baadhi ya Walimu wanashindwa kufundisha ile Mitaala. Hata baadhi ya Waandishi wanashindwa kuandika vitabu vinavyokidhi ule Mtaala ambao ulibadilika mwaka 2005 na halikadhalika tumefika mpaka hata Vyuo Vikuu hilo tatizo bado lipo. Hata juzi tulikuwa tunaongea na Walimu wa Chuo Kikuu cha Muhimbili, wakasema kabisa kwamba, wataalam wanakimbia kazi kwa sababu Mtaala ulipobadilika wameshindwa kuufundishia. Kwa hiyo, hilo ni tatizo kutoka elimu ya msingi, elimu ya sekondari mpaka vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, kama Taifa tuangalie, tunapobadilisha Mitaala tuwashirikishe na wadau wale, ili tusipate matatizo ya watoto wetu kufeli mitihani na mambo mengineyo. Tukiyafanya hayo na kwa pamoja tukadhamiria na tukazingatia maagizo ya Serikali na Serikali yetu ikaleta maagizo kama tunavyoishauri, mimi ninaamini kabisa kwamba, kiwango cha elimu katika nchi yetu ya Tanzania kitakuwa cha juu sana. Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki elimu ya Tanzania. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii muhimu iliyopo mbele yetu hapa.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nianze kwa kumnuuu Waziri Mkuu wa kwanza wa Tanganyika na Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kitabu chake alichokiandika mwaka 1965, kinachoitwa "Tujisahihishe" na kilirudiwa tena mwaka 1980. Anasema hivi, naomba ninukuu zile sehemu ambazo ninataka nizitumie, anasema:-

"Nitajielimisha kwa kadiri ya uwezo wangu wote na kutumia elimu yangu kwa faida ya wote."

Mheshimiwa Spika, lakini nukuu nydingine alisema hivi:-

"Watu walio hatari sana ni wale ambao wanafikiri kuwa wanajua kila kitu wala hawana haja ya kujifunza zaidi. Hii ni tabia mbaya ambayo huweza kuzuia kabisa maendeleo."

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema hivi, rafiki yangu, kaka yangu na Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Mbatia, alinukuu maneno ya Mwalimu Nyerere, aliyoyasema mwaka 1958, binafsi nakupongeza sana. Nakupongeza sana kwa maana kwamba, umeweza kufanya utafiti na umetumia vema kabisa elimu yako kwa manufaa ya nchi yetu na uzalendo wa nchi yetu, ninakupongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna gazeti moja sijui linamiliikiwa na nani, linaitwa "Habari Leo". Mara nydingi huwa linatoa nukuu, lakini katika toleo lake la leo limesema hivi:-

"Jamii isiyozingatia na kutafsiri mambo haiwezi kuelewa na huenda ikashindwa kujitambua siku zijazo."

Mheshimiwa Spika, maana ya kusema hili, mimi ninastaajabu Wabunge ambao ndio wenye jukumu la kuismamia Serikali, ndio wenye jukumu la kuwawakilisha wananchi, tunakuja kujadili mambo ya msingi kabisa katika mustakabali wa nchi yetu kwenye sekta ya elimu, tunaleta ushabiki wa kupinga hoja, tunakwenda wapi? Matatizo haya yaliyoainishwa humu, yote yanajibiwa na Sera ambayo Serikali imekubali kuileta. Mto Hoja Mwenyewe amenukuu Hansard ya Bunge ililopita kwamba, Serikali, iliahidi italeta katika Bunge hili Mitaala na Sera ambayo imeshatungwa, ili Wabunge muweze kuchangia, Bunge hili halijakwisha. Sasa mbona hatujulizi kwamba, jamani ile mliyoahidi kuleta hebu ileteni kwanza tuweze kuwakosoa. Mletaji Hoja, Mheshimiwa Mbatia, alisema hivi katika kitabu ambacho kimeandikwa humu, ukurasa wa 9 na ukurasa wa 10, anasema:-

"Pamoja na kutambua kazi kubwa ambayo Serikali, kupitia Wizara yake yenyenye dhamana ya Elimu, ilifanikiwa kuifanya... ",

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba, anatambua Serikali, inafanya mambo, ninyi mnataka nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ye ye mwenyewe anakiri kutambua jitihada za Serikali, ninyi mnakataa mnasema kwamba, hivyo sivyo alivyokusudia. Mbona mnatia maneno ya mtu kwenye vinywa vyenu mnayatamka ninyi? Hayo sio aliyomaanisha. Hebu fikirieni vizuri maana ninaamini kabisa Mungu amewapa uwezo wa kujua zaidi ya hivyo ambavyo mnafanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi niseme tu kwamba, matatizo ya elimu, Sera ya Elimu, tunaelewa kwa maana kwamba, hakuna dhununi la elimu kwa mwanadamu, elimu ya aina yoyote, elimu ni kitu ambacho mtu kitamsaidia kupambana na mazingira aliyonayo, sio vinginevyo. Sasa ni lazima mazingira yanavyobadilika na elimu itabadilika. Tuwape nafasi, tujisahihishe, tuweke sawa Mitaala yetu, ili iweze kuwiana na muda na wakati tulionao hivi sasa, nalo pia hamtaki. Maana mtu kuwa mpinzani, kuna mtu mmoja rafiki yangu sana, Mbunge hapa, anasema sisi Wapinzani. Kuna siku nikamuuliza hivi wewe umezaliwa mahali fulani? Akasema hapana, lakini baadaye akaniambia kweli, kwamba, ye ye anapinga tu kitu chochote kile. (*Makof*)

SPIKA: Naomba ujadili Hoja sasa. Jadili Hoja sasa. (*Kicheko*)

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, naomba tu kusema kwamba, pamoja na kukubaliana na maelezo ya Serikali, kwamba wataleta Sera, Wabunge wote waweze kushiriki kuchambua na kuweka sawa matatizo yote ambayo yameainishwa kama alivyowasilisha Mheshimiwa Mbatia na kama walivyowasilisha Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameshachangia, yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi ninaomba Waziri wa Elimu, ninaamini kabisa ananisikia na Naibu wake, matatizo ambayo sasa hivi Walimu na Wanafunzi wanakabiliana nayo katika shule, hatuwezi kusubiri mpaka pale ambapo Sera itakamilika. Yafanyiwe kazi kwa haraka, yapatiwe ufumbuzi wa haraka, ili tuweze kukabiliana na hali iliyokuwepo sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nyangwine na Mheshimiwa Marombwa, wote ni Walimu hao, asubuhi hapa walizungumzia Idara ya Ukaguzi katika elimu ya msingi na sekondari ina matatizo, ifanyiwe kazi haraka, matatizo haya yaweze kuondoka.

Mheshimiwa Spika, kuna marupurupu, kuna malimbikizo ya mishahara na matatizo ambayo Walimu wanakabiliana nayo, tuyafanyie kazi haraka, ili waweze kuchangia kutoa elimu kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize kwa kusema tu kwamba, Mungu Ibariki Tanzania na Mungu atusaidie na kutuongoza katika njia iliyo nyooofu. (*Makofii*)

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii na mimi kuchangia Hoja hii. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbatia kwa kuleta Hoja hii. Nikiangalia dhamira ndani ya Wabunge wote, hasa wa CCM, hoja hii ni nzuri kwa maana kwamba, yale ambayo asubuhi tulikataa, lakini ukiangalia kwa nje wote wanakubali.

Mheshimiwa Spika, sasa ninataka kusema mambo makuu kama matatu. Jambo la kwanza, linahusu Sera ya Elimu. Sera ya Taifa kuhusu Elimu.

(*Hapa kengele illilia*)

SPIKA: Sio kengele yako, hapana. Sio yako hiyo.

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Udhafu mkubwa umejidhihirisha kwamba, Sera ya Taifa ya Elimu kwa Tanzania, ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema hivi, wamesema kwamba, hatuwezi kuwa *static* ni sawa, lazima tubadilike. Ni miaka 50 sasa tangu ukoloni, ninajuliza, je, hii elimu ya Tanzania imemkomboa Mtanzania kwa kiasi gani ili aweze kupambana na maisha yake? *You can be educated but not liberated!* Sasa, kama ndivyo hivyo, mpaka leo Serikali imeahidi mara nyingi italeta Sera, italeta Sera, hatuoni.

Mheshimiwa Spika, kutoka Sera yenyewe ndipo tunapokuja kwenye kitu tunachoita *Curriculum*. Kutoka *Curriculum*, tutakuja kwenye *Syllabus* na kutoka *Syllabus* tutakwenda sasa kujua kwamba kila Mwalimu anafanya kazi hiyo. Niseme mimi ni Mwalimu pia, ukitoka *Syllabus* ni lazima utengeneze *Lesson Plan*, utengeneze *Lesson Notes*, ukafundishe, kabla ya *Scheme of Work* ambayo inakuongoza halafu uje *Lesson Plan*, *Lesson Notes*. Katika mambo yote haya, nataka kuunganisha hivi, ili kufanikiwa kumkomboa huyu Mtanzania kielimu ni lazima huyu Mwalimu atunzike sawasawa na Sera ni lazima ieleze wazi, Mwalimu atunzike sawasawa.

Mheshimiwa Spika, sisi Wafugaji tunatabia hii, ukitaka kupata maziwa sawasawa ni lazima umtunze yule ng'ombe vizuri. Ukimkuta ng'ombe jeuri kama anapiga mateke, unamwimbia na wimbo, ili wewe kwa dakika zile chache uweze kukamua maziwa haraka. Sasa Mheshimiwa Mbatia, ametufungua macho vizuri katika Hoja hizi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli, tulipoanza baada ya uhuru kulikuwa na shinikizo kubwa kutoka *World Bank, IMF*, kwamba, wanatuelekeza elimu iweje kwa sababu wao wana-sponsor. Tufike mahali sasa, Tanzania miaka 52 *plus*, elimu imkomboe Mtanzania. Kinyume cha elimu kutomkombo Mtanzania, nalinganisha sisi Wafugaji pia, tuna majosho, wale Wataalam wazee wa kilimo, yale majosho yanaangaliwa na wale *Veterinaries* wanaweka dawa, ng'ombe wanapita kule. Yule *veterinary* asipokuwa mwaminifu, ataweka dawa pembeni, ng'ombe watapita tu kwenye maji, kupe hawataondoka. Tunazo shule, wanafunzi wanahitim, wahitim wetu hawawezi kabisa kupambana na mazingira yao, ndio aina ya elimu tuliyonayo. Sasa tubadilike baada ya miaka 52 *plus*.

Mheshimiwa Spika, katika Hoja hii iliyotolewa, tuna mambo ambayo kimsingi Serikali lazima ikubali kufanyiwa kazi. Moja, tunalia juu ya ajira, hatuna ajira. Mimi ninashangaa sana tumepewa msaada wa fedha tungepaswa kufanya huduma ile hapahapa nchini, viwanda nya kuchapa tunavyo, kazi ile ingefanyika hapa nchini siyo Malaysia wala siyo Kenya, tungepata ajira. Kwa wale wafugaji, mahali unapochinjia ng'ombe wale walioko *around* pale wananaufaika zaidi.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona kwamba tunapeleka Malaysia, tunatoa ajira tunapeleka Kenya huku Tanzania sisi tunalia kila siku halafu tukisema hapa kuna harufu ya ufisadi Serikali inasema aaah tusiunde Tume. Kwa hiyo, ninaomba, wamesema wazungumzaji wengi kwamba Serikali haiwezi kujihukumu, haiwezi kujikosoa bado ni muhimu tukitaka kuwa na elimu itakayomkombo Mtanzania tuwe makini kidogo.

Mheshimiwa Spika, suala la Walimu, ni muhimu sana Serikali ikatazama maslahi ya Walimu ili elimu hii iwe bora. Walimu watakwenda tu, atakwenda shulenii atakaa masaa yataisha atachukua mshahara wake mwisho wa mwezi lakini watoto wetu wanapata shida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimalize kwa kusema hivi, Kitengo cha Ulaguzi wa Elimu kama kitaendelea kukaa chini ya Wizara maana yake hawawezi kukagua na kufanya kazi sawasawa. Kule kwenye Halmashauri zetu hata wale Wakaguzi wa Elimu kwa sababu wako chini ya Afisa Elimu, hawawezi kumkosoa bosi wao. Kwa hiyo, ni vizuri kitengo hiki kikakaa sawasawa na kiwe *well trained* katika kuhakikisha kwamba wanakagua shule na hii ndiyo inazaa vitabu vingi vinafurika bila hata sababu.

Mheshimiwa Spika, mimi nilisoma Fizikia na Kemia na Mtaala wake, *Syllabus* na kila kitu vilikuwa vinajitegemea. *Physics* peke yake, Kemia peke yake, Serikali inafanya majoribio wakaunganisha na hatimaye ilipoonekana haiwezekani wakafumua, wakarudisha ijitegemee. Maana yake hatuna dira, hatuna mwelekeo. Mbovu kuliko yote, pamoja na kwamba Mtaala lazima ibadilike *from time to time* lakini lazima kujiliza kama Serikali, kama Taifa tunaelekea wapi, Sera inasema nini siyo matakwa ya mtu mmoja, Waziri mmoja amekuja aka-*influence* mambo yake tunakwenda kule aaah, hatuendi namna hii na ndiyo maana tumeyumba sana kwa elimu yetu Tanzania, tumeyumba sana kila mmoja anajua na kila mmoja anakiri ni bora elimu na siyo elimu bora. Kwa hiyo, tufike mahali Serikali tuone Taifa linatoa elimu bora kwa watu wake.

Mheshimiwa Spika, imenisikitisha sana, nimalize kwa kusema Waheshimiwa Wabunge wenzangu wachache tena wengine marafiki zangu, kusema kwamba sisi tuwaacie wataalam, tusihangaike na hivi, aaah, hapa ni kujifunga yaani unafikiri usawa mfupi sana. Naomba tupanuke, tufikiri zaidi ya urefu. Kwa hiyo, niombe hivi, wataalam wako hapa, Sera iletwe hapa kama ulivyoahidi, Bunge hili lina haki ya kusimamia Serikali na kuishauri msiilogope Serikali, ndiyo haki ya Bunge tuisimamie na tuishauri vinginevyo hatuna sababu ya kukaa huku na wataalam wapo, Wabunge ni wataalam ma-engineer, walimu kila fani ipo hapa, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Abdul Marombwa atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Mwijage.

MHE. ABDUL A. MAROMBWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi ili kuweza kuchangia hoja ilivoletwa na Mheshimiwa James Mbatia.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi niseme nikiwa kama Mwalimu, ni hoja nzuri ambayo kwa kiasi kikubwa Serikali inatakiwa iangalie kwa makini na hatimaye Serikali iweze kuyatekeleza yale ambayo yameelekezwa katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu, mimi nianzie na alipoishia Mwalimu mwenzangu, yeye alisema kwamba Sera hii haijamkomboa Mtanzania au kwa miaka hamsini imemkomboa Mtanzania kwa kiasi gani. Sera ya Elimu kwa kiasi kikubwa imewakomboa Watanzania na uwepo wetu sisi hapa Bungeni inatokana na hizo Sera nzuri za Elimu. Amani tuliyokuwa nayo katika nchi yetu, hii inatokana na Sera hiyo ya Elimu na vitu ambavyo tunaviona sasa hivi vinaendelea Sera ya Elimu ndiyo imeweka na kutufikisha hapa tulipo, lakini sera hii inahitaji kuboreshwa, hilo mimi silipingi, lakini ukisema Sera ya Elimu haijamkomboa Mtanzania kwa miaka hamsini, siungi mkono, Sera imetukomboa sana hadi sisi kuwepo hapa inatokana na Sera hiyo.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka kulizungumzia, alizungumza pia Mheshimiwa Mbunge aliyemalizia kwamba Kitengo cha Ukaguzi kipo Idara ya Elimu, Kitengo cha Ukaguzi ni *independent*, hakipo kwenye Idara ya Elimu. Katika Wilaya kinajitegemea chenyewe, kinasimamiwa na Wizara ya Elimu, ni *independent* na kuwako kwake *independent* Kitengo hiki ndiyo inayosababisha kisiweze kupata huduma yoyote katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapendekezo ya kutaka tuwe na Wakala wa Elimu, ni nzuri sana lakini wakati Wakala wa Elimu bado hajapatikana, mimi nilikuwa naishauri, ni vizuri sasa Wizara ikakaa na kuangalia kwa makini, tumepiga makelele sana kwamba elimu yetu haiwezi kuwa nzuri kama hakuna watu wanai-monitor hiyo elimu kwamba huyu Mwalimu anafanya nini. Mheshimiwa Mwalimu Margaret Sitta amezungumza, hapa Dar es Salaam Wakaguzi zaidi ya 20 wamekagua shule nane, mimi pale kwangu Rufiji nina Wakaguzi sita na wote ni *graduates* wamemaliza Chuo Kikuu, kwa mwaka mzima wamekagua shule nne tu na kati ya shule hizo nne walizozikagua siyo zote ambazo taarifa zake zimepatikana kwa sababu kwa mwaka mzima Idara nzima ya Ukaguzi wamepewa shilingi laki mbili tu, sasa shilingi laki mbili zitafanya kazi gani?

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali ijitahidi kuhakikisha kuwa Kitengo hiki cha Ukaguzi kirudishwe kutoka kwenye Wizara kiweze kuwa kwenye Halmashauri ili Mkurugenzi atakapokuwa anapanga mipango yake ya maendeleo kupitia *own source* ile inayopatikana na Kitengo hiki kiwepo lakini sasa hivi Wakurugenzi wengi hawataki kuingiza Kitengo hiki kwa sababu wanasema kinahudumiwa na Wizara, magari yapo, Wakaguzi wapo, tena magari wanayo, siyo kwamba hawana Wakaguzi, wapo lakini namna ya kuyahudumia magari hayo, namna ya kuweza kufanya kazi zao, hakuna kinachofanyika katika hizi Wilaya zetu. Sasa

nilikuwa naomba sana Kitengo hiki kabla ya kuwa Wakala ni vizuri Serikali ione kwamba Wizara imeshindwa kukihudumia Kitengo hiki, sasa ikirudishe kwenye Halmashauri ili nacho kiweze kupata ruzuku ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa na wenzangu lakini mimi nizungumzie suala lingine la Taasisi ya Ukuzaaji Mitaala (*Institute of Curriculum Development*), yenye hii ndiyo ina kazi kubwa sana. Kule nyuma ambako sisi tulikuwa tunafundisha ndiyo iliyokuwa inaandaa mihtasari na ndiyo iliyokuwa inaandaa vitabu nya Kiada lakini kwa bahati mbaya elimu tukabinafsisha hapa katikati, tukaona mtu binafsi yejote akiweza kuandika kitabu chake akapewa dhamana pale Wizarani kwenye kitengo kile cha *EMAC* basi hicho kitabu kinakuwa ni kitabu cha Kiada, pale ndipo tulipopotoka. Tumepotoka pale kwa sababu elimu sasa ikawa ni jukumu la mtu yejote akiandika na kwenda Wizara ya Elimu, Kitengo kile cha *EMAC*, unazungumza na wale wataalam wanapitisha kwamba hiki kitabu sasa kimepitishwa kama Kitabu cha Kiada, sasa hili ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ushauri wangu, pamoja na kwamba sasa hivi mmetoa vitabu viwili nya Kiada lakini bado tunasisitiza kwamba kuna umuhimu wa vitabu vyote nya Kiada kwa maana ya *text books* zote ziwe na *source* moja ambayo ni *Institute of Curriculum Development* siyo sehemu nyingine yoyote, hilo la kwanza. Vitabu vingine nya kina Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine vipelekwe kule, viwe *reference books* tu wala visiwe vitabu nya Kiada. Hapa tutaondoa mgongano wa kimaslahi unatokana na kuuza hivi vitabu Wizara ya Elimu kama vitabu nya Kiada, vyote vikitoka kwenye *Institute of Curriculum Development* basi vitabu hivi vingine vitakuwa mtu kwenda kununua ni hiari yako aidha ununue au usinunue.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo nataka kulizungumzia, kwa muda mrefu Walimu wamekuwa na malamiko mengi, ukikaa Dar es Salaam pale ukiondoa vijijini, ukikaa Dar es Salaam utashangaa Mwalimu anakaa Mbezi anafundisha Temeke wakati wote anafika shulenii kwenye saa saba, saa nane, saa tatu, saa nne, muda wa kufanya kazi ni mdogo sana. Sasa mapendekezo mengi yalitolewa kwamba Walimu ni vizuri wakajengewa shule katika maeneo yao au wakajengewa nyumba katika maeneo yao, hili litasaidia sana kuwafanya Walimu na wao waweze kutoka kwenye mazingira mafupi ili waweze kufundisha kwa muda ule ambao wao wamepangiwa, lakini hali ya sasa haipo hivyo Walimu wetu wanateseka sana.

Mheshimiwa Spika, lakini siyo kuteseka huko tu pia Walimu hawa lazima tuangalie marupurupu yao yakoje. Mwalimu yeche kama Mwalimu akiwa na wanafunzi akalipwa vizuri hata kama hana darasa, akafundisha vizuri hata kama kwenye chini ya mti wanafunzi watafaulu. Kama Mwalimu anatesekateseka hata kama utamjengea darasa zuri lakini usipomlipa vizuri basi Mwalimu huyu uwezo wake wa kufanya kazi unapungua sana. Sasa nilikuwa nafliria tena na naiomba Serikali iangalie upya maslahi ya Walimu. Je, maslahi haya ya Walimu yanalipwa au tutaboreshaje maslahi yake ili huyu Mwalimu aweze kufanya kazi zake vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na Walimu, kuna mambo mengi ambayo yamefanywa katika Mikoa yetu, kila Mkoo baada ya matokeo ya mithiani hasa ya darasa la saba kunafanyika na tathmini ya Mkoo kwamba ni mambo gani ambayo yamesababisha Mkoo wetu kuweza kufikia hapa tulipo. Jambo hili kwa muda mrefu sana linafanyika lakini linafanyika kijuujuu, hatuingii kwa ndani. Mimi nilikuwa nashauri Wizara ya Elimu nalo iliingize kwenye sera, sijui kwenye sera au kwenye mikakati yao kwamba ni vizuri sasa kila Mkoo kila mwaka wakakaa aidha siku moja au mbili kuweza kutathmini wao wenye kwenye kwamba maendeleo yetu sisi ya elimu kwa nini yamefikia hapa. Hii itatusaidia sana kuboresha elimu ndani ya Mkoo, Mkoo na wao watapeleka maoni yao kwenye Wilaya na Wilaya itakaa, kwa kiasi kikubwa elimu yetu itaboreka.

Mheshimiwa Spika, lakini nimalizie, samahani kwa kurudia nyuma kwenye Kitengo cha Ukaguzi, ukiangalia utendaji wa kazi wa Waratibu wa Elimu Kata katika Wizara yetu ya Elimu, mara nyangi utendaji wao umekuwa ni wa kisiasa. Waratibu Kata hawa wanakuwa Watendaji wa Kata, hilo tunashukuru sana limepigwa vita na kuondolewa. Sisi tunaamini kwamba Mkaguzi wa kwanza wa shule ni Mwalimu Mkuu, yeze kazi yake kukagua masomo ya Walimu shulenii kwake, je, Mwalimu fulani anafundisha au hafundishi, yeze ni Mkaguzi wa kwanza. Mkaguzi wa pili ni Mratibu Elimu Kata, je, huyu Mratibu Elimu Kata kweli anafanya kazi yake ya ukaguzi, kweli anatembelea shule yake, kweli anatoa ripoti ambayo inakwenda kwa Afisa Elimu wa Wilaya kuonyesha ni namna gani mwenendo wa maendeleo ya shule katika kata yake upo? Hawa watu wamekaa *idle*, hawana kazi yoyote wanayofanya, wengine ni wafanyabiashara jambo ambalo linapotosha kabisa na linamwondo kwenye usimamizi wa elimu, sasa anakuwa ni mtu wa kawaida tu.

Mheshimiwa Spika, lakini hapohapo kwenye Kitengo cha Ukaguzi, kwa muda mrefu Idara ya Ukaguzi ndiyo inayotoa Walimu Wakuu, ndiyo inayotoa Waratibu wa Elimu Kata, ukitaka kwenda kupata stoo ya Walimu, wapi tutawapata Walimu, unakwenda kwenye Idara ya Ukaguzi, ndiyo watakaokupatia Walimu bora kwamba tulivyokwenda kukagua kwenye shule zetu tumeona kuna Mwalimu fulani ni bora anafaa kuwa Mwalimu Mkuu, lakini kwa kuwa kitengo hiki hakihudumiwa kwa kiasi kikubwa Walimu hawa wanachaguliwa na Afisa Elimu tu wala hawachaguliwa na mtu mwingine wakati *source* yetu kubwa ni Idara ya ukaguzi, lakini sasa hivi Afisa Elimu ndiye anayechagua lakini sasa hivi Idara ya Ukaguzi haina kazi yoyote inayofanya.

Mheshimiwa Spika, hivi tunakwenda vibaya, Idara ya Elimu wao hawakagui, wanatoa nafasi hizi za uongozi kwa Walimu kutokana tu na huyu pengine ni ndugu yake, kutokana na labda pengine ni rafiki yake lakini hana sifa za kuongoza shule na ukienda kwenye shule zetu nyangi za msingi Walimu wengi Wakuu hawana sifa za kuongoza shule, hawana. Nenda kaangalie, je, huyu kweli anafaa kuwa kiongozi, sasa muangalie ni nani amemchagua huyu kuwa kiongozi?

Mheshimiwa Spika, wale wote waliochaguliwa na Idara ya Ukaguzi ni *excellent*, ni wazuri. Sasa nilikuwa naomba sana Wizara yetu hii kwa kupitia Mheshimiwa James Mbatia, ametupa changamoto nzuri, changamoto ambayo ina uwezo wa kujenga elimu katika nchi yetu, basi mimi naunga mkono hoja hii, nashukuru sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante. Nitamwita Mheshimiwa Charles Mwijage, akifuatiwa na Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa James Mbatia, kwa kuja na hoja hii muhimu na mawazo mazuri ya kizalendo aliyonayo kwa nchi yake.

Mheshimiwa Spika, nisije nikagongewa kengele, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa James Mbatia pamoja na marekebisho yaliyofanywa na Wizara ya Elimu. Kwa kuwa udhaifu wote umeshazungumzwa na kwa kuwa wananchi wanaelewa udhaifu kwa sababu wanaishi nao. Mimi nitajikita kwenye mashaka nilyonayo kwa Waziri au Wizara ambayo yenewe imebeba dhamana ya kurekebisha kile ambacho Tume ingefanya. Lengo la Watanzania ni kujenga jamii imara na ujenzi wa jamii imara unategemea elimu nzuri, kama alivyo sema rafiki yangu mmoja siku moja, alisema rasilimali yetu muhimu ni watoto wetu. Sasa ukiwa na mtoto wako ana elimu mbovu huna rasilimali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amebeba dhamana, ningependa kujua jukumu alilopewa kwa sababu kichwa cha habari kinasema nikisome tena, hoja ni kuhusu udhaifu ulioko katika sekta ya elimu. Hoja aliyopewa, jukumu analolibeba ni udhaifu katika sekta ya elimu, ina maana kazi tunayomkabidhi sasa anakwenda kuondoa udhaifu, udhaifu unamalizwa na Sera tu? Sera itaondoa tofauti ya shule kwa sababu shule za sekondari sasa ziko za Serikali, aina mbili; za kata na zile za sekondari nyingine, zote ni za Serikali na za *private*, wananchi wangependa kuona shule zote za Serikali ziwe na mtindo mmoja, hakuna cha kata, hakuna cha nini na wote wawe kama shule za Serikali za zamani.

Mheshimiwa Spika, sisi kwetu ulipokuwa ukishindwa kwenda shule ya Serikali unatangazwa Kanisani, unapoondoaa udhaifu unakwenda kuondoa udhaifu huo. Waziri ni rafiki yangu namhurumia mzigo anaoubeba. Mojawapo ya matatizo ya Walimu ni kutokana na Walimu kuwajibika kwa mabwana wengi, wanawajibika Utumishi, wanawajibika Hazina, basi wanakwenda huku kama mwanaume mwenye wake watatu unalala njaa unategemea utakula huku, utakula huku.

Je, kitendawili ambacho nimekuwa nikikisema kwamba Wizara ya Elimu ni muhimu kwa sababu Wizara ya Elimu ni muhimu kama ilivyo Jeshi la Wananchi, unakwenda kuondoa udhaifu huu kwa kuipeleka Wizara ya Elimu ijisimamie itoke TAMISEMI? Walimu wanapata shida wanapokwenda kuripoti kwa Mkurugenzi wa Wilaya wakakuta Mkurugenzi wa Wilaya ni Afisa Uvuu au ni Bwana Nyuki. (*Makof!*)

Walimu nikizungumza nao wangependa Mkoo wao awe Mwalimu kuanzia *Headteacher*, Mwalimu; Mratibu, Mwalimu; Afisa Elimu Sekondari Mwalimu na Katibu Mkoo, Mwalimu. Kweli anayeijua ile taaluma atakuthamini, unaposema kwamba unakwenda kuondoa udhaifu huu anauangalia.

Waheshimiwa Wabunge, nimebidi niyaseme haya kwa sababu tusimalize kazi hii tukarudi tena. Kweli ukitafakari mambo yote haya, unakuja kugundua kwamba kumbe Tume ingezuka isingemaliza kwa sababu suala hili ni kubwa mno. Leo asubuhi wakati naamka, Profesa wa mambo ya elimu, Bwana Katabalo alinipigia simu akasema wewe Mbunge wangu; nikasema ndiyo uwakilishi huo. Kuna biashara katika elimu. Sera ya elimu itaondoa biashara katika elimu. Napenda niwape mwongozo nyie, kazi uliyoibeba hii ni kubwa. Je, unaweza ku-summarize hapa kusema kwamba maneno mazuri waliozungumza walimu hapa, wataalam wa elimu wamezungumza kwamba kilichotua ni kuondoa ile taasisi ya elimu ya kutengeneza mitaala ya walimu wakaenda wakatupatupa, ndiyo tulipoangukia. Ina maana mnakwenda kufuta au unaweza kutamka hapa ukasema tangu leo tumeondoa biashara kwenye akili za watoto wa watu? Nilikuwa nawapa angalizo hilo. (*Makof!*)

Lingine, mimi nilisoma kilimo. Nenda nyumbani kwangu kote, nina kijumba Dar es Salaam nafuga ng'ombe, hata mama haniulizi unga, anauza maziwa anatumia. Kijijini kwangu niliko huko mimi ni mkulima kweli kwa sababu ya elimu ya kilimo. Hivi kweli mtu aliyeondoa somo la kilimo akaondoa somo la michezo, hatuna Filbert Bayi, alitufanyia jambo la busara? Hakutudhoofisha? Ina maana nyie mnaobeba jukumu hili mnakwenda kurekebisha haya? Mnaweza kutamka hapa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nimeyasema haya kwa sababu tunawategemea watu hawa waweze kutupatia kitu ambacho kimenyooka, tusiuziwe mara ya pili. Lakini liko suala lingine muhimu katika kuondoa udhaifu katika sekta ya elimu, ni wadau wa sekta ya elimu. Wako wadau watano au sita wa haraka haraka ambaa ni mzazi, mtoto mwenyewe, jamii iliyoumzunguka, shule kwa kumaanisha mwalimu, vifaa vyaa kufundishia na miundombinu. Ina maana unaposema unaondoa udhaifu wa elimu na hivi ndiyo vinachangia kwenye udhaifu wa

elimu. Jukumu mnalokwenda kubeba linakwenda kukidhi hayo na linakwenda kuchambua hayo.

Nimeisoma sana na nilijandaa sana kuichangia kwa vyovyote vile hoja ya Mheshimiwa Mbatia. Nachelea nisingeliomba turudi tukiwa na matatizo haya ambayo tunaendelea kushuhudia elimu ikiendelea kudondoka kwa sababu hakuna mzazi yejete ambarage anekubali kuona mwanaye anapata elimu isiyo bora. Narudi kwa wenzangu waliosema kwamba mtupe *time frame work* kwamba hili linafanyika lini? Hili suluhisho linakuja lini? Kwa sababu kama mambo siyo sawa leo, basi nani anakubali mwanaye akae shule ambayo mambo siyo sawa? Ni kana kwamba wanakwambia dawa zilizoko hospitali siyo nzuri, nani atakubali kupeleka mtoto wake hospitali kama ingekuwa hospitali.

Mheshimiwa Spika, maeleo aliyotoa Mheshimiwa Mbatia ni maeleo mazito, lakini mengine yana ushahidi wake wa wazi na mimi niungane na wenzangu: Je, wale waliowalisha yale yasiyostahili watoto wetu, wanachukuliwa hatua gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Mbatia pale amekuja na toroli la vitabu, amekuja na maeleo kuonyesha umakini kwamba kweli leo hii tunakwenda kufanya kazi, muanze kuwachukulia hatua na tunapowachukulia hatua tutangaze. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa maneno machache hayo, naunga mkono hoja ya kuimarisha Sekta ya Elimu kwa kuondoa huu udhaifu ambao Watanzania wanaujua na Waheshimiwa Wabunge wameuainisha zaidi na Serikali yangu imeashiria kwamba inakwenda kuondoa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja muhimu sana aliyoleta mwenzetu Mheshimiwa Mbatia katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nina mengi ya kuongea, lakini nashukuru kwamba kila Mbunge anajua matatizo makubwa yaliyoko katika Sekta ya Elimu hapa nchini na ndiyo sababu katika kila bajeti ndani ya Bunge lako Tukufu kwa muda wote niliokaa katika Bunge, Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiongea kwa masikitiko makubwa kuhusu mfumo, kuhusu maudhui ya elimu yetu hapa Tanzania na nini hatima ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba elimu ndiyo kila kitu, elimu kama alivyosema Mheshimiwa Mbatia, *nim-quote*, ndiyo moyo.

Mheshimiwa Spika, ndiyo sababu Waziri Mkuu wa Malaysia wakati huo alipoulizwa vipaumbele vya nchi yake alisema kipaumbele cha kwanza ni elimu, cha pili ni elimu na cha tatu ni elimu. Ndiyo sababu tunaona Malaysia sasa hivi imefika mbali sana wakati kipindi tunapata uhuru tulikuwa *almost the same*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nielezee masikitiko yangu kwa jinsi ambavyo Wizara ya Elimu imekuwa ikiporomosha au ikileta matatizo katika nchi yetu. Wote tunajua kabisa ni wapi tumetoka, ni wapi tunakwenda tukianzia katika suala zima la watu wanaojua kusoma na kuandika. Tumelisema mara nyingi na inatia aibu kwamba Tanzania nchi ambayo ilikuwa mstari wa mbele kwa kuwa na watu walioelimika, wanaojua kusoma na kuandika, lakini hivi sasa zaidi ya asilimia 30 ya Watanzania hawajui kusoma na kuandika. Hali hii inatokana na ukweli kwamba watoto wanasona Darasa la Kwanza mpaka la Saba wanamaliza hawajui kusoma wala kuandika! (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, haingii akilini mtoto ambaye siyo taahira, anakaa darasani miaka saba, anaondoka hajui kusoma wala kuandika, halafu leo tunasema hatuna matatizo katika elimu. Kwa kweli hiki ni kitendawili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba matatizo ya elimu siyo tu katika Shule za Msingi, lakini kama ambavyo tunajua siku za nyuma, mtoto alikuwa akiingia darasa la kwanza anaanza na kitu kinachoitwa *three K's*, yaani Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini shule zetu sasa hivi mtoto anaingia Darasa la Kwanza anaanza na zaidi ya masomo saba, wote wale waliosoma maendeleo ya mtoto, saikolojia ya mtoto, mtoto anapozaliwa ubongo wake unakua kiasi gani? Mtoto ubongo ule unakua taratibu sana. Kwa maana hiyo, ni lazima mtoto afundishwe kuendana na umri wake.

Mheshimiwa Spika, nisemee kwenye mitaala. Wote tunajua kwamba ni kweli tuna mitaala, lakini mitaala hii na mihtasari inayotengenezwa na watu.

Ni jambo la kusikitisha kuona kwamba Maafisa Elimu ndio wanaokwenda kupewa semina kuhusu mitaala wakati wanaokwenda kufundisha ni walimu. Matokeo yake walimu wanapelekewa mihtasari na mitaala ambayo wao wenyewe hawaijui, hawajashirikishwa toka mwanzo.

Kwa mfano, sasa hivi tumekuwa na somo la *TEHAMA*, walimu wetu wengi hawaijui hata hiyo *TEHAMA* inakwendaje, inafundishwaji lakini wanatakiwa wawafundishe watoto *TEHAMA* tena toka Darasa la Nne. Tunakwenda wapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie tu kwamba matatizo haya yamefanya watoto wetu wafeli mitihani, na hapa labda nielezee tu kwamba, ukichukua shule za sekondari za Serikali na sekondari za binafsi utaona tofauti kubwa. Sasa tunajuliza, Wizara hii inachukua hatua gani?

Mheshimiwa Spika, ni matokeo ya Kidato cha Nne mwaka 2011 yanaonyesha wazi kwamba zaidi ya asilimia 51 katika shule za Serikali walipata *division zero*. Watoto hawa wanakwenda wapi? Ukilinganisha na watoto wanaotoka shule za binafsi ni asilimia 28 tu walipata *division zero*. Kwa hiyo, unaona wazi. Ukiangalia na *division one* kwa mwaka huo, shule za Serikali walikuwa *0.5 percent*, wakati wa shule za binafsi walikuwa *3.5 percent*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ule ufaulu tu toka *division one* mpaka *three* kwa shule za Serikali ilikuwa ni asilimia saba tu, wakati shule za *private* ilikuwa zaidi asilimia 24. Kwa hiyo, unaweza ukaona kuna tatizo kubwa sana na la msingi. Mimi nadhani pamoja na kwamba hoja ya Mheshimiwa Mbatia inasema kwamba, Kamati Teule isiundwe. Lakini kwa kweli kulikuwa kuna haja kubwa sana ya kuunda Kamati hiyo ili iweze kwenda kufanya mambo vizuri kwa sababu tunajua kabisa ripoti za Kamati Teule zina kazi nzito na zinakuwa za maana.

Mheshimiwa Spika, nazungumza hili kwa sababu ni kweli kwamba Serikali imesema itakwenda kufanya, lakini Serikali hii hii miaka yote imekuwa ikiambiwa na matatizo makubwa katika Wizara haijafanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ushahidi upo wa kutosha. Jana tu wakati imeletwa hoja ya Mheshimiwa Mwigulu, Waziri amekiri ni ripoti ngapi zimepelekwa Wizarani za kuboresha, lakini mpaka leo hazijafanyiwa kazi. Leo hii tunaendelea pamoja na kwamba udhaifu umeonekana wazi wazi na Waheshimiwa abunge wote bila kujali itikadi wanaona kuna udhaifu, lakini tunaipa Serikali ile ile iende ikaboreshe wakati Serikali hii hii, Wizara hii Mawaziri ni wale wale, wamepewa

hii kazi walikuwa nayo siku nyingi, wanaona kabisa upungufu mkubwa ndani ya Wizara, hawachukui hatua, leo hoja inaletwa ndiyo wanasema watachukua hatua. (*Makof*)

Sasa kwa kuwa Kamati Teule haikuruhusiwa na kwa kuwa Wizara imekiri itakwenda kufanya hii kazi, tunataka tujue Mheshimiwa Waziri wakati ana *wind-up* atuambie ni lini wataboresha? Kwa sababu hali ni mbaya, Wizara iko /CU, ni lini wataboresha hali hii ili elimu ya Mtanzania iwe bora? Suala la kuwa na shule nyingi wala siyo hoja ya msingi. Tunachokitaka sisi ni ubora wa elimu hapa nchini. Kwa hiyo, nilikuwa namtaka kabisa Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini, na haya maboresho ni makubwa sana, kwa sababu ni kila mahali, hakuna mahali utagusa ndani ya Wizara ya Elimu ukute hakuna tatizo.

Kwa hiyo, tunataka kujua ni lini atahakikisha kwamba haya matatizo yote yaliyoorodheshwa na Mheshimiwa Mbatia na hayo mengine ambayo wanayajua wao, watayarekebisha ili mtoto wa Kitanzania anapokaa darasani miaka saba atoke kweli ni mtoto ameiva, anajua kusoma, anajua kuhesabu ili kuondoa Taifa hili katika aibu, ambapo tumeonekana wazi watoto wanamaliza shule wamefaulu lakini hawajui kusoma, hawajui kuandika? Tunapeleka wapi nchi? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza ni suala la walimu. Mimi naamini ni mwalimu na ninajua Wabunge wengi hapa ni walimu. Elimu yoyote ni mwalimu hata tungekuwa na madarasa mazuri namna gani, tungekuwa na vitendea kazi vizuri namna gani, kama hujaboresha maslahi ya mwalimu, ni bure. Ndiyo sababu tunaona wazi kwamba sasa hivi walimu ni kama vile wako kwenye mgomo baridi. Watoto wanafundishwa mambo ambayo ndivyo sivyo. Mtu anaambiwa Mlima Kilimanjaro upo Mbeya, mtoto yule anakuwa na akili ile ile. Kwa hiyo, mimi nadhani ni lazima tuboreshe maslahi ya walimu, bila hivyo elimu yetu itaendelea kuyumba. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, labda nimalizie kwa kusema kwamba elimu yetu, kuna huu wanaoita kwa Kiswahili mwamaruwaza au *paradigm shift* ambao kwa kweli umeleta matatizo makubwa kama alivyosema, hii kubadilisha mitaala ni tatizo na ni lazima wale wanaohusika ambao ni walimu washirikishwe kwa kina.

Mheshimiwa Spika, la mwisho nataka kuzungumzia ni suala zima la kitengo cha ukaguzi. Wamesema wengi na naomba nirudie kwamba Kitengo cha Ukaguzi ni lazima kiboreshwe kipewe fedha za kutosha. Wakati wa bajeti nilizungumza kwamba, haiingii akilini, Kitengo cha Ukaguzi ambacho hiki ndicho kinachoonyesha ubora wa elimu, lakini kitengo hiki kimeachwa kama yatima, Kitengo hakina pesa, Mikoa mitatu, kanda; mratibu wa kanda anapewa Sh. 2,500,000/= kwa mwaka kwa ajili ya Mikoa mitatu. Hili kwa kweli ni jambo ambalo haliwezekani.

Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake wahakikishe kwamba masuala yote ambayo Wabunge wanayasema ni ya kweli, yanaonekana na ni lazima wayatafutie ufumbuzi. Vinginevyo, tunakopeleka nchi yetu tutakuwa na Taifa la watoto ambao hawajui kusoma na kizazi hicho kitapotea na wa kulaumiwa tutakuwa ni sisi. Hatutaki kulaumiwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makof*)

SPIKA: Naona kwa sababu tumekuwa na muda mfupi, nafikiri tutaendelea kujadili halafu kesho asubuhi atapewa Waziri wa Elimu dakika 15 halafu mtoa hoja saa moja kabla hatujaingia hoja nyingine. Kwa hiyo, nawaita Mheshimiwa Akunaay, atafuatiwa na Mheshimiwa Mendrad Kigola.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote, nashukuru Mwenyezi Mungu na pili nampongeza sana mdogo wangu Mheshimiwa James Mbatia kwa kuleta hoja muhimu sana katika jamii ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pia natambua mapendekezo yaliyopitishwa asubuhi ya leo ya kurekebisha hoja hii. Kama walivyotangulia wazungumzaji waliotangulia, hoja inajulikana na Tanzania nzima inafahamu udhaifu ambaao upo ndani ya elimu na ishara zote zinajulikana. Mimi nizitamka chache ili nibakize muda mkubwa wa kuzungumzia jinsi Serikali inavyotazamia kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, ni ushahidi mkubwa hapa nchini kwamba matatizo yote ya elimu sasa hivi yametokana na sera ambayo imekaa zaidi ya miaka 18 bila kutazamwa upya. Ukiangalia vilevile hakuna muda mwinge ambaao umetumiwa na Serikali kuona kwamba matatizo yaliyoletwa na wananchi yatatatuviwa. Kwa mfano, *issue* ya wanafunzi wa darasa la kwanza kupewa masomo zaidi ya matatu badala ya kufundishwa kusoma, kuandika na kuhesabu, wao wanaletewa kupewa Stadi ya Kazi na Uraia. Hii ni kumwambia mtoto aliyezaliwa aanze kutembea badala ya kutambaa.

Mheshimiwa Spika, katika marekebisho yaliyofanywa, Serikali inakubali mambo yote ilioletwa kwenye hoja binafsi. Sasa naijiliza, kama alivyouliza Mheshimiwa Mwijage: Je, Serikali inataka kusema kwamba iko tayari kwenda kutatua matatizo yote ambayo inaikumba Sekta ya Elimu katika nchi hii ikiwa ni pamoja na tatizo tuliozungumza jana la kukosekana pesa ya Mfuko wa Mkopo wa Elimu ya Juu ambayo ni asilimia 80 ya OC ya Wizara ya Elimu? Je, inajumuisha pia matatizo ya kuwalipa walimu ambaao kwa muda mrefu sana wamekuwa wakidai fedha: Je, itaondoa matatizo yakutokuwa na vitabu vya kurejea mashulenii katika muda ambaao umeelezwa katika hoja hii? Isije ikawa Serikali inaleta marekebisho ya hoja ili hoja hii kwa leo hapa Bungeni iondoke, lakini tatizo liendelee kuwepo. Usemi huu unawekewa ushahidi kutokana na ripoti nydingi ambazo Serikali hajatoa ikiwa ni pamoja na Tume ya Rais iliyofanya utafiti juu ya elimu.

Mheshimiwa Spika, mimi nashangaa, kama kulikuwa na *technical point* katika ile hoja ya asubuhi ya kutokuweza kuunda Kamati Teule ya Bunge, kwa sababu hoja ni kubwa, basi Kamati ile ingepangwa katika hoja jinsi zilivoletwa, lakini kuizua ile Kamati ina maana kwamba tunazuia kufukua ambayo yamefichwa, ndio itasababisha tena kwa miaka mingine zaidi kama tuliyopita 18 hali hii iendelee, itatukwaza katika ushirikiano *East Africa*. Sisi tuendelee kuwa na elimu ambayo ni chini kama mzungumzaji aliyepeita sasa hivi waliosema kwamba asilimia 32.2 ya Watanzania hawajui kusoma na kuandika na *Form Four* wa kwetu wanafeli asilimia 51, hiyo ina maana ya kwamba Sekta yetu ya Elimu inatoa watu ambaao wameshindwa kusoma, watu ambaao wameshindwa kusoma ina maana hawatakuwa na stadi katika mafunzo wanayopata katika Vyuo Vikuu. Sasa hatutaingia katika soko la Afrika Mashariki, soko la Wataalam, soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba, Waziri wa Elimu atoe *time frame* leo, kwa kila *item* ambayo imetuletea tatizo hili kwamba, kuhusu sera, katika muda fulani tutaleta sera kuhusu walimu watalipwa na vitabu vitapatikana. *Time frame* ambayo haitachukuwa muda katika mwaka huu ili jamii ya Tanzania iamini kwamba tatizo hili linatatuliwa.

Mheshimiwa Spika, kama kila hoja binafsi itakayoletwa Bungeni, itaondolewa kwa kubadilisha hoja kwa kutumia Kanuni za Bunge, tutakuwa tunaishi kwa ajili ya Kanuni na siyo kwa ajili ya kutatua matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naomba niishie hapa. (*Makofii*)

MHE. MENDRAD I. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja muhimu sana katika Taifa letu la Tanzania. Kwanza namshukuru Mbunge, Mheshimiwa James F. Mbatia, aliyelela mada muhimu sana ambayo inaweza ikajenga Taifa letu.

Mhehimiwa Spika, ni kweli kabisa, katika mfumo wa elimu unaonekana unayumba sana. Tumeona mara nyngi sana tukisimama tunasema kwamba, elimu ya Tanzania imeshuka. Mimi usemi wa kusema kwamba, kielimu tumeshuka, huwa siupendi sana, kwa sababu, kila siku tunapoamka kuna vitu vinabadilika na elimu ndio inabadilika.

Mheshimiwa Spika, ukiangilia kwa mfano mitaala, kwamba sera iitungwa mwaka 1995, na kutoka mwaka 1995 mpaka sasa kuna mambo mengi sana yamebadilika. Nataka niseme kwamba katika mfumo, yaani ukiangalia mfumo mzima wa elimu, ni mfumo mzuri. Naweza niseme naishukuru Serikali kwa kuwa na mfumo mzuri, kwa sababu ukiangalia elimu tunayoiongelea hapa ni elimu ile ambayo unaanzia, Shule ya Awali, unakuja Shule ya Msingi, unakuja Sekondari na Chuo Kikuu. Sasa ukiangalia mwanafunzi anapofanya mitihani ya kuingia Kidato cha Nne, au anafanya mitihani ya kuingia Kidato cha Sita, halafu tunasema kuna wanafunzi hawajui kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Spika, mimi naona kama ni aibu kubwa ambayo Wizara ya Elimu inatakiwa kuiangalia kiundani. Inawezekana kuna watu wanamaliza Vyuo Vikuu wanakuwa siyo wataalam. Kwa sababu hiyo, kama unaweza ukampata mtu anayemaliza Shule ya Sekondari hajui kusoma na kuandika, anafika Kidato cha Pili, hii inapelekeea kwamba hata Vyuo Vikuu tungefanya *assessment*, wale wataalam ambao tunao wanawenza wakawa hawana ujuzi kamili.

Mheshimiwa Spika, katika Taifa lolote lile ambalo linapiga hatua, lazima liimarishe Wizara ya Elimu. Bila kuimalisha vizuri Wizara ya Elimu, kutatua zile changamoto ambazo zipo, hata tukitengeneza sera za namna gani, hatutafika mahali popote. Tunatakiwa sasa hivi, kwa sababu sera zipo, na hatuwezi kusema elimu inaanza hatuna sera. Mimi nakumbuka miaka ya nyuma, tulikuwa na uhaba wa Walimu na Vitabu vilikuwa havipo.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka wakati namaliza Darasa la Saba, katika darasa lile sikumpata mtu ambaye hajui kusoma na kuandika. Siku hizi ukitaka kuangalia, unaweza ukaona kwamba Serikali imejitahidi sana kujenga hizi Shule za Kata. Hiyo naipongeza ni kutanua wigo mpana wa elimu.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo makubwa yako pale. Kwa mfano, vitabu vya kufundishia mashulen, havipo. Sasa kama hakuna vitabu mashulen mwanafunzi atajuaje kusoma na kuandika? Kitabu kile ndicho kinachompelekea mwanafunzi ajue kusoma na kuandika. Sasa nataka niseme kwamba, katika bajeti tunayoitengeneza ya Elimu, lazima tuipe kipaumbele, iwe bajeti kubwa inayotosheleza ili waweze kutayarisha vitabu na vipelekwe katika mashule yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ni aibu kubwa sana, mwalimu anaingia darasani anafundisha, anawaona wanafunzi hawana vitabu, kwa hiyo wanafunzi wanategemea mwalimu aandike ubaoni, ndio wajue kusoma na kuandika. Hiyo itakuwa ngumu sana. Tukiangalia kila darasa sasa hivi, idadi ya watoto inaongezeka. Unaweza ukaona darasa moja lina watoto zaidi ya 50, mpaka 60. Sasa wanafunzi 60 kuwa-*handle* mle darasani na hawana vitabu, inakuwa ni ngumu sana kujua kusoma na kuandika, yaani *possibility* ya kutojua kusoma na kuandika itakuwa ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, nataka niishauri Serikali, kwa sababu hata tukisema tunaunda Kamati, matatizo ndiyo hayo yatakayokuwepo, wala haitasaidia kitu. Ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba, katika bajeti inayokuja ya mwaka 2013/2014, lazima ilenge kutatua ununuzi wa vifaa mashulenii. Hiiyo itatusaidia sana. Sasa hivi vitabu kule mashulenii havipo kuanzia Shule ya Msingi mpaka Sekondari. Tukiboresha kwenye vitabu, kuna Mbunge mmoja ameongea vizuri sana kwamba sasa hivi watunzi wa vitabu ni wengi, lakini kila mmoja anatunga kwa mtazamo wake.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna utandawazi, watu wengine wanasoma kwenye *internet*, wanasoma sehemu mbali mbali, wana-copy. Sasa unaweza ukachukuwa ambao siyo mfumo wa kwetu, sisi tuna *system* ya kwetu. Sasa tunatakiwa tuwe na *system* moja. Wizara ya Elimu lazima iwe na *system* kama ile ya zamani. Kwa mfano, unaweza ukaona kitabu kimoja, kinatumika katika Shule ya Sekondari, lakini ukienda labda kwenye *private school*, unaona tofauti.

Kwa mfano, hizi *International Schools* au *English Medium Schools*, ukilinganisha vitabu vya *English Medium Schools*, halafu ukaangalia na shule za kawaida ambazo tunazo, unakuta kuna utofauti. Sasa ule utofauti ndiyo unaleta mchanganyiko wa elimu.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba, Serikali sasa hivi lazima tufikie mahali tubadilike, tuangalie mfumo unakokwenda. Tunaposema kwamba mtu anasoma na ameelimika, ameelimika vipi? Nakumbuka miaka ya nyuma viwanda vilikuwa vinakwenda vizuri sana, kwa sababu watu walichokuwa wakisisoma, walikuwa wanakwenda ku-*apply* kwenye viwanda. Sasa hivi viwanda vingi sana vimekuwa kwa sababu wataalam ambao wanatoka hapa hatuwapati. Sasa utasemaje viwanda vinainuka wakati hawa wataalam wenyewe hawawezi ku-*apply* ile *knowledge* waliyofundishwa Vyuo Vikuu?

Mheshimiwa Spika, ukitaka kuangalia, tuna *engineer* wengi sana, lakini: Je, hawa *engineer* walichosomea ndio wana *apply* kwenye viwanda vyetu? Sasa hivi Taifa letu limeingia sehemu kubwa sana. Unaweza ukaona wataalam wengi wanajikita kwenye masuala ya omnia omnia, mtu anakaa anaandika *proposal* apate msaada fulani au utaalam fulani. Wataalam ni sisi wenyewe, inabidi tutumie elimu ambayo tumepeewa, kama hatutatumia elimu yetu, maana yake, kila kitu, chochote ambacho tutakuwa tunapewa, inabidi tutegemee wataalam kutoka nje. Jambo hili lita tu-cost sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niishauri Serikali, kwanza kabisa tuiamini elimu yetu, na tukishaamini tuuitumie. Lakini tukisema kwamba tunakosoa mfumo ambao tunao, na huu mfumo ambao tunao tunapata elimu: Je, tunaitumiae elimu hii ambayo tunayo? Hilo ndiyo litakuwa suala la msingi sana. Huwezi ukawa unakosoa kitu halafu huwezi kutumia mfumo uliopo, badala yake unaanza kulalamika. Hivi tutalalmika mpaka wapi? Ndiyo maana kila kitu tunakuwa tunaomba, hatutumii elimu hii.

Kwa mfano, ikienda kule kwa walimu, bahati nzuri Mbunge mmoja ameongea vizuri sana kwamba, ukimwandaa Mwalimu vizuri anatoa wanafunzi wazuri.

Sasa kwa mfano hii mitaala inabadalika, lakini walimu wake wanabadilika? Ndiyo suala la kujuliza. Walimu inabidi wawe wanapelekwa kwenye kozi fupi, kwani Mwalimu anamaliza Shule au anamaliza Chuo na anakaa miaka 10 mpaka 20 bila kwenda kozi hata siku moja na mitaala inabadilika mara kwa mara, unategemea huyo Mwalimu atatoa kitu kizuri? Atatoaje kama hajapelekwa kozi? Walimu lazima wawe wanapelekwa kozi kila baada ya miaka kadhaa.

Serikali itengeneze utaratibu, walimu wetu wawe wanapewa kozi, kwani bila kupewa kozi, huo mtaala unaobadilisha ata-*apply* vipi?

Mheshimiwa Spika, naona hili haliongelewi! Lazima Serikali hapa iangalie, siyo suala la kubadilisha mitaala. Suala hata la kubadilisha walimu vichwa vyao, kwamba je, wanaendana na mitaala inayobadilika? Walimu wengi sana, wengine karibu wanastaafu hawajawahi kugusa kozi hata moja. Kuna kozi nyingi sana zinafanyika. Hata kwetu sisi Wabunge, tunakaa muda fulani, unakuta kila baada ya muda tunapewa kozi, na tunaelimishwa mara nyingi. Lakini ni mara ngapi walimu wanaelimishwa? Walimu wale hawaelimishwi, halafu tunasema elimu inashuka. Kwa nini isishuke kama humwelimishi Mwalimu?

Mheshimiwa Spika, kupata cheti siyo elimu. Mwalimu yejote anaweza akapata cheti, lakini kuna mabadiliko ya kila siku. Kila siku tunapoamka, ulimwengu unabadiilika. Sasa kama watu hawapewi kozi inakuwaje? Kozi lazima itolewe kwa Walimu kulingana na mitaala inavyobadilika kila siku. La sivo, tutakuwa tunalamika kila siku. Bahati nzuri, nimeona hata wataalam ambao wako nje ya shule, ambao sio wataalam hili ni tatizo la kozi. Labda nilete mfano mzuri sana; sasa hivi tumeingia masuala ya *system* mpya, masuala ya ving'amu, masuala ya *TEHAMA* kutoka dijitali kwenda analogia. Lakini ukitaka kuangalia bado vinatusumbua, kwani ile elimu tunayo-*apply* kwenye ufundi bado siyo elimu inayotakiwa. Hivyo ving'amu vyenyewe vinaanza kuzima. Tanzania nzima sasa vinazima, tunakosa hata kuangalia mpira, hatuna wataalam wanaoweza kuleta kitu kinacholingana sawa na watu wa Ulaya.

Mheshimiwa Spika, wenzetu Ulaya kule wakitangaza kitu, wana-*apply* elimu yao, unaweza kukuta siku hiyo hiyo kitu kiko-*smart* kwa sababu wanaelewa wanafanya nini. Sasa sisi kitu kidogo, *consultant*; kitu kidogo, mtaalamu kutoka nje; sijui nini, mtaalam kutoka nje! Bado elimu ambayo tunapewa hatuitumii vizuri.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba, sasa elimu lazima izingatiwe vizuri na ifuatiliwe vizuri. Lakini kitu kikubwa sana ambacho napenda kusisitiza kwenye bajeti, ndiyo maana tumeona hata kile kitengo cha ukagazi hakifanyi kazi kama inavyotakiwa. Siyo kwamba hakifanyi kazi kwa kupenda, hakifanyi kazi kwa sababu bajeti ile hairuhusu.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wameshaongea kwamba, ni vyema kile Kitengo cha Ukagazi kipelekwe Halmashauri, hiyo ni sahihi kwa sababu, wakitegemea kutoka Serikali Kuu, kwanzza zile *funds* zinachelewa sana kufika. Unaweza ukaona kwa mwaka hawajafanya kazi kubwa. Mimi napendekeza kwamba, ili kuiboresha elimu, kitengo kile cha Ukagazi lazima kiimarishwe. Wale Wakagazi wawe wanapelekwa kozi kila wakati. Wengine wanafikiri ukagazi ni kwenda kumkagua Mwalimu anapoandika ubaoni, siyo hivyo. Tunakagua kuanzia majengo, mazingira kwa ujumla, na unaangalia Mwalimu anaishije na baadaye wanatoa ripoti. Hii itasaidia sana.

Sasa utaona kuna Shule nyingine zinakaa tangu zijengwe miaka ya hamsini mpaka leo hazijakaguliwa. Yaani hazijakaguliwa yale mazingira ya shule nzima. Utasikia Mkagazi alipita. Amekagua nini? Amekagua jinsi ya kufundisha, Mwalimu anafundishaje? Siyo hicho tu! Mwalimu lazima ukague, mwanafunzi anakaaje darasani? Unaweza ukaenda shule nyingine, kiti kimoja wanakaa watoto saba mpaka nane, watoto wamebanana pale, lakini kwenye ripoti haiandikwi vile, kwamba amekagua ameona watoto saba mpaka nane, inabidi viti pale viongezeke. Hawasemi!

Mheshimiwa Spika, wanasema tu maslahi ya Walimu, sijui Mwalimu hajafika darasani, sijui hajaanda mitaala. Lakini lazima tukague mazingira makubwa. Wale kwa sababu hawajapelekwa kozi, wafanye vitu gani, lazima watakatua kitu cha zamani ambacho

kimepitwa na wakati. Kwa hiyo, naiomba hii Wizara iangalie vizuri kile kitengo cha ukaguzi ili kifanye kazi vizuri. Vile vile katika kile kitengo, kuna mtu mmoja amesema labda Mtendaji anakwenda kukagua, ni kosa kubwa Mtendaji kukagua. Anakaguaje huyu Mtendaji? Ana elimu gani? Watendaji wengine wana elimu ya Darasa la Saba, sasa Darasa la Saba atakagua masuala ya sekondari na wakati hajasomea?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami nilishaanza kupata mashaka, lakini uliposema kuwa tunajadili muda wote, nikajua na mimi nitapata nafasi. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii vile vile kumpongeza mtoa hoja. Ni hoja ya msingi sana ambayo inawagusa Watanzania wote moja kwa moja. Nampongeza sana kwa sababu ameleta mjadala ambaao utasaidia kwa njia moja au nyiningine japokuwa mchakato wa sera upo, lakini utaleta chachu katika hilo. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, kuna usemi unaosema kuwa, elimu ni ufunguo wa maisha. Ni kweli kabisa elimu ni ufunguo wa maisha. Vile vile elimu ndiyo urithi pekee ambaao tunaweza tukawapa watoto wetu. Ni urithi wa uhakika kabisa kwa sababu urithi mwингine wowote ukimwachia mtoto, anaweza akanyang'anywa. Unapompatia mtoto elimu bora na siyo bora elimu, basi umempa urithi wa uhakika ambaao mtu hataweza kupasua kichwa chake na kuchukua elimu ambayo iko katika kichwa chake.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu ni muhimu sana katika nchi yetu tukawa na elimu bora. Ndiyo maana leo watu wamekuwa wakali kidogo katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia awamu ya kwanza ya Mwalimu Nyerere, malengo makubwa yalikuwa ni kupata msingi wa kujua kusoma na kuandika. Kwa kweli alifanikiwa katika hilo, lilikuwa ni lengo kuu na alifanikiwa. Katika awamu zilizofuata, walishindwa kuundeleza msingi ule; awamu zilizofuata, walikuwa wanatakiwa kujenga msingi ule wa nyumba ile ya elimu kwa kuweka kuta, madirisha na kumalizia kwa kufanya *finishing* ya elimu. Lakini kwa kweli kama tukisema hapa tuulizane nyumba hiyo hiyo inafanananje, sijui kama tutapata jibu la moja kwa moja. Kwa kweli hali sasa hivi inatisha, huo ni ukweli. Nashukuru Wabunge wote wamelikubali hili, hata upande wa Serikali wanalionia hilo. Kwa kweli itasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia sasa hivi elimu inarudi nyuma badala ya kwenda mbele. Ukiangalia mwaka 1980, watu waliokuwa hawajui kusoma na kuandika, lilikuwa ni asilimia 10, lakini hii leo kinachosikitisha, watu ambaao hawajui kusoma na kuandika, idadi inaongezeka siku hadi siku. Viashiria viro, kwa sababu kuna watoto ambaao wanakaa miaka saba darasani, lakini hawajui kusoma na kuandika. Hilo linasikitisha sana. Kwa hiyo, idadi inaongezeka na mimi nina ushahidi katika hilo.

Mheshimiwa Spika, kuna mtoto wa jamaa yangu ambaye alimaliza Darasa la Saba, kijini huko Pangani, akaja Dar es Salaam likizo, alimaliza mwaka 2011/2012, alipokuja likizo akafaulu. Alipofaulu huyu mtoto akalia sana, tukamwuliza, unalia kwa furaha au unalia kwa huzuni? Yule mototo hakutujibu. Tukajua anatania, mpaka usiku akakataa kula, ikabidi siku ya pili sasa mama yake mkubwa aniite mimi. Hebu njoo, wewe una uelewa mpana zaidi, mwulize mtoto kwa nini analia namna hii? Mimi nikatumia utaalamu wangu, nikamshawishi aweze kunieleza kwa nini analia na yeye amefaulu? Akasema mimi sijui kusoma wala kuandika. Sasa mbona umefaulu? Hataki kusema. Nikamshawishi sana, nikamwambia, sikiliza nikwambie,

hupelekwi popote, hebu niambie ukweli. Akasema sisi tumelishwa kiapo na tukapewa mtihani tukaambiwa tutafungwa, na kwa sababu ya *multiple choice*, akaweza kuandika zile A, B, C.

Kwa hiyo basi, nilimwambia nitalichukua, nitalifanyia kazi. Kweli nillifanyia kazi kwa uwezo wangu, tukamshawishi kwamba nenda tutakutafutia Shule za MEMKWA ili angalau uweze kusoma tu na kuandika. Huyu ni mtoto mmoja tu Tanzania. Sasa tuangalie na watoto wengine. Kwa kweli suala la elimu linauma hapa kwa sababu ni asilimia ya watoto wa Tanzania 80 na kuendelea ambao hawatapata elimu za aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, hatukatai Serikali inajitahidi katika hilo, lakini bado ni kwa sababu ni kujenga madarasa. Lakini madarasa yale yanahitaji yaende sambamba. Muda usipite sana, kwa sababu tunawakusanya watoto tunawaweka kule, lakini hakuna wanachokifanya. Miaka saba mtoto hajui kusoma na kuandika na anahudhuria kila siku.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hilo linasikitisha sana. Naomba Serikali waliangalie kwa macho yote. Kwa kweli kabisa mfumo uliopo haukidhi Soko la Dunia, kwa hiyo, kama kweli Serikali inafanya mchakato huo wa sera, basi ulete haraka ili tuweze kujadili iweze kutumika.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Tanzania bado tuna safari ndefu sana, kuelekea katika elimu bora na siyo bora elimu. Najua Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa ana mzigo mkubwa lakini unatakiwa ujitali katika hili. Kwa kweli Tanzania bado sana. Pia kuna kiashiria kingine cha Walimu. Walimu hawatoshi kabisa! Ushahidi ni kwamba kila mtu anapiga kelele Bungeni hapa, ni kweli kwa takwimu mlizozionyesha hapa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii - Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, inaonekana Vyuo vinaongezeka lakini bado Walimu hawatoshi kwa sababu hata wale ambao wanapata yale mafunzo, wengine wanakataa kwenda kufundisha. Mtu anafika anachukua posho ile ya kujikimu anaondoka. Ni kwa sababu ya mazingira mabovu ya wanakopangiwa. Hakuna nyumba za Walimu, mazingira Mwalimu akiangalia, marupurupu yake ni madogo. Kwa hiyo, wanachukua zile na kukimbia. Kwa hiyo, hata wale wanaopata hayo mafunzo kuwa wakasaidie, nao pia hawaendi kufundisha.

Naomba nikubaliane na mtoa hoja kwamba tatizo tulilonalo ni ubora wa elimu. Kwa kweli mfumo uliopo haukidhi. Mfumo huu ambao tukonao, ndio ambao ulipelekea kutumia kufundisha lugha mbili kwa Shule za Msingi. Kuna Shule za Msingi zinazofundisha kwa Kiingereza na Shule za Msingi ambazo zinazofundisha kwa Kiswahili. Hili amelisema Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa alilichangia. Kwa kweli mimi linanichanganya kweli kweli! Kwa sababu, hawa watoto wanaosoma hizo shule za umma ambazo wanatosoma kwa Kiswahili, akimaliza Darasa la Saba, anakuwa na kazi ya ziada. Akienda sekondari, hajui kile kinachofundishwa, anaanza kujifundisha lugha.

Naomba Serikali katika hayo ambayo yanafanya sasa hivi, hili waliangalie kwa umakini mkubwa sana. Watoto wanadhalilika katika hili la lugha ya kufundishia mashulenii, na ndio maana watu wenye uwezo wanakimbilia shule za *academy*, lakini walio wengi zaidi watoto wa maskini, watoto ambao sisi ndio tunawakilisha hapa wazee wao, wanapata elimu ambayo inawachanganya. Mtoto anapokwenda sekondari anachanganyikiwa, inabidi afanye nguvu ya ziada. Kwa wale wachache ambao ni *ma-genius*, wanawenza. Lakini leo jamani kuna ushahidi kabisa mtu anamaliza ni *graduate* hajui kitu!

Ukiangalia tatizo kubwa, msingi mkubwa ni lugha. Lugha Mheshimiwa Waziri inachanganya na ni lazima liwe ni suala la kitaifa. Kuwe na mjadala wa kitaifa ambapo liangaliwe kwa umakini, tutumie lugha ipi ili watoto wote kuweza kuwapeleka kwa usawa.

Katika suala hilo la lugha tunajua kuwa tunahitaji kutumia Kiswahili na tumelikubali hilo na Kiswahili sasa hivi kinakua; lakini tusikatae, hatuna njia ya kukikimbia Kiingereza. Hatuna! Sasa hivi kizazi ambacho kipo hapa katikati kwa kweli wanaathirika kwa hiyo lugha. Mtu akipata Mkutano wa kwenda nje ya nchi, Watanzania wengi wanakuwa mabubu. Mtu anakuwa hajui achangie nini. Lakini ana uwezo na anajua, lakini kutokana na lugha, inamnyima, inambana kuweza kujitanua na kuweza kuchangia vizuri. Kwa upande huo naomba sana suala hilo mliangalie.

Mheshimiwa Spika, nirudie tena, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia na ninaomba Serikali ushauri wangu uchukue. Lazima kuwe na muafaka wa kitaifa kuhusu matumizi ya lugha za kufundishia katika Shule za Sekondari na Shule za Msingi.

Mheshimiwa Spika, pia mitaala. Mitaala inaangaliwa, lakini inatakiwa kuangaliwa kwa umakini sana kwenye shule zote. Shule zote, bila kuangalia shule za umma na shule za *private*. Mimi naomba Serikali ijitahidi sana katika hilo kwa sababu suala la elimu linatugusa kweli kweli!

Hapa wakati nachangia, wananchi kwa kweli wanaangalia kwa umakini mkubwa, kuna mwananchi mmoja ambaye hata simjui, lakini ameweza kuniandikia *message* na akasema mnajadili Sera, wakati huku Ukerewe Shule ya Msingi Katende, Kata ya Bwisia Ukara imefungwa tangu tarehe 8 Januari kwa kukosa choo na hatima yake haijulikani na sielewi kama watafanya mtihani tofauti. Hao watoto wanakosa gani ukizingatia ni shule ya tangu mwaka 1953?

Mheshimiwa Spika, hii shule imefungwa kwa sababu ya choo. Kwa hiyo, kwenye suala la elimu kuna mambo mengi yanayochanganya. Najua uwezo wa Serikali, lakini basi ningeomba vitu viende sambamba ili kuweza kuwa makini. Wananchi waangalia, wanaona ambavyo tunajadili, lakini bado wanaguswa kwa sababu matatizo wako nayo kule.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa mara nydingine, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia katika mada hii muhimu. Kwanza nianze kwa kumpongeza mtoa hoja, lakini vile kwa fursa hii ya kujadili suala muhimu kwa Taifa letu kwa uwigo mpana wa Waheshimiwa Wabunge. Hapa kweli Bunge kimsingi lina utajiri, lina hazina ya maarifa kutokana na taaluma mbalimbali za watu, lakini na viwango vyta elimu vyta Waheshimiwa Wabunge kwamba wanaguswa na suala hili kwa sababu ni suala la msingi linalowahu wapiga kura, lakini vile linahusu hatima ya nchi yetu.

Kwa kiasi kikubwa, pamoja na hoja mbalimbali zilizozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kuhusu matatizo ya elimu, lakini suala lingine ambalo limechangia kuporomoka kwa elimu ni kuongezeka kwa idadi ya watu ambaao haikuendana na kupanuka kwa Miundombinu ya elimu na wataalam. Kwa hiyo, mifumo yote ya elimu kimsingi imezidiwa, japo nia njema ya Serikali ni kwamba kila mwanafunzi, kila kijana mwenye umri wa kwenda shule aweze kuingia shuleni. Ilikuwa ni nia njema, lakini miundombinu na wingi wa wataalam haukuweza kukidhi mahitaji hayo.

Sasa matokeo yake ni kwamba tumekuwa na kipindi cha mpito ambapo tuna vijana wengi wamemaliza shule lakini hawakupata elimu iliyo kamilifu na kwa kweli ni tatizo kubwa kwa sababu tutakuwa na kipindi cha rika la Watanzania ambaao elimu yao iko dhahifu.

Sasa hili ni tatizo, ni hatari kubwa na ningependa kuishauri Serikali ifanye hima sana kuziba pengo hilo, kuhakikisha kwamba kuna wataalam wa kutosha na nawapongeza Serikali kwa juhudhi wanazofanya kuzalisha walimu wa kutosha, lakini vile vile kujenga miundombinu.

Bado tuko nyuma sana. Ni mwaka huu, mwaka jana 2012 mwishoni, Mheshimiwa Rais ametoa tamko kwamba shule zote za Kata maabara zikamilike. Lakini kuna vijana wengi wamepita, wamesoma bila uwepo wa maabara. Sasa ni muhimu hili likatekelezwa na kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, suala kwa mfano la kuwa na walimu wazuri, inakuwa ni vigumu sana kuwa na walimu wazuri kwenye Shule za Vijiji kwa sababu hakuna makazi mazuri kwa ajili ya walimu, ndiyo matokeo yake unakuta walimu wengi wanakimbilia Mijini. Walimu wanatengeneza ndoa za bandia, hasa Walimu wa kike ili waweze kuondoka kwenye maeneo hayo. Sasa matokeo yake ni kwamba kunakuwa na uwiano ambao hauko sahihi sana kwa shule zetu.

Kwa hiyo, ni muhimu sana Serikali ikaliangalia hili kwa haraka sana hata bila kusubiri Sera. Lakini kingine, nafikiri Serikali hajatumia au hajafanya juhud ya makusudi kushirikisha wananchi, kiushirikisha jamii, Shule hizo za Msingi na za Sekondari zinasemwa ni Shule za wananchi, lakini ushiriki wa wananchi ni mdogo sana. Unakuta kwenye Halmashauri ya Wilaya kuna sekondari kadhaa, lakini unakuata hata Mkurugenzi hajawahi kuzitembelea shule hizo. Hawa wananchi wanashirikishwaje?

Afisa elimu, tumesema hapa, Wakaguzi hapa wamezungumzwa sana, hawajawahi kufika katika shule hizo, wananchi wanashirikishwaje? Kwa hiyo, nafikiri, hili lazima Serikali iangalie, kwa sababu wananchi wana mchango muhimu. Unakuta shule haina madawati, lakini kijji kikianza kuibua miradi, sasa hivi kuna uibuaji wa miradi; Shule ya Msingi, nyumba ya mwalimu siyo hoja inayoibuliwa, sasa matokeo yake unakuta mazingira ya kuwaandaa wanafunzi, mazingira ya kufundishia siyo mazuri sana. Kwa hiyo, ni muhimu sana ushirikishwaji wa wananchi ukapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, sisi Waheshimiwa Wabunge wengi tulioko hapa ni matokeo ya mfumo wa zamani wa elimu ambako kulikuwa na shule hizi zenye michepuo maalum. Hivi kulikuwa na tatizo gani hizi shule zikaondolewa? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mtoto anajengwa kitaaluma kuanzia utoto wake, mtu akishakuwa mtu mzima ni vigumu sana *kum-shape*. Wanasema, huwezi ukamfundisha mbwa mzee mbinu mpya. Mtoto unaanza kumjenga hulka kutokea utotonii. Sasa ni kitu gani kilharibika hata wakaondoa? Nakumbuka baba wa Taifa Marehemu J.K. Nyerere alisema, "Elimu ni Kazi", kwa hiyo, kuanzia Shule za Msingi vijana walifundishwa *skills* za maisha. Sasa baadaye zikaondolewa kabisa, ikiwemo na michezo. Sasa ni tatizo gani lilitokea mpaka wakaondoa hii?

Hii kimsingi ndiyo inatufanya Watanzania ukilinganisha hata na nchi nyingine za Afrika Mashariki, hatuwezi kushindana sana katika mambo mengi. Mhitimu wa Chuo Kikuu cha Kenya au Uganda ni shujaa sana kuingia kwenye mashindano ya kimaisha. Sasa hivi hata hapa nchini naangalia kwa Taasisi zinazotangaza mashindano ya kuandika michanganuo ili waweze kufadhiliwa, vijana wetu ni waoga sana kuingia huko. Wanaogopa kwa sababu hawakujengewa ushujaa huo. Lakini ushujaa unaanza kujengwa kuanzia umri mdogo. Kwa hiyo, ni muhimu sana vijana wetu wakaanza kufundishwa stadi za maisha kuazia utoto ili anavyokua mkubwa anakuwa kwanza ameshajitambua vipaji vyake na anajenga ushujaa wa namna ya kukabiliana na mambo mbalimbali.

Nchi hizi zinazofanya vizuri ambazo tunazitolea mfano, Japani Malaysia hata Marekani, waliwekeza katika *human resources*, waliwekeza katika utendaji kazi. Kwa maana hiyo, unakuwa na watu na jamii ambayo iko tayari kufanya kazi. Sasa hivi tunahangaika, tunapita kwenye maeneo yetu, Waheshimiwa Wabunge tunakuta watu wengi, vijana wengi wamekaa muda wa kazi wanacheza *pool*, wanafanya vitu ambavyo havina tija kwa Taifa hata muda ule

wa kuzalisha. Sasa hii yote ni kwa sababu katika makuzi yao, katika malezi yao, hawajapewa umuhimu wa kazi.

Kwa hiyo, ni muhimu sana mitaala yetu ikaangaliwa, mtakavyokuwa mnaendelea na hii Tume. Lakini bahati nzuri ni kwamba sasa itaaangaliwa na ndiyo mtazamo wa Wabunge wote kwamba hili suala la mfumo wa elimu liangaliwe vizuri kwa ujumla wake, basi liangaliwe namna gani tutaanza kujenga hamu ya kazi kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine nimekuwa nikijiliza, wakati wengi tunasoma, wengi wetu tulioko hapa hatukuwa na kitu kinaitwa *tuition*. Sasa hivi tuko karne ya *tuition*. Mtoto wa *nursery school* anakwenda *tuition*, Shule ya Msingi anakwenda *tuition*, hii ni matokeo ya nini? Yaani mtoto, ule muda wake wa kucheza ambako kucheza nako ni sehemu ya kumuimarisha kiakili, anatumia muda wote kuchosha na masomo na *tuition*. Hili limelalamikiwa kwa muda mrefu, na Wizara ipo inaangalia. Imekuwa ni mradi! Nafahamu ni mradi wa Walimu, lakini kwa sababu hawawajibiki mahali wanapotakiwa kuwajibika! Sasa Wizara inataka kuendelea na hii *tuition* mpaka lini? Nashauri wakati mfumo mzima unaandaliwa, basi hili suala la kuumiza vijana badala ya kuwajenga vijana wakakua vizuri katika ujumla wake, basi liangaliwe sana kwa sababu ni hatari vijana wanazeeka katika umri mdogo.

Kwa ujumla tatizo lingine ambalo nimekuwa nikiliona ni kwa sababu Serikali haiwezi ikakidhi mahitaji yote ya elimu na ndiyo maana ikafungua milango kwamba wawekezaji binafsi, waweze kufungua shule. Lakini pale Wizarani, utaratibu wa kutoa vibali shule zianze, yaani imekuwa na yenyewe ni biashara. Ni urasimu wa hatari sana! Mtu anaweza akawa na nia njema au Taasisi ina nia njema zinaanza kuwa na majengo, zina wataalam wako pale, lakini *process* ya kupata vibali kwa kweli sijui ni sawa na kuomba *certificate* ya kwenda Mbinguni!

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuangalia pale. Mheshimiwa Waziri, kitu kilichoko pale *team* yake haimsaidii vizuri. Lakini vile vile kwa mfano, sasa hivi kuna huu mfumo wa *TEHAMA*, kuna baadhi ya shule zinapewa fursa ya kujifunza masuala ya komputa na shule nyingine hazina fursa hiyo. Sasa tutakuwa na wanafunzi, vijana na Watanzania ambao wengine wameandaliwa vizuri kuja kuishi vizuri karne ya sayansi na teknolojia kuliko wengine. Kama mfumo huu wa kutumia *TEHAMA* katika nchi yetu unaruhusiwa, basi uruhusiwe kwa ujumla wake, siyo baadhi tu ya shule. Hasa za mjini ambako watoto wa wakubwa ndiyo wapo, shule za vijijini hazina nafasi.

Kwa hiyo, ningeomba sana kwa kweli niedelee kumpongeza sana aliyeleta hoja hii Mheshimiwa James. F. Mbatia. Lakini vile vile nishukuru kwamba, Serikali imekuwa tayari kuipokea hoja hii na hapo, niseme tu naipongeze kwamba ni ukomavu wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba inakubali hoja zinazokuwa na mashiko kama hii ili ziangaliwe kwa manufaa ya Taifa zima.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafafanua baadhi ya mambo, nimekuwa nikisikia habari ya takwimu hii ya Watanzania wasiojua kusoma na kuandika. Tulikuwa kama Taifa tumepiga hatua kubwa sana katika hili, sasa hivi naambiwa ni asilimia 30. Lakini takwimu hii ningeomba ithibitishwe kwa sababu hapa tunaongea na dunia nzima inatusikiliza. Ni kweli asilimia 30 ya Watanzania hawajui kusoma na kuandika? Maana yake tusije tukajiaibisha, tunajidhalilisha zaidi ya ukweli!

Mheshimiwa Spika, tungependa tu takwimu hii, kama ni ukweli, basi ijulikane na tujue hatua gani za makusudi zichukuliwe. Kwa sababu siyo dalili njema.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na nampongeza mtoa hoja. Ahsante sana.

MHE. BENARDETHA K. MSHASHU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii iliyo mbele yetu ambayo ni hoja juu ya udhaifu uliopo katika Sekta ya Elimu. Wote tunatambua kwamba elimu ndiyo uti wa mgongo wa maendeleo ya nchi yetu, na ili tuweze kupata maendeleo katika Sekta zote, iwe Miundombinu, iwe Afya, Klimo, tunahitaji elimu bora. Ndiyo maana napenda kuchukua fursa hii sasa kumpongeza Mheshimiwa aliyeleta hoja hii, Mheshimiwa James F. Mbatia, ameonyesha uzalendo wake na vile vile ametimiza wajibu wake kama Mbunge.

Tunakushukuru kwa sababu imezungumzia kitu ambacho kinamgusa na kinagusa hisia ya kila Mtanzania, ndiyo maana unaona Wabunge wote wakiamka wote wanazungumza wakikubaliana na wewe kwamba tunalo tatizo.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya elimu yanaweza kupimwa kwa *quantity*, yanaweza vile vile yakapimwa kwa *quality*, yaani yanaweza kupimwa kwa ukubwa na kwa ubora. Ni kweli Serikali imefanya kazi kubwa katika kupanua uwigo wa upatikanaji wa elimu. Takwimu tunazo, tumeona Shule za Msingi, Shule za Sekondari zilivyopanuka, Shule za Msingi zimetoka kwenye 10,000 zimekwenda mpaka 16,000, shule za sekondari zilikuwa 500 zimekwenda mpaka 4,000, Vyuo vya Juu vimeongezeka, sasa hivi tuna Shule za Msingi kila Kijiji, tuna Shule za Sekondari kila Kata.

Wanafunzi wanaohitimu kutoka katika Shule za Msingi, Shule za Sekondari na Vyuo na wao wameongezeka sana. Kwa kweli tuna sababu zote za kuipongeza Serikali kwa kazi hii kubwa na nzuri waliyofanya. Nina uhakika leo tungekuwa bado tuna Vyuo Vikuu vitano tungekuwa tunalalamika kwamba watoto hawapati elimu kabisa kwa sababu hakuna mahali pa kusomea. Sasa baada ya kuwa tumepanua huo uwigo wa upatikanaji wa elimu, kwa maana ya wingi, unabidi sasa Serikali ijkite katika kuangalia ubora wa elimu.

Mheshimiwa James Mbatia amezungumzia mambo ya Sera, Mitaala, Mihitasari pamoja na vitabu. Lakini hata hivyo vikishakuwa *in place*, havitoshi kuboresha elimu. Kuna mambo mengine tunapaswa kuyaangalia yapo mengi, lakini mimi nitazungumzia machache.

Kwanza kabisa, ukiangalia kwenye shule zetu kuna upungufu mkubwa wa zana za kufundishia. Kila siku hapa tunalalamika kwamba wanafunzi wanashindwa Hisabati, lakini Hisabati zinafundishwa bila zana. Lakini wote tunatambua kwamba hata Hisabati ina zana zake za kufundishia.

Zamani enzi zetu ufaulu katika somo la Hisabati ulikuwa mkubwa kwa sababu tulifundishwa, Walimu walitumia zana, tulisahihishwa na baada ya Mwalimu kukusahihisha ulikaa na wewe ukafanya masahihisho na Mwalimu alisahihisha tena. Lakini sasa hivi kwa sababu ya wingi wa wanafunzi katika darasa na upungufu wa Walimu, unakuta hata wanafunzi kazi zao hazisahihishwi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho kinachangia ubora wa elimu ni ufundishaji katika masomo ya Sayansi ambayo yanapaswa kufundishwa kinadharia pamoja na kwa vitendo, lakini unakuta shule nydingi hazina maabara.

Napenda kusikia wakati Sera ikitoka basi, itamke wazi kwamba shule zote za Sekondari lazima ziwe na maabara zote zinazohitajika yaani Maabara ya Jiografia, Biology, Physics na Chemistry. Hivyo kama wanafunzi wanafanya *practical* pale karibu tu na mtihani, Walimu wameanza kubunibuni labda ni maswali gani yatatokea, lazima ufaulu utashuka. Kwa hiyo, sera ihakikishe kwamba hayo mambo yanakuwa *in place*.

Mheshimiwa Spika, ubora wa elimu vilevile unapimwa kwa ufaulu wa wanafunzi. Mitihani ina umuhimu wake katika ubora wa elimu na katika ufaulu wa wanafunzi. Utaratibu wa sasa uliopo wa kuruhusu watoto walioshindwa kupanda madarasa unachangia kwa kiasi kikubwa kufifisha ubora wa elimu katika Tanzania. Mtoto anamaliza Darasa la Kwanza anashindwa kabisa mtihani lakini anapanda Darasa la Pili, au mtoto anashindwa kabisa mtihani Darasa la Tatu lakini anapanda Darasa la nne. Mtoto anakuwa *Form One* lakini anashindwa mwisho wa mwaka mitihani yote amepata *average 12* au sifuri lakini anapanda darasa linalofuata. Hata tukiweka haya yote na sera ikaja kama hatujaangalia umuhimu wa mitihani na ubora wa elimu unaopatikana utakuwa umeathirika.

Wote tunatambua kwamba watoto wetu siku hizi hawapendi kusoma hata kama Walimu waliwapa mazoezi wao wakitoka shulenii wanapitia *internet* kuangalia lakini akirudi nyumbani anakwenda kuangalia video, hawana muda wa kufanya yale mazoezi wanayopewa na Walimu.

Ninapendekeza kwamba wanafunzi wasipimwe kwa mtihani wa mwisho tu bali Walimu katika ufundishaji watoe mazoezi ya kila siku kama sisi tulivyofundishwa. Watoe mazoezi ya kila wiki na hayo yote yakijumlishwa ukute kwamba yale mazoezi yanachukua uzito fulani kwenye mtihani wa mwisho kama asilimia 40 na ule mtihani wa siku moja unachukua kama asilimia 60 ukizijumlisha hizo zote ndiyo tupime ufaulu wa mtoto. Kwa kufanya hivyo, watoto wetu ambao hawapendi kusoma wasasoma kwa sababu mitihani na mazoezi yatakuwepo kila siku na hapo tutaboresha elimu wanayoipata watoto wetu kutoka kwenye shule hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia Kitengo cha Ukaguzi. Hiki ndicho kitengo ambacho kinapima ubora wa elimu na ufundishaji na ufundishwaji wa kila siku shulenii. Naomba *ku-declare interest* kwamba mimi ni Mwalimu na tena nilikuwa Mkuu wa Shule. Enzi zetu kila wakati tulikaa tumejiandaa tukilogopa kwamba Wakaguzi wanaweza kuja *any time*. Kwa hiyo, Mkuu wa Shule alikuwa anahakikisha kwamba anawakagua Walimu wake na Mwalimu anakaa anaweka mambo yake sawa anahakikisha kwamba maandalio yake yapo sawa hata na mwanafunzi anaogopa kwamba Wakaguzi wanaweza kuja.

Tulihakikisha kwamba kila Mwalimu anakuwa na *continuous assessment records*, yaani anapokuja Mkaguzi ni lazima uonyeshe kwamba umeshatoa mazoezi mangapi katika muhula. Tulikuwa tunatoa mpaka mazoezi 10 au 20 kwa muhula mmoja kwa mwanafunzi na ndiyo maana wanafunzi walikuwa wanafanya vizuri. Hii ilitufanya wakati wote tuwe tumejiandaa. Sasa tukishakirudisha na kukiboresha kitengo kile ambacho kimekuwa *paralysed* sasa kitengo hiki kitakuwa kinafanya ukaguzi, hakikagui tu masomo ya darasani lakini pia kitakagua na *extra curriculum duties*, kitaangalia na mambo ya michezo shulenii, kitaangalia elimu ya kujitegemea shulenii, namna watoto wanavyofundishwa kutengeneza bustani na kadhalika.

Pia kitaangalia usafi wa shule kwani ukienda kwenye shule nyingine utashangaa zilivyo chafu. Itaangalia nidhamu ya wanafunzi na pia Wakaguzi wataangalia nidhamu ya wanafunzi na Walimu pia kwani siku hizi ni milegezo tu mashulenii. Pia wataangalia maandalizi ya Mwalimu kwenda darasani kufundisha kama: Je, Mwalimu anatayarisha *schemes of work*? Je, Mwalimu ameandika *lesson plans*? Wataangalia na *notes* kama zinaendana na *syllabus* na ile mitihani wanayotoa wanaitisha na hata zile karatasi za wanafunzi: Je, ile mitihani uliyotoa inaendana na *syllabus*? Kile kitu unachokipima ndiyo hicho kilichotarajiwa kwamba ukipime na wanaangalia namna tunavyotumia vitabu au wanafunzi wanavyofundishwa kutumia vitabu na ukamilishaji wa *syllabus*.

Sasa hivi kitengo hiki kama Waheshimiwa Wabunge wengi walivyosema, kimekuwa *paralysed*. Hivyo tungeomba pamoja na sera na vyote vitakavyoandaliwa, basi Kitengo hiki

kifufuliwe na kama hawana magari, wapewe; wapewe fedha za kutosha na vitendea kazi ili waweze kuzikagua shule. (*Makofi*)

Ndugu zangu, tunaweza tukayasema yote na tunesema juu ya mwanafunzi, lakini bila kumwangalia Mwalimu hatuwezi kupata elimu bora. Lazima motisha kwa Walimu iangaliwe upya na ikiwezekana kama *it is not too much* na yenyewe iingizwe kwenye sera kwamba ni lazima Walimu wa Tanzania wapate motisha na mishahara yao ilingane na hadhi ya taaluma yenyewe. Wote tunatambua kwamba tusingkuwa hapa kama isingkuwa ni elimu. Lakini anapokuja yule mtu aliyekupa elimu tunamsahau. Kwa hiyo, mishahara yao ipande na wapate posho ya kufundishia na wapate nyumba za kuishi na mengine mengi ili kusudi wapate moyo ule wa kuendelea kuifanya ile kazi yao. (*Makofi*)

Naomba Serikali kwenye bajeti ijayo watenge fedha za kutosha na nyingi kwa sababu haya mambo tunayopendekeza ni mengi sana. Tumesikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali tangu asubuhi, tumegusa sekta ngapi? Tumegusa nyanja ngapi? Tumesema mambo mangapi? Yanahitaji bajeti kubwa! Kwa hiyo, tuiombe Serikali, kwa sababu najua Mkoa kwenye mchakato wa bajeti sasa itakapofika kwenye elimu na mkijua kwamba tumesajua na tumeshaongeza wingi wa shule na kadhalika tunataka kuboresha sasa ubora. Mhakikishe kwamba mnatenga bajeti kubwa ya kuweza kuyafanya haya mambo makubwa tuliyoyapendekeza.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napendekeza na ninazidi kuwasitizia Wizara walete sera hiyo waliyosema mapema na mapendekezo ya Mheshimiwa James Mbatia yazingatiwe, michango mbalimbali ya Wabunge iweze kutiliwa mkazo, lakini kubwa mno ni kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii ikae chini na iangalie kwa kina kuboresha elimu siyo lelemama ni kazi kubwa na itachukua muda.

Kwa hiyo, waitake Wizara ya Elimu iainishe maeneo yote ambayo wanapaswa kuyagusa ili kusudi waweze kuboresha elimu. Waweze *ku-come up with a plan of action*, waweze kuonyesha *time frame* kwamba hiki kitu tutakuwa tumezikamilisha ifikapo muda fulani na maabara tutakuwa tumezikamilisha na kadhalika ili kila kitu kiwe *in place* na Kamati iweze kuisimamia vizuri Serikali na ikiwezekana kila tunapotoa taarifa humu Bungeni au hii Kamati ipewe kipaumbele au upendeleo maalum ili waweze kutoa taarifa angalau mara mbili kwa mwaka juu ya utekelezaji wa haya mambo ambayo Waheshimiwa Wabunge wanayasema.

Mwisho kabisa namalizia kwa kumpongeza kwa mara nyingine mtoa hoja, Mheshimiwa James Mbatia. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Msemaji wa mwisho ni Mheshimiwa Aliko N. Kibona.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kusema machache na kuchangia juu ya hoja iliyopo mbele yetu, katika kuangalia udhaifu uliopo katika Sekta ya Elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu ambao wamesema kwamba Mbunge mwenzetu Mheshimiwa James Mbatia ameleta hoja ambayo ikijadiliwa vyema ni ukombozi kwa watoto wetu na itatupelekea kwenda kwenye hali bora ya elimu na mustakabali wa elimu yetu kwa ujumla hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tangu mimi nimefika hapa na kabla sijaingia Bungeni nilikuwa nikisikia jambo ambalo siyo la kawaida likitokea huwa linashughulikiwa kama dharura. Hapa tulipofikia elimu yetu nilifikiri kwamba Mheshimiwa Waziri mhusika angetuambia au Bunge

lingeleta kwamba hili jambo tulishughulikie kama ni dharura. Watoto wetu mwaka 2012 walifeli sana *Form Four*, mwaka huu hali ni mbaya zaidi, huwezi kuamini kuna mzazi mmoja huko Mbeya anakataa mtoto wake asiende Sekondari. Kisa, mzazi ana uhakika mtoto wake hajui kusoma na kuandika. Hii inadhihirisha kwamba utafiti wa mwenzetu ni sahihi kabisa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa natembea mahali fulani kuonyesha jinsi gani mambo ambavyo hayajakaa sawa katika Idara au katika elimu yetu, nimewakuta watu wanasema mahali mtoto taahira amefaulu kwenda kwenye shule za vipawa maalum. Sasa huu ni mwendelezo wa vioja na vituko katika elimu yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi niseme kwamba tumejadili vizuri, wataalamu waliobobea katika mambo ya elimu wametoa michango mizuri, ninaamini Mheshimiwa Waziri wetu ameichukua. Mimi kila walipokuwa wanachangia nilikuwa namwangalia nakuta ana-note.

Sasa ushauri huo mimi napenda kuona atakapokuwa anakuja ku-*wind up* atuambie kwamba ni lini mwisho wa jambo hili utakuwa kwa sababu wakati mwingine ukipewa ushauri halafu ikapita miezi mitano au mwaka au miaka miwili hakuna kinachotekeliza, basi pia itakuwa haina maana.

Mheshimiwa Spika, udhaifu katika elimu ni mkubwa, lakini tuseme ukweli kwamba bajeti ya Elimu inachukua asilimia kubwa ya haya tunayoyaona. Lakini pia hiyo tulioambiwa kwamba ipo Sera ya Elimu ya mwaka 1995 mimi nashindwa kuelewa kwamba ndani ya sera hiyo ndiyo humo kwenye sera wamesema kwamba mithiani ya Darasa la Saba watoto wetu wachague A,B,C au D? Lakini pia najiuliza kwamba kwenye hiyo sera iliyopo sasa hivi ndiyo hiyo inayosema kwamba Waziri wa Elimu asiwe na madaraka ya kumwadhibu au kufanya jambo lolote kwa Mwalimu aliyepo kule kijijini? Hii ni kwa sababu Wizara ya Elimu Mwalimu ambaye yuko kwenye Halmashauri naona Ndugu yangu, Mdogo wangu, Mheshimiwa Mlugo anahangaika na Walimu, anakimbizana huku na huko, huyu hafanyi hiki, huyu hafanyi kile na kadhalika.

Wakati mwingine nasikia Walimu wanalamika wanasema anaingilia Wizara ya TAMISEMI. Lakini nashauri Mheshimiwa anayehusika katika eneo hili aliwekee nyota, Wizara ya Elimu irudi ijitegemee isiwe chini ya *TAMISEMI*.

Mheshimiwa Spika, Walimu wanateseka. Asubuhi nilikuwa naongea na Mwalimu wangu kule kijijini anasema lazima afanye mjadala na mke wake, wauze kuku ndipo akanunue chaki ya kufundishia. Hapo ndipo tulipofika! Ananiambia mwaka 2012 tulioumaliza shule yake imepata *capitation Sh. 200,000/=* kwa mwaka mzima. Haya mambo yanatisha! Haya mambo yanatisha!

Mheshimiwa Spika, zamani kidogo kulikuwepo na utaratibu ule wanaosema ni *Teachers Resource Centre*, zile zilisaidia. Wale Waratibu walikuwepo pale muda wote wa kazi, Walimu walitembelewa na kazi ilifanyika. Wenzangu wameongea kwa kirefu, wamezungumzia habari ya kukagua shule. Kule lleje Jimboni kwangu nilimsikia mwenzangu mmoja mteule alikwenda kule akawakusanya watu akihutubia akasema, ndugu wana lleje, siku za karibuni palikuwa na tatizo, sisi wenyewe tutajipanga turekebishe elimu lleje. Mimi nasema tatizo la elimu ni kwenye mfumo. Tatizo la elimu ni la kitaifa.

Naomba niungane na Wizara sasa kwamba Sera inayokuja ije haraka kama tulivyojadili umeme, tatizo lile la umeme tukasema jambo hili linaathiri maisha ya Watanzania na linaathiri uchumi wa nchi. Kwa hiyo, lile tulitengenezee utaratibu wa dharura tuweze kulitatua. Mpango wa dharura ukandaliwa. Hata hili kwa hakika lilipaswa kuandaliwa utaratibu wa kutatuliwa kwa namna ile ya dharura.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri, ametuhakikishia kwamba ameandaa timu ambayo italeta mapendekezo ya sera itakavyokuwa. Mimi naomba sera hiyo kwa kweli tutaisoma itupelekee kuondoa uozo na takataka ambazo Waheshimiwa Wabunge wameendelea kulisema tangu tulipoanza kujadili jambo hili.

Mheshimiwa Spika, siyo vyema nikaendelea kusema ambayo wenzangu wamesema. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, tusubiri sera ya wenzetu tuijadili kwa ajili ya mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha, lakini nina matangazo machache kama ifuatavyo:-

Kesho Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii watakuwa na shughuli ya uzinduzi wa mpangokazi wa pili wa kitaifa wa huduma za watoto walio kwenye mazingira hatarishi. Sasa uzinduzi huo utafanyika *Jamhuri Stadium* kuanzia saa tatu asubuhi na mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Sasa kwa sababu hii shughuli inaingiliana na shughuli za Bunge, hivyo basi, napenda kuagiza Kamati ya Huduma za Jamii ndiyo waende kwa sababu wenyewe hili suala la watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu lipo katika sehemu yao. Kwa hiyo, naomba wao waende na wengine tuje tufanye kazi.

Asubuhi nilighafiliaka kidogo kutangaza kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) - Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri alitoa taarifa hapa kwamba aliyekuwa Mbunge wa Siha kati ya mwaka 1995 - 2000 Mheshimiwa Elias Mikidadi Mossy alifariki jana jioni kutokana na ajali ya gari ambayo ilitokea eneo la Africana Dar es Salaam. Alikuwa Mbunge na wengine wengi wanamfahamu, lakini Waheshimiwa Wabunge wengine hawamfahamu. Basi Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amen.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa mchango wenu mzuri wa kuboresha namna ya kuweza kuisaidia Serikali kuingia katika kuondoa udhaifu uliopo katika mfumo wa elimu. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa majadiliano yenu, kesho asubuhi baada ya kipindi cha maswali tutamwita Waziri anayehusika ili aweze kusema kidogo kwani yeye ni mchangiaji, lakini mtua hoja Mheshimiwa Mbatia ndiye atakayepewa muda kwa mujibu wa kanuni ya 62(1)(a).

Kwa hiyo, sasa naahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 1.40 usiku Bunge lilahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa,
Tarehe 1 Januari, 2013 Saa Tatu Asubuhi*)

